# *Kwa Nini Sisi Si Madhehebu?*

Nimejaliwa kurudi mimbarani tena baada ya kama, nadhani, karibu kutokuwepo kwa muda wa miezi mitatu. Kindi wamekuwa na wakati mgumu, na mimi pia. Loo, nimeburudika, hata hivyo, sasa, na unajisikia sana kama kuingia katika ibada tena. Na tunatarajia kuanzisha juma hili lijalo, Jumatano hii ijayo usiku, kwa ajili ya u—ufunuo papa hapa Maskanini. Na kama Mungu akipenda, nimeninii kwa namna fulani, Bwana ameniahidi huduma mpya na ya namna nyingine. Na kama akifurahiwa kufanya jambo hilo, ninatarajia kuanzisha hiyo—hiyo aina mpya ya ibada juma hili lijalo, hapa Maskanini, kwa mara ya kwanza.

2 Halafu sina mikutano iliyopangwa, lakini ni Australia tu na New Zealand Januari hii ijayo. Halafu Ndugu Osborn anaomba mkutano wa pamoja ambao kwa namna fulani nilimwahidi hapa muda fulani uliopita, huko Tulsa, lakini baadaye kidogo, ila hatuna uhakika na huo bado.

3 Bila shaka lilikuwa ni jambo zuri, Ndugu Jeffreys, kupata kukupa mkono hapa nyuma, na pia kumsikia kijana wako akiimba wimbo huo, na wewe ukipiga kinanda. Kwa namna fulani ninapenda jambo hilo, baba na mwana. Hampendi jambo hilo? "Mlee mtoto jinsi impasayo." Hiyo ni kweli, Bw. Guenther, u—unajua ya kwamba jambo hilo ni kweli, ninyi nyote wawili. "Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee." Na hiyo ni kweli. Huenda kukawa na nyakati fulani atakapoiacha, lakini haitamwacha, unaona. Ita—daima itadumu naye. Hayo malezi ya mwanzoni na yo yote aliyofunzwa kufanya, bila shaka yata—yatadumu naye. Sasa hii ni . . .

4 Nilikutana na Ndugu Jeffrey huko nje, nami nikasema, "Ndugu Jeffreys . . ." Nikawaza, wajua, daima mimi hufurahi kumwona ye yote wa ndugu zetu wanaotutembelea amekuja, lakini ni usiku wa jinsi gani kwa ndugu kuja kututembelea! Huu kwa kweli ni usiku wa watu wanaohudhuria Maskanini, ni wa maombi tu, ufufuo huu, huu ndio usiku huo. Tunataka kuchukua usiku wa leo, na kesho asubuhi, na kesho usiku yale tu tunayoamini hapa Maskanini, ku—kuyarudia tena. Tuna mafundisho ya kipekee sana, ya kushangaza sana, lakini kwa njia yo yote, tunayakuta katika Biblia hii. Yanaonekana haidhuru kuwemo humo.

5 Na sasa kama kuna ndugu mgeni ama dada hapa ndani, ambaye ni mfuasi wa madhehebu fu—fulani, ama—ama haafikiani, akiwa ameketi ndani kusikiliza haya usiku wa leo, tunataka ujue ya kwamba unakaribishwa kabisa. Unaona,

unakaribishwa tu uwezavyo kuwa. Lakini sasa natumaini... Nasi tunafanya jambo hili kuwa kali sana. Kwa hiyo kama—kama inaonekana ya kwamba hukubaliani nalo, vema, sasa, wewe basi fanya jambo hilo kama ninavyofanya ninapokula sambusa ya matunda. Na wakati ninapokula sambusa ya tunda hilo, ambayo naipenda sana, daima mimi, wakati ninaponinii—ninapokula sambusa hiyo, ninapokuta mbegu, siitupi sambusa, ni—ninatupa mbegu tu na—na kuendelea tu kula sambusa. Kwa hiyo, ama kama vile kula nyama ya kuku. Sasa, ninyi nyote mnapenda nyama ya kuku, mnaona. Na unapokutana na mfupa, huachi kula, unauzunguka tu huo mfupa na kuendelea kula kuku. Vema, hivyo ndivyo mtakavyofanya usiku wa leo, ninayosema hapa, wewe unaninii tu...unapokula kitu fulani, unasema, "Sasa, mimi—mimi sininii tu... Ninaketi tu kwenye jambo hili kama Fundisho dogo la kanisa kwenye mikutano hii mingine mitatu inayofuata, wao kwa namna fulani wanarudia tu yale wao—yale wanayoamini, na kuyapitia."

6 Na njia pekee ambayo unaweza kumfanya mtu karibu aamini Hilo, ni kulishindilia sana mpaka itawabidi kujua ya kwamba jambo Hilo ndio kweli. Hivyo ndivyo tu unavyoweza kulifanya lishikilie. Na ni kama vile tu rafiki yangu, Bw. Woods ambaye nimekuwa pamoja naye, kama—kama ukipigilia tu msumari uingie nusu tu, na ubao umelegea wote, upepo utaupeperusha mara moja, lakini huna budi kuupigilia ndani na kuufanya ushike kabisa. Kwa hiyo sasa kama nikilifanya jambo hili kuwa gumu kidogo kwenye hizi sehemu fulani fulani, na kwenu ninyi wageni usiku wa leo mlioketi humu, si—sijaribu kuwakwaza, ninajaribu tu kulieleweshа kanisa hili yale tunayoamini. Wote wanaoelewa hilo vizuri sana, semeni "amina." [Kusanyiko linasema "Amina!"—Mh.] Vema, hilo—hilo ni sawa. Nami nitaliondoa hili mikononi mwangu. Na halafu basi—basi ninii...Wao wanaurekodi, na kadhalika, ili kwamba baadaye kama walitaka kujua basi yale tunayotetea hasa, na yale tunayoshikilia, kanda hizi zitaelezea. Nasi basi tunafanya jambo hili mara kwa mara, kwa maana kuna watu wapya wanaoingia na—na tunaendelea. Na sasa hatutaweza kupitia Mafundisho yote ya kanisa, lakini ni baadhi yake tu ambayo tunataka ku—kuzungumzia. Na sasa Jumatano usiku, hata hivyo, inaanza...

7 Sasa, Jumatatu na Jumanne, ninaenda zangu kuomba, nipate kuwa tayari kwa ajili ya ibada ya uponyaji. Nanyi mnaweza kupiga simu, ama po pote mtakapo, na kumleta mtu fulani mnayetaka, kwa ajili ya ufufuo huu ujao. Na, waambieni wasije wakiwa na haraka, sasa. Sio waje, waseme, "Vema, sasa nitaingia ndani kule haraka na kuombewa usiku wa leo, na kesho usiku yote yameninii..." Hufanyi hivyo. Ingia ndani usikilize kwa muda kidogo, kwa maana tunataka kuchukua wakati wetu na kulielezea Neno hilo vizuri sana hata Ibilisi hatapata chembe

moja ndogo ya nafasi ya kusogea kamwe. Na sasa wakati unapoachilia imani yako iende mpaka mwisho wake, mpaka uanze kuamini, ndipo uache dhamiri yako ya ndani ianze kutenda kazi, ndipo imani ya Mungu itaiunga mkono, ndipo utaendelea moja kwa moja. Unaona? Kwa maana imani yako haitafanya mengi; dhamira yako ya ndani haina budi kusogea kuelekea mahali imani yako inakoenda, ndipo basi imani ya Mungu inakuja nyuma yake na kuthibitisha yote. Mnaona? Lakini kama ni imani yako, "Loo, naam, nimefanya hilo sasa hivi"; na hata dhamiri yako ya ndani inazunguka inarudi hapa, ikisema, "Sijui kama itafanya kazi kwangu." Ha—haitatenda kazi papo hapo. Unaona? Kwa hiyo tunataka hii iwe ni ibada halisi ya uponyaji. Na kabla sijampata mtu ye yote kwenye vile vyumba na kadhalika, kwa ajili ya uponyaji, ama ibada hizi mpya, ninataka wafahamu bila shaka lo lote linalowaleta kule. Kwa hiyo kumbukeni tu, na mje mtutembelee, nasi tutafurahi kuwa nanyi.

8 Sasa, kumbukeni sasa, asubuhi, tutaendelea na Mafundisho ya kanisa, na kesho usiku vile vile. Sasa, mnakaribishwa kuja, na mtu ye yote anaweza kuja. Daima tunafurahi kumwona mtu ye yote. Lakini sasa huu usiku wa leo limeelekezwa moja kwa moja kwa watu ambao ni wa hapa Maskanini, ambao—ambao wamelelewa katika Mafundisho haya. Kwa kuwa, huko nje hudumani, kwenye viwanja vya uinjilisi, tunachukua tu Mafundisho halisi ya kimsingi ya kiinjilisti ya Maandiko. Lakini hapa Maskanini, tuna mawazo yetu wenyewe na imani zetu, kama—kama—kama kanisa, na hilo ndilo tutakalopitia usiku wa leo.

9 Na kabla hatujafungua Neno Lake lililobarikiwa, tafadhalini tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi.

10 Mungu Mwenyezi na mwenye nguvu, Ambaye, kabla ulimwengu haujaanza bado kuzunguka kwenye atomi ya kwanza, Wewe ulikuwa Mungu. Hujabadilika hata kidogo. Na wakati hapatakuwepo na atomi za kuushikilia tena, na hakuna ulimwengu mwingine wa kushikiliwa, Wewe utakuwa ungali ni Mungu. Wewe ni wa milele, na tangu milele, Wewe ni Mungu. Wewe kamwe hukuwa na mwanzo wa siku wala mwisho wa maisha, Wewe utakuwako daima. Na, Baba, Wewe ukiwa asiye na kikomo, nasi tukiwa wenye kikomo, basi tunaomba rehema Yako ya Kiungu, Mungu, tukitambua ya kwamba roho hii yetu itachanganyikana na Umilele kutoka katika kipindi hiki cha wakati kuingia Umilele. Kwa hiyo, Bwana, tuko hapa kuchunguza wokovu wetu, kuona jinsi tunavyosimama mbele ya Neno Lako, na kuona jinsi tulivyo katika ujuzi wetu. Je! tunaishi vile inavyokupendeza Wewe? Je! roho zetu zinashuhudia pamoja na Roho Wako? Na je! mafundisho yetu yanashuhudia pamoja na

Biblia hii? Na, Baba, jalia tuchunguze yote mawili, kwa makini, katika ibada hizi nyingine tatu zijazo. Tujalie, Bwana.

11 Mbariki mchungaji hapa, mashemasi, wadhamini, na wafuasi wote, watu wanaohudhuria kanisa hili. Tangu siku zangu hapa, Bwana, kuna wengi, wengi sana ambao hata sijui majina yao ama mahali wanakotoka, lakini nina hakika ya kwamba unajua yote kuwahusu. Nasi tuko hapa kwa kusudi lile moja usiku wa leo, Bwana, kufanya ushirika kwenye Neno lililoandikwa. Na utupe Roho Mtakatifu maishani mwetu, ili kwamba tuweze kuketi kwa amani na kwa utulivu na katika kumcha Mungu, na kuyachunguza maisha yetu kwa Neno Lake. Tujalie, Bwana.

12 Na katika jengo hili usiku wa leo, Bwana, kuna ndugu zangu wa hatua mbali mbali za—za kanisa. Na, Bwana, ninashukuru mno ya kwamba wamekuja hapa kufanya ushirika. Labda huenda tusikubaliane katika kanuni ndogo za mafundisho. Lakini katika kanuni hiyo moja kuu, tunasimama kama ndugu walioungana vitani kwamba, Ee Mungu, jalia hilo litie nguvu kushirikiana kwetu—kwetu mbalimbali, na ninii yetu…na vifungo vya neema ya Mungu na upendo uwe juu yetu kwa wingi. Sasa, tukitambua, Bwana, ya kwamba hii ni kazi kubwa sana kwa mwanadamu kufanya, kwa maana tunatafakari hapa, usiku wa leo, kikomo cha nafsi ambazo zinaelekea katika Umilele. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu ataingia moja kwa moja kwenye Neno, na ataliweka wazi na kulieleza katika njia Yake Mwenyewe, kwetu sisi, mambo ambayo angetutaka tuyajue. Tujalie, Bwana. Na wakati hizi tatu…nyakati za ibada zimekwisha, jalia tuondoke kama kanisa lililotiwa nguvu, tumeungana pamoja, kuweka mioyo yetu na malengo yetu vyote pamoja, pamoja na wenyeji wenzetu wa Ufalme wa Mungu, na tusonge mbele kuliko isivyowahi kuwa kamwe hapo awali.

13 Ninataka kukushukuru, Bwana, hapa Mbele ya kanisa na—na watu walio hapa, ya kwamba ulinipa mimi sasa majuma kadha ya kupumzika. Ninajisikia vizuri sana usiku wa leo kwa sababu ya Uwepo Wako na baraka Yako. Na, Ee Mungu, tunamwombea ndugu huyu hapa, ndugu yetu anayeenda ng'ambo, mbali huko chini kabisa katika nchi hizo zenye giza, chafu, ambako maisha yake yenyewe yamo hatarini. Na, Ee Bwana, mbariki Ndugu yetu Jeffreys anapoondoka, na mwanawe, na mkewe, na umpe ongezeko kubwa sana. Jalia atoboe mashimo katika giza mpaka Nuru ya Injili itang'aa kila mahali. Tusikie, Baba, kwa maana tunaomba ombi hili katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao. Amina.

14 Sasa, usiku wa leo, ninasoma kwenye Biblia yangu ndogo ya Scofield. Tayari nimepitisha miaka ishirini na mitano, hivi majuzi. Nami ningali ninaweza kuisoma, lakini inafifia sana, kwa hiyo nilijinunulia miwani ya kusoma ninaposoma. Nami nitaona jinsi inavyofanya kazi usiku wa leo, kwa mara yangu

ya kwanza. Sasa mimi nina masomo kama haya, kwamba, *Je! Kanisa*. . . Loo, mambo mengi, kama tunaweza kuyafikia. Moja la hayo, *Kwa nini tunaitwa Kanisa? Kwa nini sisi si Madhehebu? Kwa nini—kwa nini tunaamini katika usalama wa Milele wa nafsi ya mwamini? Kwa nini tunawakataa wahubiri wanawake? Kwa nini tunabatiza kwa maji mengi? Na je! Kanisa litapitia katika ile Dhiki*? Na mengi ya masomo hayo hapa, nafikiri nina kama kumi na tano ama kumi na nane ya hayo, kwa ajili ya siku chache zijazo usiku.

15 Kwa hiyo ninawazia usiku wa leo, kwanza, kuanzia na, inaonekana kwamba Bwana ameweka ndani ya moyo wangu kwa somo hili, ninii. . . *Kwa Nini Sisi Si Madhehebu*? Sababu ambayo. . . Sasa, hatuna neno dhidi ya watu wengine ambao ni madhehebu. Hatuna neno dhidi yao, lakini ninataka kueleza ni kwa nini sisi hatukuungana na madhehebu yo yote. Niliwekwa wakfu katika kanisa dogo la Kibatisti, kama mjuavyo. Na Batisti si madhehebu, halikuwa hivyo mpaka hivi karibuni, na sasa linakuwa madhehebu tu kama mengine yao. Lakini, sababu ya sisi kamwe kutofanyika madhehebu.

16 Sasa, sisi ni shirika. Sisi ni shirika, lililosajiliwa hapa kwenye—kwenye mahakama kama shirika, kundi la watu walioungana pamoja kumwabudu Kristo, lakini sisi si madhehebu. Hakuna mtu atakayetutawala, mnaona, Si madhehebu. Ni—ni shirika tu la ushirika miongoni mwa waamini Wakristo. Watu huja mahali hapa kanisani, na hili linakuwa kanisa lao la nyumbani, kama wanataka kuja maishani mwao mwote.

17 Nao wanaweza kuja hapa na kupinga kila kitu tunachohubiri. Hilo ni sawa kabisa. Ungali, mradi tu wewe ni Mkristo, una ushirika na uhusiano mzuri kama wengine wao. Unaona? Kama nilisema ninaamini katika kubatiza kwa kuzamisha katika maji, nawe unaamini katika kunyunyizia, na kudumu kwa huo, tungali tutakuwa jinsi tungalikuwa kama sote tungalikubaliana. Huenda tusingekubaliana, lakini mradi tu wewe ni ndugu Mkristo ama dada, unakaribishwa vizuri sana, unaona, kila mmoja.

18 Kwa hiyo sisi si wa madhehebu yo yote, kwa sababu ninafikiri ya kwamba madhehebu hutenganisha undugu. Baadhi yao, husema, "Vema, sisi hatuna uhusiano wo wote na ufufuo huo, huo ni ufufuo wa Kimethodisti. Vema, huo ni wa Kibatisti, hatuna. . . Sisi ni Wamethodisti, hatuna uhusiano wo wote na huo." Ndugu, kama Kristo yuko ndani yake, tuna—sote tunahusika nao. Hatuna budi kuweka ninii yetu. . . Ni—ni mwili wa Kristo unao—unaoteseka. Nami ninaona jambo hilo sana nchini leo, jinsi ambavyo tumeninii. . . Sasa, Kristo kamwe hakuninii, wakati wo wote, hajapata kuunda madhehebu yo yote ya kanisa. Sasa, hebu hilo lihakikishwe vizuri.

19 Basi, sasa, nitawaulizeni kesho usiku, kama lo lote la mambo haya mnayotaka kujua, kama vile historia fulani ninayonukuu, ama jambo lingine. Sina tu wakati wa kumalizia jambo hilo, sitaingilia somo lingine, maana ungeweza kutumia majuma kadha kwenye somo lilo hilo. Lakini kama ukitaka kujua mahali, jambo lo lote, niulize tu na uliweke hapa kwenye—kwenye dawati, nami nitalipata, nitakujibu.

20 Sasa, madhehebu ya zamani sana, na madhehebu ya kwanza ya kanisa tuliyopata kuwa nayo, ni kanisa Katoliki. Nalo lilifanywa madhehebu miaka mia tatu na kitu baada ya kifo cha mtume wa mwisho. Hiyo ni kweli. Unapata jambo hilo katika wale Makasisi wa Nikea wa mwanzoni, na unalipata kwenye maandishi haya ya Josephus, na, loo, wengi wa wale—wale wanahistoria mashuhuri. Unaona? Na kadiri ya—ya . . . wakati wo wote wa kanisa, kote kote mpaka kifo cha mtume wa mwisho, na miaka mia tatu upande mwingine wa mitume, hakukuwako na makanisa ya kimadhehebu. Na Katoliki lilikuwa ndilo madhehebu ya kwanza ya kanisa.

21 Na kanisa la Kiprotestanti ndio madhehebu ambayo yametoka kwenye madhehebu. Matengenezo ya kwanza yaliyokuja, yalikuwa Luther; baada ya Luther akaja Zwingli, baada ya Zwingli akaja Calvin, na kuendelea tu baadaye namna hiyo. Na hata kufikia ule Ufufuo wa Wesley, na hata kufikia Alexander Campbell, John Smith, na kadhalika, unaona, kote. Na ufufuo wa mwisho tulio nao, uliopo sasa, ni vipindi mbalimbali vya wakati wa Kipentekoste.

22 Nami ninaamini ya kwamba Mungu ameshughulika katika kila wakati. Lakini ulipata kuona ya kwamba kila wakati kanisa linapowahi kushindwa, na mara wanapounda madhehebu wao wanaanza kuanguka papo hapo basi? Na kila wanaposhindwa, Mungu kamwe haliinui kanisa hilo tena. Linakufa papo hapo. Sasa wewe ninii tu . . . Iwapo unataka kujua historia ya jambo hilo, tu—tunaweza kuitoa, ya kwamba—ya kwamba hakuna kanisa, hata katika historia ya makanisa, ambapo madhehebu yo yote yamepata kuanguka kisha yakainuka tena. Batisti, Methodisti, Presbiteri, Luther, na yo yote yale, wakati yalipoanguka, yamekwisha. Sasa, hiyo ni kweli. Sasa, hili, ni—niliwaambia sasa, vaeni makoti yenu, maana tutashindilia jambo Hili. Mnaona? Hapajapata kuwepo, wakati wo wote, ambapo mtu mmoja alitoka kama mtu binafsi na kuunda madhehebu ya kanisa, likaanza.

23 Mungu hushughulika na watu binafsi, si na madhehebu. Hakuna wakati wo wote ambapo Mungu aliwahi kuyashughulikia madhehebu. Daima Yeye anashughulika na mtu binafsi. Katika Agano la Kale, Yeye alimshughulikia mtu binafsi. Katika Agano Jipya, Yeye alishughulika na mtu binafsi. Katika wakati wo wote, Yeye daima alishughulika na watu binafsi, wala si na madhehebu. Kwa hiyo, basi, kama Mungu

hayuko katika madhehebu, kuna faida gani ya mimi kuwa na uhusiano wo wote nayo kama madhehebu? Sasa, sizungumzii juu ya watu katika madhehebu hayo, ninazungumza juu ya madhehebu hayo yenyewe, maana watu wa Mungu wako kwenye madhehebu hayo yote..

24 Sasa, Mungu kamwe haachilii jambo lo lote litukie pasipo Yeye kutoa onyo. Siamini kuna jambo lo lote ambalo . . .

25 Sasa, kama vile tulivyo na hoja zinazotoka makanisani, kama ile tuliyokuwa nayo hivi majuzi kuhusu damu na mafuta, na kadhalika, nanyi mnajua ile barua ya "Mpendwa Ndugu Branham," na kadhalika. Lakini sababu ya mimi kupinga jambo hilo, ni kwa sababu haliko kwenye Neno. Na hiyo ndiyo sababu mimi ninapinga madhehebu, kwa sababu hayako kwenye Neno. Na hapana budi kuwepo na kitu fulani ambapo tutawekea msingi imani yetu. Na iwapo hatuwezi kuiwekea msingi juu ya madhehebu fulani, hatuna budi kuiwekea msingi juu ya Neno la Mungu. Kwa kuwa, huo ndio msingi wa pekee, ni, Neno la Mungu.

26 Na halafu kama Neno la Mungu halizungumzii juu ya madhehebu, lakini linapinga madhehebu, basi hatuna budi kunena pamoja na Neno. Haidhuru askofu, lo lote mtu ye yote analosema, lo lote mtu ye yote analowazia, lo lote mtu fulani mzuri analosema, lo lote cho chote kisemalo, kama si kulingana na Neno la Mungu, basi ni makosa. Unaona, halina budi kuwa, Neno halina budi kuwa ndilo jambo la mwisho. Neno la Mungu halina budi kuwa ndilo Amina ya mwisho.

27 Sasa kumbukeni, mimi simwondolei mtu Ukristo (mnafahamu jambo hilo) katika madhehebu. Kuna makumi elfu ya watu wa thamani katika madhehebu hayo yote, ambao ni watoto wa Mungu. Lakini kuwatenganisha na kuwabagua, mimi ninapinga jambo hilo. Na Neno la Mungu linapinga hilo.

28 Nami ninaamini ya kwamba hakuna itikadi iliyo nchini leo, hakuna itikadi iliyopata kuwa nchini, ila ile iliyotabiriwa kwamba itakuja, na Neno la Mungu. Ninaamini ya kwamba Neno la Mungu hutupa kila kitu tunachohitaji, mumu humu katika Neno. Tangu . . . mwanzo wetu hata mwisho, unapatikana katika Neno la Mungu. Halafu basi ni—ninaamini ya kwamba kama limo katika Neno la Mungu, basi hatuna budi . . . Linatabiri. Na Neno la Mungu ni onyo.

29 Sasa, husomi Neno la Mungu kama tu vile unavyosoma gazeti. Unasoma Neno la Mungu kwa Roho Mtakatifu, unaona, kwa sababu Roho Mtakatifu Mwenyewe hunena kwa kwa njia ya Kristo. Kristo akimshukuru Mungu ya kwamba alikuwa ameyaficha mambo haya kwa wenye hekima na akili, na angewafunulia watoto wadogo wanaoweza kujifunza. Kwa hiyo, unaona, hakuna njia yo yote ya kupata kuelemishwa kamwe, hakuna njia yo yote ya kuunda madhehebu. Kuna njia moja tu

ya kuwa sahihi, hiyo ni, kuongozwa na Roho wa Mungu, na ujuzi huo uliokuwa nao hauna budi kulingana na Neno hili. Unaona, ndipo umelipata. Unaona?

30 Kama vile wakati tutakapofikia hapa chini katika dakika chache sasa, tunashughulika na watu ambao ni—ni . . . baadhi yao ni Wakalvini wenye msimamo mkali, wengine wao ni Waarmenia wenye msimamo mkali, na—na njia mbalimbali. Sasa, daima kuna ninii, haidhuru utalipunguza namna gani katika visehemu vyembamba namna gani, lazima liwe na sehemu mbili. Hiyo ni kweli kabisa. Zote mbili zina mambo muhimu ya kubishania. Lakini, jambo lenyewe ni kwamba, Ukweli wake upo wapi? Hapo ndipo tunapokaribia, mahali ambapo tunafikiri, kwa neema ya Mungu, tunaweza kuwaonyesha Kweli yake. Sasa hebu na tuchukue tu . . . na hapa ndipo nilipoandika tu baadhi ya Mafundisho haya ya kanisa.

31 Hebu tufungue Biblia zenu kwa dakika chache tu, ninyi nyote sasa, na hebu tufungue Ufunuo, mlango wa 1, ama Ufunuo, mlango wa 17, kwanza. Na hebu tuanze tu kusoma na tuone sasa mahali ambapo makanisa haya yalipoanzia, na ni—ni kitu gani kilichoyaanzisha. Sasa, Biblia hutangulia kuonya kila jambo. Inatangulia kuonya siku tu—tunazoishi. Na sasa, Ufunuo, mlango wa 17, kama mkifungua. Nilisema wa 13, sikumaanisha huo, huo uko kwenye . . . Tutachukua huo baada ya kitambo kidogo, pia, huo uko katika unabii wa Marekani. Lakini sikilizeni kwa makini sana sasa.

> *Akaja kwangu mmoja wa wale malaika saba, wenye vile vitasa saba, akanena nami, akisema, Njoo huku, nami nitakuonyesha hukumu ya yule kahaba mkuu aketiye juu ya maji mengi*;

32 Sasa kumbukeni, hili linasikika la kisiri. Sasa mwanamke huyu mwenye sifa mbaya, sasa, kama tutafundisha jambo hili, huna budi kuchunguza kwanza maana ya mifano hii. Sasa, *mwanamke,* katika Biblia, anawakilisha "kanisa." Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Sisi ni Bibi-arusi, Kanisa ni Bibi-arusi.

33 "Njoo huku nami nitakuonyesha hukumu." Sasa, kuna hukumu kubwa itatolewa juu ya yule kahaba mkuu, yule mwanamke mchafu anayeketi juu ya maji mengi. Sasa, *mwanamke* ni mfano wa "kanisa," na *maji* ni mfano wa "watu." Sasa, kama mkiangalia hilo, pia, angalieni kwenye aya ya 15 wakati mkiwa hapo, aya ya 15, mlango ule ule.

> *Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa na makutano . . . mataifa na lugha.* Unaona?

34 Sasa, kanisa hili kuu, mwanamke huyu mkuu, sasa kumbukeni yeye ana sifa mbaya. Na iwapo mwanamke anawakilisha kanisa, (na Kanisa la Kristo ni Bibi-arusi, Bibi-arusi mtakatifu), basi hapa yupo mwanamke mchafu. Huyo

hana budi kuwa ni mchafu, anyejifanya kwamba ni bibi-arusi. Unaona? Sasa, yeye anafanya nini? "Anaketi juu ya," ama, "kuwa juu ya" maana yake ni "kuwa na mamlaka juu ya maji mengi." Kwa maneno mengine, yeye ana mamlaka juu ya mataifa yote na lugha na watu. Yeye ni mtu mkuu, mwanamke huyu ni mkuu.

Sasa, *ambaye wafalme wa nchi wamezini naye*, . . .

35 "Kwa kuwa wafalme wa nchi wamezini naye," matajiri, watu wakuu wamezini naye. Ungewezaje kufanya ninii, mfalme angewezaje kuzini na kanisa? Ni Uzinzi wa kiroho, kiroho! Uzinzi ni kitu gani? Ni, vema, ni kama mwanamke anayeishi bila uaminifu kwa mumewe, anaishi na mwanamume mwingine wakati yeye ana mume. Na kanisa hili, basi, li—linajifanya kuwa ni Bibi-arusi wa Kristo, huku likifanya uzinzi na wafalme wa nchi, kwa maisha yake machafu, kazi yake chafu. Loo, lina kilindi na linakolea, mimi ninalipenda tu Neno! Sasa angalia.

> . . .*ambaye wafalme wa nchi wamezini naye, nao wakaao katika nchi wamelevywa kwa mvinyo ya uasherati wake* . . .

36 "Mvinyo" wake ni kile alichokuwa anatoa, changamko lake, "Sisi ndio kanisa lenyewe! Sisi ndio tulio na kitu chenyewe." Mnaona? Sasa, ingiza tu hilo moyoni mwako sasa. Vema. Kwa hiyo akanichukua . . .

37 Kama vile malaika alivyomwambia Yohana, "Nitakuonyesha hii hukumu inayokuja juu ya kanisa hili kuu." Sasa angalia.

> *Akanichukua katika Roho hata jangwani, nikaona mwanamke, ameketi juu ya mnyama mwekundu sana*, . . .

38 Rangi *nyekundu sana*, katika Biblia, inawakilisha "kitu cha kifalme." Ile rangi *nyekundu sana* inamaanisha "nyekundu." Na *mnyama* anawakilisha "nguvu." Je! uliona ya kwamba mnyama huyo alitokea baharini, huyo aliyekuwa katika Ufunuo, mlango wa 13. Na wakati unapomwona mnyama akitoka baharini, inamaanisha ya kwamba mamlaka hii ilikuwa ikitokea kati ya watu. Lakini katika Ufunuo 13, wakati mwana-kondoo huyu alipotokea, yeye alitokea ardhini, pasipo watu, Marekani. Lakini basi baada ya yeye kuwa na pembe mbili ndogo, nguvu za kisiasa na za kanisa, kisha akapokea mamlaka na kunena kama lile joka lililomtangulia. Kwa hiyo huna budi tu kuliandika, tunaelekea kwenye mateso ya dini na mambo yale yale waliyofanya katika Rumi ya kipagani miaka mingi iliyopita, kwa kuwa, ni BWANA ASEMA HIVI! Sasa jambo ni kwamba, "ameketi juu ya mnyama, mamlaka fulani."

39 Uliona Rebeka wakati Elieza alipokutana naye, ilikuwa ni wakati wa jioni, naye akampa ngamia maji. Maana, Elieza alisema, "Kama msichana anayekuja atamnywesha ngamia huyu, basi huyo atakuwa ndiye . . . na kunipa maji ninywe,

huyo ndiye ambaye umemchagua, Bwana, kuwa bibi-arusi wa mtumishi Wako, Isaka." Na hapo alipokuwa katika maombi, Rebeka akaja na kuchota maji kisha akampa maji anywe, halafu akamnywesha maji ngamia. Angalia, ngamia alikuwa ni mnyama. Na mnyama yuyo huyo aliyekuwa akimnywesha maji, ndiye aliyempeleka kwa bibi-arusi wake, Isaka.

40 Na siku hizi, nguvu za Roho Mtakatifu, ambazo kanisa linazitilia maji na kuabudu, ndicho kitu kitakacholiondoa humu duniani, kumlaki Bibi-Arusi. Hakika, Isaka alikuwa huko nje kondeni jioni. Hatumlaki Bwana huko juu Utukufuni. Waefeso, sura ya 5, ilisema ya kwamba "tutamlaki Yeye hewani." Loo, hilo linawafanya Wamethodisti wawe tayari kupiga makelele. Wazia jambo hilo! Unaona? Bwana. . . Isaka alikuwa ametoka katika nyumba ya baba yake, na alikuwa huko kondeni hapo alipomwona Rebeka akija juu ya ngamia, naye akampenda alipomwona mara ya kwanza, ndipo akashuka kutoka kwenye ngamia akakimbia kumlaki. Hiyo ni kweli. Huko ndiko tunakokutana na Bwana. Na ngamia yule yule aliyempa maji, alimbeba akampeleka kwa mumewe. Na nguvu zile zile ambazo kanisa linaabudu, ambazo ulimwengu unaita ushupavu wa dini, ambazo kanisa linaabudu, ndizo nguvu zile zile zitakazolinyakua kanisa hewani, kumlaki Bwana hewani. Roho Mtakatifu, unaona. Hapo lina. . . Pia, angalia, Rebeka alikuwa bikira.

41 Na mwanamke huyu ni kahaba, tunayenena habari zake hapa. Sasa, mmeelewa hizo nguvu ni nini sasa? Ngu—nguvu, ninii. . . inamaanisha ya kwamba yule mnyama, alikuwa juu ya yule mwekundu sana. Sasa, ingekuwa ni mnyama wa namna gani? *Mwekundu sana*, hiyo ingekuwa ni "mamlaka tajiri." Ni kanisa la namna gani hili atakalokuwa sasa? Ni kanisa tajiri, na ni kanisa kuu, na ni kanisa lenye nguvu, na yeye. . . ushawishi wake unaenea katika makutano ya watu na katika watu. Na wafalme wa nchi wamefanya uzinzi wa kiroho naye, hiyo ni kusema, watu mashuhuri wa duniani. Sasa tutaona kwamba yeye ni nani hivi punde, pia tuone kuhusu madhehebu haya.

> *Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau* (kifalme), *amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na vito vya thamani,. . . lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake.*

42 Angekuwa na nini mkononi mwake? Mafundisho yake, yale aliyokuwa akiwaonyesha watu, "Sisi ndio kanisa! Sisi tuko *hivi!*" Naye amewalevya wafalme wa nchi na nafsi yake namna hiyo. "Sisi tuko *hivi*! Sisi ndio mamlaka kuu! Tumeenea katika kila taifa! Sisi ndio kanisa lililo kuu sana lililopo. Njoni, mnywe ninii yetu. . . Hapa, mimina kidogo mvinyo, inywe, kunywa."

En-he, unaona, "naye alikuwa na kikombe mkononi mwake." Angalieni.

> *Na mwanamke yule alikuwa amevikwa nguo ya rangi ya zambarau, na rangi nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na vito vya thamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na* chukizo*, na machafu ya uasherati wake.*

43 Sasa enyi marafiki, hatusomi gazeti la kila siku, tunasoma Neno la Mungu la Milele na lililobarikiwa. Mbingu zote na nchi zitapita, lakini Neno hilo litasimama! Hiyo ni kweli.

> *Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina* lililoandikwa, *alikuwa na jina limeandikwa,* hasa, *LA SIRI, BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA, MACHUKIZO YA NCHI.*

44 Sasa, hapa wakati fulani uliopita, sidhani ni katika kanisa hapa, lakini nilihubiri juu ya somo, *Yale Maandiko ya Mkono Ukutani*, na kutoa habari za historia ya Babeli. Sasa, kila itikadi iliyopata kutokea, kila dini na kila itikadi iliyopo duniani leo, ilianzia kule Mwanzo. Sasa, kama utachukua kitabu kiitwacho *Two Babylons* kilichoandikwa na Hislop, kama unataka kulifuatilia katika historia, ama katika baadhi ya hivyo vitabu vizuri, hata unaweza kupata kila itikadi unayotaka kupata. Nitawapeleka kule nyuma kwa dakika chache juu ya wahubiri wanawake, mnaona, na kuwaonyesha ni mahali gani hasa lilipoanzia, unaona, kule nyuma katika Mwanzo. Na juu ya mambo haya mbalimbali, jinsi tu yalivyotokea katika mwanzo. *Mwanzo* maana yake ni "chanzo." Ni wangapi wanaojua ya kwamba jambo hilo ni kweli? Mwanzo ni chanzo. Kwa hiyo, kila kitu kilichoko, kilipaswa kuwa na mwanzo.

45 Ninapouangalia mti. Nimekuwa mwituni kama miezi miwili, mitatu, kama miezi miwili. Ninaona mti, jinsi ulivyo mzuri. Ninauona, unaharibika; mwingine unakuja kuchukua mahali pake, maisha yanayoendelea daima. Nami ninawazia juu ya jambo hilo. Lakini mahali fulani huo mti ulikuwa na mwanzo. Ilibidi uwe na mwanzo. Na njia pekee ambapo ungaliweza kuwa ni mti, ama kuwa ni mninga, ama mpingo, ama namna ya mti msanduku, ama mtende, ama cho chote kile, ilibidi kuwepo na Akili Kuu nyuma yake. Ama kama kuna mmoja tu, kulikuwa na mninga moja, kila kitu ulimwenguni kingalikuwa ni mninga tu. Lakini Kitu fulani kikuu, Akili Kuu, ilipaswa kuiweka katika utaratibu. Jina Lake takatifu libarikiwe! Yeye Ndiye anayeweka mwezi na nyota katika mfumo wa jua. Yeye aliweka kila kitu katika utaratibu wake. Naye ataliweka kanisa Lake katika utaratibu, litazunguka tu kama vile Yeye anavyolitaka lizunguke, mashariki, magharibi, kaskazini, ama kusini, ama cho chote kile, wakati tunapoweza kutoa mawazo haya ya kimadhehebu kutoka niani mwetu na kujitupa wenyewe kabisa

huko Kalvari. Yeye ataliweka katika utaratibu kama tutajitolea tu kama hiyo miti na viumbe vingine Vyake. Huoni mwezi ukisema, “Mimi sitatoa mwanga usiku wa leo, baadhi yenu ninyi nyota angazeni mahali pangu.” Lakini, sisi, la, ni tofauti, unaona.

46 Sasa, Babeli, angalia jinsi Babeli ilivyopatikana. Inatokea mwanzoni mwa Biblia. Inatokea katikati ya Biblia. Na inatokea katika mwisho wa Biblia. Sasa, kuna jambo fulani. Sasa, inaanzia na Nimrodi. Nimrodi alianzisha Babeli katika Bonde la Shinari, karibu sana kati ya Mto Tigrisi na Frati, na Frati ulipitia ndani yake. Na—na jinsi ambavyo kila barabara kote nchini ilivyoelekea Babeli! Na kila mmoja wa malango hayo ulikuwa na upana wa kama futi mia mbili, malango hayo yaliyotengenezwa kwa shaba. Na wakati ulipoingia ndani ya mji wa Babeli, kila barabara ya mji ilinyosha moja kwa moja kuelekea kwenye kiti cha enzi.

47 Sasa, unaweza kwenda huko Rumi leo, na kila barabara itakuelekeza Rumi. Na kuna maskini bikira Maria ameketi kwenye kila kona, mahali barabara inapopiga kona, na mtoto Kristo mikononi mwake, akielekeza Rumi. Unaona? Inatokea katika mwanzo wa Biblia, inatokea katikati ya Biblia, na hii hapa katika mwisho wa Biblia. Sasa ninataka kuendelea kusoma tu kwa dakika chache tu, ili kwamba mpate msingi wa jambo hili, unaona. Vema.

> *Nikamwona yule mwanamke*. . .(sasa angalia kanisa, wakati unapoona *mwanamke* wazia tu juu ya “kanisa,” unaona). . . *nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu*,. . .

48 Sasa, neno *mtakatifu* linatoka wapi? Neno *mtakatifu* linatokana na “mwenye kutakaswa” ama “aliyetakaswa.” Mwenye kutakaswa! Vema.

> . . .Nikamwona amelewa *kwa damu ya watakatifu*,. . .

49 Sasa, kama mwanamke huyu ni kanisa, yeye anawatesa watakatifu. Naye ndiye kanisa lililo kuu sana, nalo lina mamlaka juu ya dunia yote. Yeye yuko juu ya maji mengi, naye. . . wafalme wa nchi wanafanya uzinzi naye. Vema, yeye ni nani? Kwa namna fulani ni siri. Sasa Roho ataninii. . .Mwajua, kunapaswa kuwe na karama tisa za kiroho katika kanisa, kwa hekima, na nyingine kwa ufahamu, na moja ya kuponya na moja kwa *kadhalika*.

> . . .*na kwa damu ya mashahidi wa Yesu*. . .

50 Ilionekana kana kwamba wao hawakujali sana aliyosema Yesu, ilikuwa ni yale liliyosema kanisa. Hiyo ni kweli. Na hiyo ni sahihi pia.

> . . .*Nami nilipomwona nikastaajabu ajabu kuu.*

51 "Nilishangaa ajabu kuu. Mimi...Ilikuwa ni—ni mshangao mkuu juu yake, jinsi nilivyoshangaa jinsi ambavyo yeye..." Sasa hebu mimi nipachukue mahali pa Yohana na kujaribu kufungua jambo hilo kidogo, unaona. Yohana alisema, "Huyo hapo ameketi. Anajifanya kwamba ni kanisa la Kikristo. Yeye ndiye aliye na fedha zote za ulimwengu. Amewaweka wafalme wote wa nchi chini ya miguu yake. Ana mali nyingi na ni mrembo, na anawezaje kulewa kwa mashahidi wa Yesu? Anawezaje kuwatesa watakatifu? Anawezaje kuwaua mashahidi wa Kristo, na hata hivyo anadai yeye mwenyewe kuwa ni Mkristo, kanisa la Kikristo?" Sasa angalia.

> *Na yule malaika akaniambia, Kwani kustaajabu? Nitakuambia siri ya mwanamke huyu, na ya mnyama huyu amchukuaye, mwenye vile vichwa saba na zile pembe kumi.*

52 Sasa, huku ni kusoma kwa kawaida hapa sasa. Shika hili, hili litakuwa rahisi sana.

> *Yule mnyama* ambaye *umemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari* kushuka—*kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha Uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu wamwo—wamwonapo yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako.*

53 Sasa, sasa hili halina budi kufinya, kwa hiyo hili hapa. Kasema, sasa angalia, ya kwamba wakati wote, si wachache tu, lakini wote wakaao juu ya nchi watastaajabu, wote watastaajabu. Ulimwengu mzima utastaajabu juu ya mwanamke huyu. Kuna kundi moja tu ambalo halitakuwa linastaajabishwa na jambo hilo, na hilo ni hao walioandikwa majina yao katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

54 Sasa, afadhali tu nisukumize jambo hili papa hapa, maana tutaliingilia katika dakika chache. Mnaona? Majina yao yaliandikwa lini katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo? Tangu lini? Ule ufufuo wa mwisho waliohudhuria? Ule usiku walipokwenda madhabahuni? Ule usiku walipojiunga na kanisa? Silengi kuwaudhi, lakini, ninawaambia, Biblia ilisema majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo "tangu kuwekwa misingi ya ulimengu." Kweli kabisa! Wakati Mungu, hapo mwanzo, alipoona ya kwamba Yeye angemtuma Mwanawe, Naye angepachukua mahali pa mwenye dhambi, wakati Damu ya Mwana wa Mungu ilipomwagika, Biblia ilisema Damu Yake ilimwagika kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Biblia inasema jambo hilo, ya kwamba Damu ya Kristo ilimwangika kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu? Wakati Damu hiyo ilipomwagika, kila mshiriki wa huo Mwili,

majina yake yaliandikwa kwa Damu hiyo kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo wakati wa kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu. Unaogopa nini? Loo, ndugu! Jambo hilo linaifungua milango, sivyo?

55 Vema, sasa hebu na tusome tu hili papa hapa na tuone kama vile hilo linavyosema ni kweli, unaona. "Na yule malaika akaniambia, 'Kwani kust-. . .'" Naamini ni kifungu cha 8. "Na yule mnyama uliyemwona . . . " Vema, ndipo penyewe.

> *Yule mnyama uliyemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu* . . . (sasa, tutarudi kwenye jambo hilo, lakini ninataka kupata hili lingine, kwa maana tunalifikia) . . . *na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha Uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu,* . . .

56 "Kutakuweko na kundi fulani duniani," kwa maneno mengine, "litakalodanganywa," kwa kuwa yeye aliwadanganya. Na kulikuweko na kundi moja pekee ambalo halikudanganywa, na hilo lilikuwa ni lile ambalo majina yao yamo kwenye Kitabu cha Uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Tutaingilia jambo hilo baadaye kidogo . . .

57 Sasa angalia yule mwanamke, kanisa lile, yeye alikuwa Babeli wa Siri. Tunamwona akitokea kwa Nimrodi. Kusudi la Nimrodi lilikuwa ni nini? Nimrodi alianzisha mji fulani na kuifanya miji mingine yote kulipa ushuru kwa mji huu. Je! tungeweza kuona jambo kama hilo leo? Je! kuna mahali kama hapo siku hizi? Kuna kanisa ambalo linatawala juu ya kila taifa ulimwenguni? Bila shaka. Je! kuna mahali leo panapolifanya kila taifa kulipa ushuru kwake? Kuna mahali kama hapo? Hebu tuendelee na kusoma haya mengine, kidogo tu, ili kwamba mpate picha yake yote. Vema.

> . . . aliyemwona *yule mnyama* ambaye *alikuwako,* . . . *hayuko, naye atakuwako.*
>
> *Hapo ndipo penye akili* ambazo zina *hekima.*

58 Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba hekima ni moja ya karama za Roho? Sasa, Yeye anazungumza na kundi la namna gani, basi? Yeye hana budi anazungumza na kundi la watu walio na—na karama za Roho zikifanya kazi katika kanisa hili.

> . . . *hapa ndipo penye akili zenye hekima.*

59 Sasa, ninyi simameni, tafuteni jambo hilo katika nyakati zote hizi za kanisa hapa, zikitoka. Roho Mtakatifu akineka jinsi hizo karama zitakavyokuwa zikifanya kazi katika siku za mwisho. Sasa, tuna karama za uponyaji zinazofanya kazi. Loo, zi—zinatenda kazi vizuri. Vema, ndugu, kuna karama nyingine! Hiyo ni moja tu ya hizo. Hicho ni kitu kidogo tu. Vema, kuna karama kubwa sana kuliko hizo papa hapa. Ni ipi ingekuwa

nzuri kuliko zote, kipawa cha Roho Mtakatifu cha hekima kuliweka Neno la Mungu pamoja na kulionyesha kanisa mahali tunaposimama, kuliko tu kumfanya mtu fulani kuponywa? Sote tunataka kuwa na afya; lakini ni afadhali nafsi yangu iwe nzima, kuliko mwili wangu kuwa mzima, wakati wo wote. Loo, jamani! Msikie Roho Mtakatifu akinena kupitia kwa kinywa cha Yohana huko Patimo, kasema, "Hii hapa hekima, hebu na asikilize jambo Hili." Sasa tunachora picha hapa.

> *Hapa ndipo penye akili zenye hekima. Vile vichwa saba ni milima saba anayokalia mwanamke huyo.*

60 Kuna mji mmoja tu niujuao ulimwenguni, kuna miji miwili niijuayo, ambayo ina milima saba ama zaidi. Cincinnati ni mmoja wao, ambapo panapaswa kuwa na hadithi ya kujibunia juu ya Cincinnati, mbwa mwitu mwingine, mnajua jambo hilo, na kadhalika. Lakini kuna zaidi ya hiyo ndani yake. Lakini hakuna kanisa linalotawala Cincinnati. Kuna mahali pamoja tu katika ulimwengu mzima ambapo pana kanisa linalosimama juu ya milima saba, ambalo linautawala ulimwengu mzima. Sasa, nimetoka kule hivi majuzi tu, mambo hayo yote. Nami niliona pale mahali iliposema, "Hapa ndipo penye hekima." Ufunuo 13, "Yeye aliye na akili na aihesabu hesabu ya mnyama huyo, maana ni hesabu ya kibinadamu." Si kundi la watu, kundi la watu, lakini ni mtu "mmoja." "Na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita."

61 Mara nyingi nimesikia ya kwamba juu ya kiti cha enzi cha papa wa Rumi, imeandikwa, "Vicarivs Filii Dei." Daima nilishangaa kama jambo hilo lilikuwa ni kweli. Chora mstari, na uandike katika tarakimu katika herufi za Kirumi, uone kama ndivyo ilivyo. Ni kweli kabisa. Nilisimama karibu *hivi* na ile taji yenye sehemu tatu ya papa, ikiwa ndani ya kioo. Utawala juu ya kuzimu, mbinguni, na purgatorio, unaona. Kwa hiyo, mambo hayo, nimetoka tu kule hivi karibuni, nimetoka tu Rumi karibuni nami ninajua ni kweli. Sasa, tunajua ya kwamba imeonyeshwa wazi.

> *Navyo ni wafalme saba. Watano wamekwisha kuanguka* (ambao walikuwa tayari wameanguka wakati huo), *na mmoja yupo* (huyo ni yule ambaye amekuja sasa, ambaye alikuwa ni Kaisari), *na mwingine hajaja bado* (ambaye alikuwa ni Herode, ambaye alikuwa mwovu);. . .

62 Sasa angalia, angalia jinsi lilivyo kamilifu.

> . . .*naye atakapokuja imempasa kukaa muda mchache.*

63 Je! Kuna mtu anayejua Herode alitawala kwa muda gani? Miezi sita. Akamkokota mamaye barabarani kwa mti mmoja wa farasi. Kisha akauteketeza mji, na kuwasingizia Wakristo. Na kucheza fidla mlimani wakati wa—walipokuwa wanauteketeza

mji. Miezi si—sita. Na unaona, "Naye yule mnyama . . ." Sasa angalieni, angalieni jinsi alivyokuwa mlaghai. Mnaona? Sasa angalieni.

> *Na yule mnyama aliyekuwako naye hayuko, yeye ndiye wa nane, naye ni mmoja wa wale saba,* (tabia ya yule wa saba), *naye aenenda kwenye uharibifu.*

64 Mtu ye yote anajua *uharibifu* ni kitu gani, ni "kuzimu." Basi angalia kwamba alipanda kutoka wapi, "kuzimu." Ni kitu gani? Shimo lisilo na mwisho. Mafundisho ya Katoliki hayana msingi. Mafundisho ya Katoliki hayana Biblia. Hakuna kitu kama Biblia yo yote kwa mafundisho ya Katoliki, hakuna hata kidogo. Wao hawadai kuwa nayo. Kasisi alisema kule, maskini kasisi huyu hapa wa Kanisa la Moyo Mtakatifu alikuja kule, akasema, "Loo, yeye . . . " Nilikuwa nikimwambia juu ya kumbatiza Mary Elizabeth Frazier. Akasema, "Loo, ulimbatiza jinsi kanisa la mwanzoni la Katoliki lilivyobatiza."

Nikasema, "Hiyo ilikuwa ni lini?"

Akasema, "Katika Biblia, Biblia yako."

65 Nikasema, "Je! kanisa Katoliki lilibatiza namna hiyo? Hilo ndilo fundisho la kanisa Katoliki?"

"Naam."

66 Nikasema, "Katika kutokosea kwa kanisa Katoliki, kwa nini limebadilika hivyo sana?" Unaona?

67 Yeye akasema, "Vema, unaona, nyote mnaamini Biblia. Sisi tunaamini kanisa." Unaona? "Hatujali Biblia inasema nini, ni vile kanisa lisemayo." Hiyo ni kweli kabisa. Kama ukijawahi kufikia kwenye uamuzi wa mwisho wa jambo hilo, ijaribu wakati mmoja, uone. Wao hawajali kile Biblia isemacho, Hiyo haihusiki kwa cho chote, wanajali yale kanisa lisemayo. Mnaona?

68 Lakini sisi hatujali yale kanisa lisemayo. Tunaamini yale asemayo Mungu. Kwa maana Biblia, imeandikwa, "Na neno la kila mtu liwe uongo, na Langu liwe Kweli." Hiyo ndiyo sababu sisi si madhehebu.

69 Sasa angalia, sikiliza jambo hili kwa muda kidogo tu. "Wafalme watano, ambao wamekwisha kuanguka, wafalme watano." Kama unataka jambo hilo kutoka kwenye historia, nitakuonyesha. "Na mmoja yupo, na mwingine atakuja." Sasa angalia, "yule mnyama." Sasa, huyo mnyama hakuwa mfalme. Alikuwa yeye aliyeko; ambaye hayupo; na hata hivyo yupo, na hayupo; hata hivyo yupo, na hayupo. Ni kitu gani? Miliki ya mapapa, mamlaka, utawala wa mnyama. Hapo ni wakati Rumi ya kipagani ilipogeuzwa ikawa Rumi ya kipapa. Rumi ya kipagani ilibadilishwa, na ndipo ikawa miliki ya papa, ambao, wao walimtawaza papa awe mfalme, na papa ni mfalme wa kiroho. Hiyo ndiyo sababu yeye ni mfalme aliyetawazwa kiroho,

anadai kuwa ndiye halifa wa Yesu Kristo. Haya oneni basi. Sasa angalia.

70 Basi tutaleta hilo fundisho la Katoliki kutoka kule na kuwaonyesha jinsi lilivyopenya moja kwa moja likaingia katika makanisa ya Kiprotestanti, unaona, jinsi ambavyo lingali limo katika kanisa la Kiprotestanti, mengi ya hayo. Yanapinga, kweli, Biblia, ni kinyume kabisa. Sasa, "mnyama aliyekuwako, ambaye hayupo." Sasa kumbuka, wote watadanganywa walio juu ya uso wa nchi, ambao majina yao hayakuandikwa tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu. Hebu tuone.

> *Naye yule mnyama aliyekuwako naye hayuko,* (kifungu cha 11) na *yeye ndiye wa nane, naye . . . mmoja wa wale saba, naye aenenda kwenye uharibifu.* Ataendelea mpaka atakapofikia mashimo yasiyo na mwisho kwenye kikomo chake.

> *Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, . . .* (Sasa angalia hapa. Kama ukitaka kuona jambo fulani muhimu sana, angalia jambo hili) . . . *ni wafalme kumi ambao hawajapokea ufalme bado, lakini wapokea mamlaka kama wafalme muda wa saa moja pamoja na yule mnyama.*

71 Wao hawatawazwi kama wafalme; wao ni madikteta. Unaona, hawakuwahi kutawazwa kama wafalme, lakini walipokea mamlaka kama wafalme, muda wa saa moja, katika utawala wa yule mnyama. Huo ni katika wakati huu mfupi wenye giza sasa hivi ambapo madikteta wanainuka, unaona, "Walipokea mamlaka kama mfalme, muda wa saa moja, pamoja na yule mnyama." Sasa, vema.

> *Hawa wana shauri moja, nao wampa yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao.*

> *Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana-Kondoo atawashinda,* (utukufu!) *kwa maana Yeye ni Bwana wa bwana, na Mfalme wa wafalme; na hao walio pamoja naye ndio walioitwa na wateule, na waaminifu.*

72 Laiti ningaliweza kuhubiri somo moja sasa hivi juu ya jambo hilo, wale "waliochaguliwa" kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na wanadumu waaminifu kwa wito wao! Haleluya! Jambo ndilo hilo. Wanaitwa "waliochaguliwa" na "waaminifu." *Na* ni kiungo, unaona, waliochaguliwa na waaminifu. Watamshinda, haidhuru wao ni wakuu namna gani.

73 Na ushawishi mkuu wa kikomunisti, ushawishi wa kikomunisti tulio nao siku hizi, msijali hilo. Huo unatenda kazi hasa katika mikono ya Mungu, ninaweza kuwathibitishia hilo kwa Biblia hii. Yeye atamwadhibu kwa kila shahidi aliyepata kumwua. Naam, bwana. Wewe waangalie wafalme hawa watatu wote wakikubaliana pamoja, nao watamchukia huyo mwanamke. Na taifa zima, ulimwengu mzima unenea

ukomunisti. Kwa nini, haina budi kuwa ni tendo la Mungu ili kumwadhibu. Unasema, "Ngoja kidogo, Ndugu Branham, ati ukomunisti ni tendo la Mungu?" Kweli kabisa, bila shaka, ni tendo la Mungu. Biblia ilisema hivyo. Lakini huo unaingia upate kutangaza hukumu juu ya watu wasiomcha Mungu na watu haramu wenye kuleta aibu. Ni nini kilichosalia katika ulimwengu huu? Tuna kitu gani? Hapa hivi majuzi . . .

74 Nitasimamisha somo langu kwa muda kidogo tu ikiwezekana. Nilikuwa nikisoma kwenye sehemu ya Maandiko ambapo kwamba mwana haramu hataingia katika kusanyiko la Bwana kwa vizazi kumi na vinne. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Hiyo ni kweli, Kumbukumbu la Torati 23, mwana haramu. Kama mwanamke akishikwa kondeni, hiyo ni kusema, nje ya ulinzi wa mwanamume, na mwanamume fulani amshinde nguvu mwanamke huyo, itambidi mwanamume huyo kumwoa. Haidhuru kama yeye alikuwa kahaba, itambidi kuishi naye mpaka atakapokufa. Na kama mwanamke huyu akiolewa naye, akisingizia ya kwamba yeye ni bikira, wala si bikira, basi anaweza kuuawa kwa ajili ya jambo hilo. Na kama mwanamume na mwanamke ambao wamefanya ndoa, nao wamzae mwana haramu, huyo, hataingia katika kusanyiko la Bwana, hata vizazi kumi na vinne; na miaka arobaini ni kizazi kimoja, itachukua miaka mia nne kabla uzao huo haujakwisha katika Israeli.

75 Mungu anachukia dhambi! Unatarajiaje kupitia kwenye ile Damu Takatifu ya Bwana Yesu, ati kwa sababu tu wewe ni mfuasi wa madhehebu fulani na kutarajia kuingia? Utakuja kwa masharti ya Mungu ama hutakuja kamwe. Kweli! Shemasi, mhubiri, hata tuwe nini, haina uhusiano wo wote na jambo hilo. Unakuja katika masharti ya Mungu.

76 Vizazi kumi na vinne. Mtu huyo yuko hapa sasa aliyekuwa anazungumza jambo hilo na mimi. Kasema, "Tunajuaje ni nani atakayeokolewa basi?"

77 Nikasema, "Hapo ndipo unapopaswa kuwa Mkalvini mzuri." Jina lako liliandikwa kwenye kile Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu anachukua huo mkondo wa damu, hiyo ni juu Yake. Unaona?

"Vema, hilo lina . . ."

78 Sikilizeni, ninyi vijana leo. Sijui kama mnahudhuria kanisa hili, ama mnakohudhuria, ninyi vijana wanaume na wanawake. Mlitambua, mambo mnayofanya, kama kuna kizazi kingine, watoto wenu watahukumiwa kwa mambo mnayofanya? Je! hamna heshima ama adabu? Ninyi wasichana mlio hapa mnaovaa hizo maskini vikaptura vifupi na vichafu na kadhalika mitaani, mnajua, jambo hilo linajionyesha katika binti yako. Je! ulijua ya kwamba nyanya yako alikuwa ka—kahaba, na mama yako malaya, na hiyo ndiyo sababu wewe unavua nguo zako hadharani leo? Kweli! Watoto wako watakuwa nini? Naam,

bwana. Mungu alisema atapatiliza uovu wa wazazi juu ya watoto wao na watoto wao, hata vizazi vitatu ama vinne.

79 Na je! unatambua, ndugu yangu, kila wakati unapofanya jambo lile lililo jema, hilo litakuja kwa watoto wako?

80 Angalia hapa, hebu tuchukue Waebrania, sura ya 7. Biblia ilisema, wakati—wakati Melkizedeki alipokutana na Ibrahimu akitoka kumpiga mfalme, na akambariki, na kusema . . . Sasa, Lawi, ananena kuhusu kutoa sehemu ya kumi. Kasema, "Lawi alikuwa na agizo kutoka kwa Bwana kutwaa sehemu ya kumi kutoka kwa ndugu yake." Na Lawi aliyetwaa sehemu ya kumi, alitoa sehemu ya kumi, kwa kuwa yeye alikuwa bado yuko katika viuno vya Ibrahimu wakati alipokutana na Melkizedeki. Naye Ibrahimu alikuwa baba wa babu yake. Ibrahimu alimzaa Isaka, Isaka akamzaa Yakobo, Yakobo akamzaa Lawi; Lawi, baba, babu, baba wa babu. Na wakati Lawi alipokuwa katika viuno vya Ibrahimu, Biblia ilisema yeye alimtolea Melkizedeki fungu la kumi. Haleluya!

81 Usiache mtu ye yote akwambie ya kwamba kila namna ya tukio ulimwenguni linaweza kuingilia kati gurudumu kuu la Mungu, linasonga mbele moja kwa moja! Lilipangwa kule nyuma hapo mwanzo. Hakuna pepo ama pepo wa kutosha wawezao kuingilia kati mpango Wake.

82 Sasa, Biblia haikusema "kwa siri" yeye alitoa, Biblia ilisema "alitoa sehemu ya kumi" wakati alipokuwa katika kiuno cha baba ya babu yake. Utukufu! Huyo ni Bwana wangu. Loo, Yeye alijua jambo hilo kabla ulimwengu haujaumbwa. Alijua kila kitu. Na katika Ibrahimu Yeye alitoa sehemu ya kumi.

83 Nawe dada, ndugu, unawezaje kuishi hapa nje, na watu wanaishi na kuzurura na wake za watu, na wake wakivunja nyumba za watu, na—na kuishi jinsi mnavyoishi, unatarajia kizazi kingine kiwe namna gani? Jambo ndilo hili hapa, imekuwa sasa si kitu ila kundi lililozaliwa kiharamu, chafu na lililooza. Na kuna jambo moja tu lililosalia kwake, na hilo ni siku ya atomiki tunayoishi. Hiyo ni kweli kabisa. Tuko katika wakati wa mwisho.

84 Akiwa ameketi asubuhi hii, huko nyuma katika milima ya Kentucky, ni maskini mvulana mdogo, karibu usingeweza kusogelea futi kumi kutoka hapo alikokuwa, akitengeneza molasi ya mtama, labda ilikuwa ni vigumu kujua ni upi ulikuwa mkono wake wa kulia ama wa kushoto, wakati aliposikia . . . Nilikuwa nimekwenda kwenye mahali pasipoamriwa. Sikujua nilikokuwa, nilikuwa tu katika moja ya zile pori. Nami nilikuwa ninakwenda tu kule kuwinda kindi. Ndipo nilipoketi chini kule, nilianza kuzungumza naye, naye mvulana huyu akasema alikuwa anaenda jeshini. Ndipo nikakuta kwamba, tukaanza kuzungumza juu ya Bwana, naye akasema, "Mhubiri, je!

huamini ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho?" Huko juu kabisa milimani!

85 Nikasema, "Hakika, tuko. Hakika, mwanangu, tuko katika wakati wa mwisho."

86 Tumewasili. Hii ndiyo saa tunayoishi, ndugu. Tumewasili. Huwezi kuona jinsi ambavyo wale mama kule nyuma, na akina baba, jinsi walivyoishi, na babu na nyanya? Huwezi kuona jinsi mama na baba walivyoishi? Si ajabu tuko katika upotovu kama huu leo. Si ajabu ungeweza kuhubiri mpaka uumwe na kichwa, wao watavaa suruali vile vile na kukutemea mate usoni mwako. Watavuta sigara na kukupulizia nayo, na kusema, "Shika lako." Kwa nini? Kwa sababu walitoka katika kabila hilo. Nitafikia jambo hilo moja kwa moja, *Uzao wa Nyoka*, tutaona mahali mwanamke anapoingilia, tuone ni kwa nini wao wanatenda namna hiyo. Wao ni watoto wa Ibilisi tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo ni kweli. Wala hakuna jambo lililosalia, ni—ni hukumu tu ndicho kitu kilichosalia. Hatuwezi kuwa na jambo lingine lo lote ila hukumu. Mungu atakiangamiza tu kitu hicho chote kabisa, na wanadamu wenyewe ndio wamefanya jambo hilo. Mungu hakutarajia jambo hilo kuwa namna hiyo, lakini alijua lingekuwa namna hiyo. Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema Yeye angewadanganya wote walioishi juu ya uso wa dunia, ila wale ambao majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

87 Hebu tuninii...tusome mbele kidogo sasa. Sasa, sasa ninaamini tuko kwenye kifungu cha 12.

> *Na zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi, ambao hawajapokea ufalme bado, lakini wapokea mamlaka kama wafalme muda wa saa moja pamoja na yule mnyama.*
>
> *Hawa wana shauri moja, nao wampa yule mnyama nguvu zao na mamlaka yao.*
>
> *Hawa watafanya vita na Mwana-Kondoo, na Mwana-Kondoo atawashinda, kwa maana Yeye ni Bwana wa* bwana, *na Mfalme wa wafalme; na hao walio pamoja naye ndio wa—walioitwa, wateule, na waaminifu.*
>
> *Kisha akaniambia, Yale maji uliyoyaona, hapo aketipo yule kahaba, ni jamaa...makutano...mataifa na lugha.*
>
> *...zile pembe kumi ulizoziona za huyo mnyama, hao watamchukia yule kahaba,...*

88 Angalia hilo sasa, hizi *pembe kumi*, hizi "falme" kumi. Unaona, hiyo ni kila kitu kikianguka, vile hawa madikteta walivyo. Angalia kule madikteta wanakoegemea. Inaegemea wapi? Ni—niambie dikteta mmoja asiyeegemea kwenye ukomunisti. Unaona? Na watafanya nini? "Watamchukia

huyo kahaba," huyo mwanamke, kanisa. Lakini nini? Angalia watakayofanya.

> . . .*hao watamchukia yule kahaba, nao watamfanya kuwa mkiwa na uchi, watamla nyama yake, watamteketeza kabisa kwa moto.*

89 Watakilipua kitu hicho wakiondoe kwenye ramani, hakika tu kama ninavyosimama hapa. Tulikuwa tu na wakati wa kuchukua somo hilo pale la kanisa hilo, na kulifuatilia katika Maandiko, mahali liliposema, lilisema, "wafalme wote wa dunia hii, na manahodha wote, na hao wote wanaomboleza, kwa kuwa Babeli mkuu amepata ukiwa wake katika sasa moja." Saa moja, wakati wake uliwadia! Na, loo, jinsi alivyosema, "Furahini, enyi watakatifu, nanyi nyote manabii watakatifu, kwa kuwa Mungu ameipatiliza damu ya watakatifu na ndugu zenu juu yake." Mnaona, hiyo ni kweli. Hakika, ukomunisti unatumika moja kwa moja katika mikono ya Mungu. Kama tu vile Mfalme Nebkadreza alivyotumika moja kwa moja katika mikono, kuja na kuwachukua hao Wayahudi wakati walipotembea zao wakiwa uchi.

90 Nayo dhambi inaweza kuendelea kuharibu, uzao wa haki unaweza kubaki ndani humo na mbegu inaweza kuendelea kuharibika, na kuharibika na kuharibika mpaka baada ya kitambo kidogo inakwisha. Inafikia mahali ambapo kwa sababu mama zao na baba zao na wengine wameishi hivyo mbele zetu, na—na huyo mwovu ninii, hakuna kilichosalia kwa ajili yetu. Na unajua vile alivyosema Yesu? Kama hangaliifupisha hiyo kazi, hata hakungekuweko na mtu ye yote atakayeokolewa.

91 Je! unaweza kuona, unaweza kuona ni kwa nini tuna mambo haya? Mimi sitoi maelezo. Ya Arthur Godfrey na kila mtu, mwajua, yakiwa ya Elvis Presley, na—na viweo chini pamoja na maovaroli, na nywele zikining'inia chini kwenye shingo zao, na namna hii yote ambavyo matineja wanafanya. Inafanya nini? Ni kitu gani? Ni kwa sababu inatokana na kundi la watu haramu, walioishi zamani. Hakuna kilichosalia! Loo, wao watasimama na kuimba "Karibu na Wewe, Mungu Wangu," kama Ernie mpenda vidonge na hao wengine wote namna hiyo, wanaimba namna fulani ya wimbo wa dini, na kadhalika namna hiyo. Ndugu, mnajua nini? Huo, huo ni unafiki kwelikweli. Ndiyo, bwana.

92 Mtu hana shughuli zo zote kwenye mimbara hii ambaye anatoka nje huko na kucheza rumba na bugi na upuzi wote wa namna hiyo. Yeye hana hata chembe moja ya shughuli hapa nyuma. Hii ni kwa ajili ya ukuhani, walioitwa na Mungu. Hapa ni mahali pa wahudumu walioitwa na Mungu. Na si pa huko nyuma kwa watu kama hao. Hiyo ndiyo shida yake leo, wamelifanya kanisa si zaidi ya loji fulani. Loji ni sawa, ukitaka kufanya hivyo, hiyo ni juu yako. Lakini hebu nikwambie, kuna

tofauti kubwa sana kwa kujaribu. . .kati ya loji na kanisa. Naam, bwana. Ukitaka kufanya mambo hayo yote kwenye loji, na kufanya karamu hizo zote za namna hiyo na kadhalika, hiyo ni juu yako. Lakini, ndugu, kanisa linapaswa kusafishwa tangu mimbarani kote kote mpaka kwenye orofa ya chini. Hiyo ni kweli. Simaanishi kufagiliwa na madirisha mapya na kadhalika. Ninamaanisha kwa ufufuo wa mtindo wa kale, uliotumwa na Mungu, ambao utatawanya kitu hicho kutoka upande mmoja hadi mwingine. Ndiyo, Bwana. Ni kama kuwasha taa, kuwasha taa ya umeme kwenye kundi la mende kwenye ganda la tofaa. Ndiyo, bwana, watatawanyika wakati taa inapowashwa.

93 Sasa angalia, "Hawa wana shauri moja, humpa nguvu zao." Niko chini ya hilo sasa. "Zile pembe kumi." Ndiyo, sasa.

> *Maana Mungu ametia mioyoni mwao kufanya shauri lake*, (haya basi), *na kufanya shauri moja, na kumpa yule mnyama falme zao hata maneno ya Mungu yatimizwe.*
>
> Sasa, *na yule mwanamke uliyemwona, ni mji ule mkuu, wenye ufalme juu ya wafalme wote wa nchi.*

94 Sasa, hakuna haja ya kusukumana, tunajua huo ni serikali ya ukasisi wa Katoliki. Hakuna haja ya mtu ye yote. . .Ni— ninaamini jambo hilo kwa uthabiti tu kama ninavyoamini ya kwamba nimempokea Roho Mtakatifu. Ninaamini jambo hilo vizuri tu kama vile ninavyoamini mimi ni Mkristo anayesimama hapa leo, ya kwamba huo—huo serikali ya ukasisi wa Katoliki ni ninii—ninii. . .Mji wa Vatican ndio—ndio mji unaoketi juu ya milima saba. Serikali ya kanisa ni mnyama aliyekuwako, ambaye hayuko, naye ni Babeli. Ni kila kitu kimepigwa picha vizuri kabisa, kikamilifu kote kote katika Maandiko, ni kanisa Katoliki.

95 Sasa, basi hapa pana jambo la kukushangaza. Unasema, "Vema, hunishambulii mimi, Ndugu Branham." Lakini hebu nikuulize tu jambo fulani. Hebu na turudi nyuma moja kwa moja sasa kwenye kifungu cha 5.

> *Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, BABELI MKUU, WA SIRI, MAMA WA MACHUKIZO, MAMA WA MAKAHABA NA MACHUKIZO YA NCHI.*

96 Yeye alikuwa nani? K-a-h-a-b-a. Tena alikuwa m-a-m-a. Ati nini? M-a-m-a, alikuwa amezaa kitu fulani. Mama wa wavulana? Wa malaya! Malaya ni nini? Ni sawa na—na kahaba, mwanamke mzinifu. Ni kitu gani kilichomfanya mzinifu? Mafundisho yake. Yeye alikuwa akijifanya kuwa ni kanisa la Kikristo, lakini alikuwa akitoa mafundisho ya kujibunia. Na hapa yeye alisema ya kwamba alikuwa. . .Kama yeye alikuwa ndiye madhehebu ya kwanza, basi inaonekana kana kwamba kuna madhehebu yaliyotoka kwake. Yeye alikuwa mama wa makahaba. Hiyo ni

kweli? Mama wa makahaba. Hangeweza kuwa mama sasa wa wavulana. Hangeweza kuwa mama wa . . . Ilibidi awe ni mama wa wanawake. Na, kama walikuwa ni wanawake, walikuwa ni makanisa. Sasa hebu na tuone. Ni nini kilichotoka katika . . .

97 Madhehebu ya kwanza yalikuwa ni yapi? Kanisa katoliki. Madhehebu ya pili yalikuwa ni yapi? Luther Madhehebu ya tatu yalikuwa ni yapi? Zwingli. Yote yaliishia wapi? Kalvin. Ndipo ikaja kwenye Anglikana, na kutoka kwa Anglikana ikafikia kwa Methodisti. Methodisti, Methodisti ilizaa nini? Kutoka mle alitokea Alexander Campbell. Na kutoka kwa Alexander Campbell akaja John Smith; kutoka kwa Alexander Campbell lilitokea kanisa la Kikristo, ndipo wakawa na makanisa manne ama matano ya Kristo na itikadi hizo nyingine zote zilizotokea. Ndipo hili hapa kanisa la Kibatisti likaja, lilikuwa na vikundi vingi vilivyojitenga. Na kutoka kwa kanisa la Kimethodisti kukaja—kutoka kwenye kanisa la Kimethodisti kukaja, kukaja kwanza, Methodisti ya Wesley, kisha wakavunjika mara nne ama tano. Ndipo wakafikia kwenye namna nyingine ya Methodisti, na halafu wakatoka tena, kisha wakafikia kwenye Methodisti Huru. Na—na halafu wakatoka huko wakaja kwa la Nazarayo. Na kutoka la Nazarayo wakafikia kwa Pilgrim Holiness, na kutoka kwa Pilgrim Holiness wakaendelea moja kwa moja. Itikadi ndogo-ndogo tu zikitokea namna hiyo, zikiendelea tu hivyo, kila moja ya hivyo vitawi vi—vidogo kule nyuma vikaendelea moja kwa moja. Na kila kimoja cha hayo kilifanya jambo gani? Mwishowe waliishia kwenye Pentekoste.

98 Nao Wapentekoste walifanya nini? Jambo lile lile mama yao alilofanya, walirudi nyuma moja kwa moja na kuunda madhehebu. Nayo yakawa nini? Ma—madhehebu. Hebu ingia katika moja ya hayo; jambo la kwanza, "Fundisho lako ni nini?" Jamani, wanakuchana kwa kichanuo laini kabisa, unaona, wapate kujua wewe ni nani, unachoamini. Na kama hukubaliani moja kwa moja nao, ndugu, unatupwa nje sasa hivi. Na hiyo ni kweli.

99 Na usifikiri ati kwa sababu tu unasema wewe ni Mpentekoste ya kwamba wewe u salama. Ndugu, kutakuweko na Wapentekoste wengi sana waliopotea njia kama tu wale walio njiani, nina hakika. Unaona?

100 Sasa, madhehebu hayo yote, kama wangaliachilia tu baraka za Kipentekoste zitiririke, si kuziunda madhehebu, kuziweka tu katika undugu na kumwacha Roho Mtakatifu afanye ubaguzi. Roho Mtakatifu hubagua. Akina Anania, Safira walikuja wakati mmoja, wakasema *fulani*, naye Roho Mtakatifu akasema, "Kwa nini ulisema uongo?"

101 Lakini sisi tunasema, "Lakini, huyo ni Ndugu Jones, usiseme neno baya juu yake sasa, yeye ndiye mtoaji mzuri sana kanisani. Ninajua ana Roho Mtakatifu, nilimsikia akinena kwa lugha

na nimemwona akipaza sauti katika Roho." Hiyo haina zaidi ya kumwaga mbaazi kwenye ngozi kavu ya ng'ombe. Unaona? Haina uhusiano wo wote nayo. Mungu ndiye aliye na la kusema. Hana budi kusema kama ndivyo alivyo ama sivyo. Kabisa. "Lakini tumelipeleka jambo hilo kwenye madhebu yetu. Lakini tulimfukuza ku—kukoka Assemblies, la Umoja likamchukua." La Umoja linamchukua kitambo kidogo, kisha likamfukuza kwa sababu . . . Wanambeba kule nao wa Yesu Pekee wanamchukua. Wa Yesu pekee wanambeba kwa muda, na halafu kitu kingine kinachomwokota ni Kanisa la Mungu, likamwokota. Kanisa la Mungu la Unabii linamchukua, na la ufufuo wa Tomlinson linampata. Loo, jamani! Ndugu, kama hatukufilisika! Hayo ni mambo ya Kipentekoste, ule ufufuo wa mwisho. Na sasa wana sifa ya buluu, na wana waabudu mafuta, na—na damu usoni. Na, loo, rehema, sijui wamefikia wapi sasa. Ni jambo moja tu lililoninii . . .

Unajua ya kwamba Biblia ilisema lingeoza? 102 Jambo hilo lote limeoza. Ulijua Bi—Biblia ilisema siku hii itakuja, wakati hata meza za Bwana zitakuwa zimejaa matapiko? Na kasema, "Ni nani ninayeweza kumfundisha Habari hii? Ni nani ninayeweza kumfanya anifahamu Mimi? Kwa kuwa amri inabidi kuwa juu ya amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni." Ni nani Yeye anayeweza kumfundisha Habari hii? Ni wale walioachishwa matiti, mama. Unaona?

103 Sasa, hakuna—hakuna mwanamke, mwanamke mchafu katika mji huu ila yule ambaye angeweza kuzaa binti bikira. Anapozaliwa huwa ni bikira. Sasa, na anaweza kuishi msafi. Lakini kama huoni ya kwamba mama yake alikuwa wa tabia hiyo, msichana huyo, mara tisa kati ya kumi, atatenda kama tu anavyotenda mamaye. Sasa, mnajua hiyo ni kweli. Mwanamke mzee anayefanya ukahaba kwenye nyumba ya makahaba, angeweza kuzaa msichana mdogo, naye akiwa na umri wa miaka kumi na sita, msafi na mwadilifu tu kama ye yote aliye hai, lakini, kama akibaki namna hiyo. Lakini, jambo ni kwamba, anarudi moja kwa moja na kutenda kama mamaye.

104 Sasa, kanisa Katoliki lilikuwa ndilo kahaba wa kwanza wa zamani lililokuja na mafundisho liliyojitengenezea, ushirikina, ambao, Biblia ilisema, "Alitoka katika mashimo yasiyo na mwisho na litaenda kwenye uharibifu." Biblia ilisema jambo hilo. Sasa, wao wanafundisha ya kwamba hilo ni kosa. Ni kosa kulingana na Neno la Mungu. Halafu hili hapa kanisa la Kimethodisti laja lililozaliwa kutoka kwake, msichana mrembo, lakini lilifanya nini? Liligeuka moja kwa moja na kufanya mambo yale yale mama yake anayofanya. Linawaacha wafuasi wake wavae kaptura, linawaacha wavute sigara, linawaacha wafanye yasiyofaa na kutenda vile tu watakavyo. Hakuna jambo linalosemwa juu yake. Maskini yule mchungaji aliyeokwa

nusu kule nyuma, mimbarani kule nyuma, anaogopa atakosa mshahara siku moja, ama sufuria ya biskuti.

105 Hebu nikwambie, ndugu, afadhali nihubiri Injili, na kula mikate mikavu na kunywa maji ya matawi, na kusema Kweli ya mambo. Kama kila mmoja wa kusanyiko langu angaliamka na kutoka nje, kama ningewaambia Ukweli. Naam, kweli.

106 Kuna nini? Loo, ni kupata riziki. "Vema, mwajua, mimi ndiye mchungaji wa kanisa kubwa sana lililopo mjini." Ninyi Wabatisti na Wamethodisti, mnaomsikiliza nabii wa uongo. Sasa, hilo ni kali, lakini cho chote kinachofundisha kinyume cha Biblia hii ni nabii wa uongo. Sijali kiweze kuwa kimeng'arishwa vipi, ni unabii wa uongo. Hiyo ni kweli.

107 "Loo, kila kitu ni sawa mradi tu jina lako limo katika kitabu." Huenda ikawa jina lako limo kwenye vitabu dazani moja; kama halimo kwenye Kitabu cha Uzima, umepotea! Unaweza kuwa mzuri sana, unaweza kuwa mwaminifu tu na msafi na mwadilifu uwezavyo kuwa, hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo.

108 Esau alikuwa muungwana maradufu ya alivyokuwa Yakobo, inapofikia swala la kuwa mtumishi, akimshughulikia baba yake mzee kipofu na cho chote kile. Naye Yakobo alikuwa maskini mdanganyifu aliyening'inia kwenye aproni ya mamaye, maskini mvulana dondoadume. Lakini Mungu alisema, "Ninampenda Yakobo na kumkataa Esau," kabla ye yote wa wavulana hao kuzaliwa. Warumi 8 inasema hivyo. Hiyo ni kweli kabisa.

109 Mungu anajua yaliyo ndani ya mwanadamu. Naye anajua yaliyo ndani ya kanisa, pia. Tunaishi kwa Chakula cha Uzima, Mkate wa Chakula cha Neno la Mungu. Sasa, hiyo ndiyo sababu sisi si madhehebu.

110 Sasa ninataka kuwapa niniii nyingine ndogo. . .Ninataka kuwapa maelezo mengine mafupi niliyokuwa nimeyaandika hapa. "Ile ninii kuu. . ." Sasa katika Ufunuo, katika 19:2, nina jambo fulani lililoandikwa hapa, ninataka kuangalia nione ni kitu gani sasa.

> *Kwa kuwa hukumu zake ni za kweli na za haki; maana amemhukumu yule kahaba mkuu aliyeiharibu nchi kwa uasherati wake, na kuipatiliza damu ya watumwa wake mkononi mwake.* Huo ndio mwisho wa kanisa Katoliki.

111 Sasa, tunataka pia wewe uone, pia hapa, ya kwamba madhehebu, ya kwamba madhehebu pia yanapatikana katika Maandiko hapa, kwamba ninii. . .Na Biblia haizungumzii kamwe madhehebu. Madhehebu yanatokana na kanisa Katoliki. Yeye ndiye mama wa kwanza wa madhehebu na kila madhehebu yametokana nalo moja kwa moja. Sasa, hili kidogo litaumiza, litazidi kuwa kali kila wakati, unaona. Lakini na—nawatakeni mwone kwamba madhehebu hayakuzaliwa wala kuchaguliwa na Mungu, yalichaguliwa na Ibilisi. Kanisa la Mungu ni . . .

112 Sisi hatujagawanyika, sisi ni mwili mmoja; tumaini moja na Fundisho moja, mmoja katika upendo. Hilo ndilo Kanisa la Mungu aliye hai. Haidhuru ninii wao, mambo hayo, sisi tuko pamoja! Hiyo ni kweli. Kama ni Mmethodisti ama ni Mbatisti, ndugu, kama amezaliwa mara ya pili na kujazwa na Roho Mtakatifu, yeye ni ndugu yangu, tunatembea bega kwa bega. Kweli. Naam, bwana. Haileti tofauti yo yote.

113 Musa. Wakati mwingine unaweza kuangalia huku na huko na kusema, "Unajua, kundi hilo la Wapentekoste washupavu, Ndugu Branham, kwa nini unaambatana na kundi kama hilo?" Unajua nini? Musa aliwaangalia wana wa Israeli, aliangalia kupitia dirisha lile lile Farao aliloangalilia. Farao aliwaangalia kama kundi la wakanyaga matope, lakini Musa aliwaangalia kama wateule wa Mungu. Alijua walikuwa na ahadi. Kwa nini? Alijua jambo hilo kwa Neno. Na kwa imani. . . Wakati alipowekwa kwenye kiti cha enzi awe Farao, huku ulimwengu mzima ukiwa miguuni pake, ameketi pale na kunywa divai, na wanawake wenye sura nzuri wa kumpepea, kama mkuu wa dola, ama dikteta, ama mfalme wa ulimwengu, kijana Musa akiwa na umri wa miaka arobaini, alivyokuwa navyo mkononi mwake, alipoliangalia hilo kundi la wakanyaga matope huko nje; lakini yeye alijua kwamba alikuwa ni mmoja wao. Haleluya! Jambo ndilo hilo. Yeye alijua alikuwa ni mmoja wao. Na kwa imani, akiwa peke yake, alichagua!

114 Kila mtu hana budi kuchagua. Huna budi kujichagulia. Utachagua sasa. Utachagua asubuhi. Utachagua kesho usiku, kama ukiishi. Huna budi kuchagua wakati mmoja. Ndugu, muda mrefu uliopita nilichagua; Biblia hii ilikuwa ndiyo kamusi yangu, Biblia hii ilikuwa Kitabu changu cha Uzima, Biblia hii ilikuwa ni Neno la Mungu. Ninaishi kwa Biblia hii. Nitasimama na Biblia hii.

115 Kwa hiyo Musa aliangalia nje akawaona wana wa Israeli, wala hakusema tu, "Loo, hao ni watu wazuri sana. Sina neno dhidi yao. Loo, la, nisingesema neno moja dhidi yao." Hivyo ndivyo watu wengi sana wanavyofanya leo. "Loo, hao Wapentekoste na hao watu walio na Roho Mtakarifu, na hao watu wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu, loo, si—si—sina kitu dhidi yao." Lakini huyo hakuwa Musa. Yeye aliacha Misri akawa mmoja wao, akaondoka akaenda kati ya ndugu zake. Alikuwa ni mmoja wao.

116 Ndugu, hapo ndipo ninapochukua njia yangu. Nitachukua njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, hata wawe ni wachache sana ama wo wote wale. Wao wana ahadi, nami ninaona majina yao yameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Hao ni ndugu zangu. Hiyo ni kweli. Jichagulie na usimame pamoja nao. Wawe wamekosea ama hawajakosea, simama pale hata hivyo. Kama wamekosea,

wasaidie waingie katika kweli. Sawa. Huwasaidii hata kidogo kwa kuwapiga mateke. Unaona, jaribu kuwavuta watoke.

117 Charlie, kama walivyosema juu ya Ndugu Allen, juu ya moto walioninii . . . damu mikononi. Nilisema, “Kamwe, kamwe sikumdharau Ndugu A.A. Allen.” Nilisema, “Kama ningeweza kuhubiri kama A.A. Allen kamwe nisingekuwa hata na ibada ya uponyaji.” Sasa, inapofikia kutokukubaliana juu ya damu kwamba ni thibitisho la Roho Mtakatifu, mikononi mwako, nitapinga jambo hilo. Lakini inapofikia undugu, yeye ni ndugu yangu. Ninasimama bega kwa bega pamoja naye vitani. Hiyo ni kweli. Kama yeye amekosea, nitajaribu kumsaidia. Na iwapo yeye hakukosea, kama mimi nimekosea, nataka yeye anisaidie. Na hivyo ndivyo tutakavyolipata, tutakavyoendelea. Sasa angalia hapa.

> . . . Yeye alikuwa *BABELI WA SIRI . . . MAMA WA MAKAHABA . . .*

118 Sasa mnaona jinsi kanisa leo, enyi marafiki, mnaweza kuona jinsi makanisa haya leo yanaishi tu vyo vyote yanavyotaka kuishi? “Ni sawa kabisa, endelea moja kwa moja,” nguruwe anakula nguruwe mwenzake, hawajali. “Mbona, hakuna ubaya wo wote katika kufanya jambo hilo. Mbona, unajaribu tu kuwa wa mtindo wa kale.” Sasa, angalia fundisho lao. Sasa ninataka . . . Sasa angalia. Hiyo ndiyo tabia yao. Je! unaona ya kwamba miaka michache iliyopita ya kwamba kanisa Katoliki lilikuwa ndilo pekee lililokubaliwa kwenda kuona sinema? Kanisa la Kimethodisti halingaliwazia jambo kama hilo, na madhehebu hayo yote, “La, hizo ni kazi za Ibilisi.” Vema, sijui ni jambo gani lililotukia. Naam, bwana.

119 Nanyi mnajua, mngewachukua hao wasichana wadogo Wakatoliki, walitoka na ninii hizi zao ndogo . . . (Sasa, baadhi yenu enyi vijana wa zamani ni wa rika yangu) . . . wakatokea na kwenda kwenye kitu hiki kidogo ambako walikuwa na zile zilizofikia magotini. Jamaa huyo, nafikiri, yuko kuzimu usiku wa leo. Sijui, mimi si hakimu wake. Lakini alipouimba wimbo huo mchafu wa kipuuzi uliojipenyeza redioni, bila kukaguliwa, huo wa “Zikunjeni hizo, enyi vipusa, zikunjeni; zikunjeni na mkaonyeshe magoti yenu mazuri.” Ni wangapi wanakumbuka hilo wakati huo ulipotokea kwa mara ya kwanza miaka kadha iliyopita? Huko kulikuwa ndiko kupenya kwa kwanza kwa siri papo hapo. Hiyo ni kweli. Na wakati walipompata jamaa huyu kutoka Texas, na kuwachukua wanawake hao huko na kutumia nguo hizo za ndani kuwafanya waonekane kana kwamba wao ni kitu fulani cha maana ambacho hawakuwa, na mambo kama hayo, na kuwafanya wasonge mbele na jambo hilo. Na sasa wao wanafanya nini? Ilijipenyeza. Ni roho fulani.

120 Mtu fulani alikuwa akizungumza nami majuzi, akasema, “Sijui nifanye nini. Nilikuwa na mvulana mzuri mwaminifu,

na mvulana huyo amefikia ambapo yeye huchukua kile anachogusa.”

Nikasema, “Kwa nini?”

“Yeye anashirikiana na mwizi.”

121 Ukiambatana na mtu ambaye ni mwizi, utakuwa mwizi wewe mwenyewe. Mama yangu mpendwa wa Kentucky kila mara alisema, “Ukilala na mbwa aliye na viroboto, utaamka na viroboto, pia.” Ukichukua mwa—mwanamke ambaye hafai, na kumwacha msichana ananinii, na umweke pamoja na mvulana m—mzuri mwenye adabu, na muda si muda wajua yeye ni mchafu kama kitoto cha mbwa. Ligeuze vinginevyo. Unajulikana kwa kundi lako. Jitenge! “Tokeni kati yao,” ilisema Biblia, “mkatengwe nao!” Hiyo ni kweli.

122 Kama madhehebu yao yakiingia kwenye upotovu kama ule wa kuwafanya watu wao. . . Vema, hapa majuzi, kanisa kubwa na zuri la Kibatisti, iliwabidi kuwafanya watu wafumukane. Kunahubiriwa tu kwa dakika ishirini, ndizo mtu huyo angeweza, kwa sababu ilimbidi mchungaji kuvuta sigara. Kusanyiko lote lilitoka nje. Wote walisimama huko nje katika makundi ya kuvuta sigara, kisha wakarudi tena, mchungaji na hao wote. Nilienda kwenye Kanisa la Congregationist, pale aliketi mtu fulani, amevaa joho kubwa refu, amesimama pale, kasema, akainamia mimbarani namna *hii*, akizungumza juu ya namna fulani ya ua alilopata huko mlimani. Hakukuweko na jambo lingine. Ndipo akashuka akarudi, na vidole vyake vilikuwa manjano kwa moshi wa sigara. Ndiyo. Na kuzungumzia kuhusu wanawake, ya kwamba wanaume walikuwa wanaenda kucheza. . . Huu mchezo wa Kijerumani wanaocheza na ninii, zaidi sana u—unachanganya karata, wajua? Ulikuwa. . .Loo, nilifikiri ningeukumbuka. Pinochle, walikuwa wacheze mchezo wa pinochle. Nafikiri hapo—hapo ndipo unapotumia, ni karata za mchezo wa kawaida. Kucheza pinochle kwenye orofa ya chini. Jamani, jamani! Hapo ndipo msingi wake ulipo. Si ajabu! Wao wanafanyaje jambo hilo, kisha wanapigia makelele kuhusu kanisa Katoliki huku nje kwenye sehemu hizi za michezo ya bahati nasibu nao wanacheza kamari. Mbona, ninyi Waprotestanti ni wachafu tu kama walivyo wao, kwa hiyo mnaweza kusema nini juu ya jambo hilo? Nyungu haiwezi kuiita birika “chafu.” Haiwezi bila shaka. Na unafanya, na jambo hilo, wao wangesema, “Vema, Mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti.” Wewe si kitu mpaka utakapozaliwa mara ya pili. Hiyo ni kweli. Na wakati unapofanya jambo hilo, unajua kuna jambo fulani ndani yako linalokwambia mambo hayo ni mabaya, nawe utatoka humo hakika tu kama tu vile ulivyotumbukia mpaka magotini kama bata. Unajua jambo hilo ni kweli. Bila shaka. Naam, bwana. Upuuzi huo huendelea namna hiyo, kwa nini?

. . . *MAMA WA MAKAHABA* . . .

123 Moja ya siku hizi mama wa kale atasema, “Mnajua nini? Hata hivyo, kipenzi, sisi wawili tuko sawa.” Na mnajua ni jambo gani basi? Muungano wa Makanisa wataungana wote pamoja kama walivyo sasa. Na unajua ni jambo gani litakalotukia kwa kundi dogo kama hili? Mtajuta, enyi vijana. Hiyo ni kweli kabisa.

124 Lakini usijali, Mwana-Kondoo atamshinda! Kwa kuwa Yeye ni Bwana wa bwana na Mfalme wa wafalme, naye Mungu ataliongoza kanisa Lake, badala ya madhehebu. Yeye atamimina yale Mafuta ya dhahabu ya Roho Mtakatifu juu ya kanisa lile, ndugu, Moto utashuka kutoka Mbinguni, pamoja na ishara na maajabu vitafanyika jinsi ambavyo hujawahi kuona hapo awali. Naam, bwana. “Msiogope, enyi kundi dogo, ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa Ufalme.” Naam, bwana. “Yeye avumiliaye hata mwisho!” Naam basi. Shika njia, elekeza kichwa chako Kalvari. Biblia hii ni kweli. Usijali.

125 Sasa angalia, hizo hapo baadhi ya tabia walizo nazo. Baadhi ya maadili waliyo nayo. Tungeweza tu kuendelea. Muda si muda wajua, lilipenyeza kwenye makanisa ya Kiprotestanti. Ndipo wanawake wa Kikatoliki wakaanza kuninii . . . ”Mbona, haikuwa vibaya kuvaa kaptura, mradi tu ulienda kanisani na wakaweka kitambaa kidogo juu ya vichwa vyao.” Namna fulani ya mapokeo. “Msile nyama zo zote Ijumaa.” Na, loo, umeona wapi kuweka kitambaa kidogo kichwani mwako ili upate kuingia kanisani? Ninataka unionyeshe Maandiko. Ni unabii wa uongo. Ni wapi kanisani unapopaswa kuvaa kofia kichwani mwako kanisani? Unapovaa kofia kichwani mwako, unamwaibisha Kristo, hiyo ni kweli; mwanamume, ndiye ninayezungumza habari zake. Wanawake, mna kifuniko, lakini nitamsai mtu ye yote anionyeshe mahali ambapo ni kofia ama kitambaa. Ni nywele zenu! Nanyi mmezikata zote. Na jambo hilo je? Loo, eti wanasema, “Hilo ni la mtindo wa zamani.” Kama ndivyo lilivyo, ni Biblia! Neno la Mungu ni la kweli.

126 Nikizungumza hapa si muda mrefu uliopita juu ya mwanamke aliyeosha miguu ya Yesu, na kutwaa nywele zake, wajua, na—na kuipangusa kwazo. Nilisema, “Njia pekee ambayo mwanamke angetumia kufanya jambo hilo, ni kusimama kwa kichwa chake kusudi apate nywele za kutosha hapa chini kusafisha miguu Yake na kuipangusa.” Hiyo ni kweli. Loo, hilo—ni—ni fedheha kuona jinsi ninii . . . Hapa, hali ya hewa inayoganda kwa baridi, akitembea huko na huko amevaa koti fupi la mviringo namna hiyo, huku mwili wao ulio uchi ukionekana.

127 Kwa nini, useme, “Mbona unawakemea wanawake?” Mnapaswa kukemewa.

128 Nanyi wanaume mnaowaruhusu wanawake zenu kufanya jambo hilo, ndugu, si—sijui la kuwazia juu yenu. Sasa, hiyo ni kweli.

129 Nanyi wachungaji, sidhani mko hapa. Lakini kama ukiona jamaa huyo, mwambie aje aniambie, anione mimi. Unaona? Kama hana heshima yo yote kwa Kristo kuliko kuliacha kusanyiko lake liendelee na jambo hilo bila. . . Sasa yeye. . . Wanaweza kufanya jambo hilo kule nje bila yeye kujua, lakini kama yeye hawaambii jambo hilo, yeye hafai kuwa mtumishi wa Yesu Kristo. Hiyo ni kweli kabisa. Yeye hafai kuwa mtumishi wa Kristo. Mtumishi wa Krito anapaswa kuwa asiye na woga kama ni jambo linalokuja kwenye Biblia. Hakika. Lakini hao hapo, wanatoka nje na kufanya jambo hilo hata hivyo.

130 Na basi, muda si muda wajua, iliwabidi Waprotestanti kulichukua. Ninyi Wamethodisti wazuri, nanyi Wabatisti, nanyi Wapresbiteri na Wanazarayo, Wapilgrim Holiness, na ninyi nyote. Jambo lile lile, wakatoka moja kwa moja, sita ya moja, na nusu dazani ya hiyo nyingine. Haya yaoneni hayo basi, "mama wa makahaba." Madhehebu yenu, "Mradi tu yalianzia kwenye makao makuu, ilifanya tofauti gani?" Mnaona? Inaleta tofauti kubwa sana. Hayakuanzia kwenye *yale* Makao Makuu. Huenda yalianzia kwenye makao makuu yako hapa chini, lakini si yale huko Juu. Inategemea unakotoka. Hiyo ni kweli.

131 Sasa sidhani tuna muda wa kupata jambo hili lingine, labda afadhali niliache kwa ajili ya asubuhi. Vema, hebu tuchukue tu hili moja dogo fupi. Hapa tuna "ubatizo wa maji," pia tuna "kuchaguliwa tangu zamani," na, loo, mambo mengi. Kwa hiyo hebu na tuchukue tu jambo hili, hili moja dogo fupi la "wahubiri wanawake," na tulipate hili.

132 Sasa, sasa, *mhubiri mwanamke,*, sitaki kukuudhi, lakini ninataka kukwambia jambo fulani. Huna hata chembe moja ya Maandiko, huna hata moja katika Biblia. Naam, ninajua mahali unakoelekea, nami tayari nimekuwa na ninii yako yote. . . Ndiyo, "Na wana wenu na binti zenu watatabiri." Sasa, kama mchungaji wenu hajui maana ya jina "kutabiri," ha—hajui, hana shughuli sana nyuma ya mimbara, akijaribu kukwambia uwe mhubiri. Unaona? Maana kabisa, limekatazwa tangu Mwanzo hata Ufunuo. Sasa hebu niwaonyeshe hapa, mnaona.

133 Sasa ninawatakeni mfungue pamoja nami I Timotheo 2:11. Fungueni tu hapa nasi tutaona hili sasa, na tutapata jambo hili hapa, pia Matendo yako 2. Na mninii tu—msikilize tu hapa yale Maandiko yanayowaambieni juu ya somo hili.

134 Sasa, mtu fulani alikazana kusema, "Vema, Ndugu Branham, wewe ni mzee mwenye kuchukia wanawake." Mimi siwachukii wanawake. Mimi ni ninii. . . Sitaki tu kuwaona wanawake wakijaribu kupachukua mahali pasipo pao. Mnakumbuka huko kwenye Karakana ya Meli ya Howard huku,

moja ya karakana zilizofanikiwa sana kule kwenye Mto Ohio, walimweka mwanamke aiongoze, angalia jambo lililotukia. Walimpa mwanamke haki ya kupiga kura, angalia yaliyotukia.

135 Hebu niwaambie papa hapa sasa hivi. Sio kuwachuna wanawake, ninataka wanaume wafahamu ya kwamba mmo kwenye jambo hili pia. Lakini hebu nikwambie jambo fulani, ndugu, taifa hili ni taifa la mwanamke. Nitawathibitishia hilo kwa ninii yako, kwa Maandiko, kwa cho chote unachotaka nikuthibitishie kwacho. Ndivyo lilivyo. Ni kitu gani kilicho kwenye fedha zetu? Mwanamke. Linapatikana wapi hapa katika Ufunuo, mnapoliona? Hili ni namba kumi na tatu, pia, kila kitu lilichoanza. Nyota kumi na tatu, milia kumi na tatu, koloni kumi na tatu, kumi na tatu, kila kitu kilikuwa kumi na tatu kwanza. Linapatikana katika mlango wa 13 wa Ufunuo. Mwanamke, kumi na tatu!

136 Na katika mwaka wa 1933 wakati Bwana, tulipokuwa na mikutano mahali hapa ambapo Kanisa la Kristo linasimama sasa, ile nyumba ya kale ya Masonic, ono la Bwana lilinijia hapa na kutabiri ya kwamba, "Ujerumani ingeinuka na kujenga ile Ngome ya Maginot pale." Wengi wenu mnakumbuka jambo hilo. "Na jinsi wao wangejizungushia hapo ndani, na Wamarekani wangepigwa sana papo hapo kule kwenye hiyo ngome. Na pia nikasema yatakayotukia, na juu ya Roosevelt na mambo hayo, jinsi yeye angepigiwa kura na kuingia katika zamu hiyo ya nne." Sawa kabisa, ni sawa kabisa jinsi tu ilivyotukia. "Na pia nikasema ya kwamba motokaa zingeendelea kuwa na umbo la yai, mpaka katika siku za mwisho zitakuwa tu katika umbo la yai." Sasa Yeye alisema, "Itakuwa ya kwamba magari hayo hayataendeshwa kwa usukani, yataongozwa na kitu fulani kingine. Hayo ndiyo magari wanayotengeneza hivi sasa, yanayoongozwa kwa rimoti, kwa ajili ya usalama. Hiyo ni kweli. Hutaweza kuingia katika mji wakati huo, eneo la maili ishirini, unaweza tu kwenda maili ishirini. Huwezi kugonga gari lingine, kwa sababu linaongozwa kwa rimoti. Unaona, hivyo ndivyo mambo yanavyoendelea hivi sasa. Tena nikasema, "Kumbukeni, katika siku hiyo, kabla ya wakati wa mwisho kuja, kabla ya wakati wa mwisho kuja, ya kwamba mwanamke . . . Sasa, ninyi nyote andikeni jambo hili. Kutakuwako na mwanamke mmoja mkubwa mwenye nguvu atakayeinuka, ama atakuwa Rais, ama dikteta, ama mwanamke fulani mkubwa mwenye nguvu katika Marekani hii. Nayo itazama chini ya ushawishi wa wanawake. Sasa, kumbukeni, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI."

137 Mnaona, na iko makosani. Tena imeachilia kitu gani kiingie? Hebu niwaambieni. Iweni wa kiroho, hebu fungukeni, angalieni. Kwa nini inafanya jambo hilo? Kusudi iwape kanisa Katoliki nafasi ya kuingia. Mnaona? Mnaabudu hawa wachezaji wa sinema na mambo haya mengine yote mbalimbali huku nje. Mnakumbuka somo nililohubiri? Margie, unakumbuka,

miaka mingi iliyopita juu ya ku—kuvamiwa kwa Marekani na kupinduliwa kwa Serikali ya Marekani. Na jinsi ambavyo nilisema ya kwamba aliinuka huko Paris baada ya sisi kuwaokoa kule kutoka kwa wanawake hao, mvinyo na starehe, kisha akawaka akaingia moja kwa moja Hollywood. Sasa badala ya sisi kuagiza Paris tupate mitindo, wao wanaagizia hapa wapate mitindo. Ilifanya nini? Ilifikia. . .Hatungewaruhusu watoto wenu waende wakaone sinema, lakini iliingia moja kwa moja kwenye televisheni, ikaendelea moja kwa moja na kuchafua jamii yote, ikamaliza taifa kabisa. Na sisi hapa leo wasichana wote wadogo na wavulana wote wadogo wakionekana kama na namna fulani ya hawa wachezaji wa televisheni. Ni nini? Ni kutengeneza njia. Jamani, mwanamke mmoja mwenye tabia mbaya anaweza kuwapeleka watu wengi zaidi kuzimu kuliko baa zote ungaliweza kuanzisha katika mji mmoja. Hiyo ni kweli. Mwangalie akishuka kwenda barabarani akiwa amevua nguo zake zote, sijali mwanamume huyo ni nani, kama yeye ni mwanamume mwenye afya na timamu, wakati anapomwangalia mwanamke huyo hana budi apate kitu fulani kitakachopita ndani yake. Sasa iweni tu waaminifu. Sijali.

138 Nimekuwa na Roho Mtakatifu kwa miaka kadha. Huwezi kumwangalia mwanamke naye amevaa nguo nusu. . . Mi—mimi hubeba msalaba mdogo katika gari langu, wengi wenu mumeuona. Mtu fulani aliniambia, “Je! wewe ni Mkatoliki?” Wakatoliki walipata wapi haki ya pekee ya msalaba? *Msalaba* maana yake ni “Mkristo.”

139 Maskini hao akina Mtakatifu Cecelia na kadhalika ndio alama ya Ukatoliki. Sisi hatuamini takataka za namna hiyo. Tunamwamini Kristo. Wana kila namna ya watu wafu wanaowaabudu. Ni uabudu mizimu wa hali ya juu. Ndivyo ilivyo, kuabudu wafu. Hakuna kitu kama hicho, la.

140 Nilimwuliza kasisi huyo, nikasema, “Kwa nini basi—basi kama. . . Ati Petro alikuwa Papa wa kwanza?”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

141 Nikasema, “Basi ni kwa nini Petro alisema, ‘Hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na mwanadamu ila Mtu huyo Yesu Kristo.’ Nanyi mna wanawake elfu tano waliokufa na kila kitu ambao mnawafanya wapatanishi. Sasa ni kitu gani kimetukia?” Haya basi oneni. Wao hawana jawabu la jambo hilo. Hiyo ni kweli.

142 Na sasa baadhi ya mafundisho yao, mafundisho yao ya uongo, kundi la manabii wa uongo wa Kiprotestanti wamekuja na wanafundisha jambo hilo, nanyi Waprotestanti mnameza hayo. Hiyo ni kweli kabisa. Madhehebu na namna za mabatizo, na desturi mbalimbali na kadhalika mnazopitia, ambazo si za Kimaandiko kabisa. Maandiko yanapinga jambo hilo, hata hivyo mnayazingatia. Ni kweli.

143 Sasa sikilizeni jambo hili juu ya wahubiri wanawake. Vema, jambo la kwanza lingekuwa, ninataka ninii—I Timotheo 2:11. Sasa sikilizeni kile inachosema hapa.

> *Wanawake* wenu *na wajifunze katika utulivu. Wakitii kwa kila namna.*
>
> *Lakini simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu.*

144 Mimi sihusiki katika kuliweka mle ndani. Mimi ninawajibika kuwaambia kwamba liko mle ndani. Mnaona? Mnaona?

> *Wanawake* wenu *na wajifunze katika utulivu, na wakitii kwa kila namna.* (Kama uliwahi kwenda katika kanisa la Kiorthodoksi na kuwaangalia, unaona. Unaona?)
>
> *Lakini simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala* (kuwa mchungaji, shemasi, au kitu cho chote kama hicho) *mwanamume*, unaona, *kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu.*
>
> *Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye.*

145 Je! mlipata kujua. . .Sasa sikilizeni, enyi wanawake. Ninyi wanawake Wakristo wazuri na wenye haki ndio kitu kizuri sana ambacho Mungu angaliweza kumpa mwanamume kama sivyo angempa kitu kingine tofauti. Naam, bwana. Unaona? Mwanamke hata hakuwa katika ule uumbaji wa asili. Mwanamke si kitu kilichoumbwa cha Mungu. Yeye ni zaotuka la mwanamume. Mungu alimuumba mwanamume akiwa mwanamume na mwanamke pia. Ndipo akawatenganisha, na baada ya mwanamume kuwa ameishi duniani na kuwapa wanyama majina na kuishi hapa kwa muda mrefu, Yeye alitoa ubavu kutoka ubavuni mwa Adamu kama zaotuka na kuufanya mwanamke kutoka kwake. "Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye." Sasa angalia.

> *Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika kukosa.*

146 Mungu alimchukua mwanamume; Ibilisi akamchukua mwanamke. Angalia jambo hilo moja kwa moja usoni. Ni kitu gani kinachofanya hivyo leo? Liangalie kanisa halisi la Mungu, litasema, "Yesu!" Mpinga-Kristo atasema, "Maria!" Ziangalie hizo roho, unaona, hizo hapo. "Salamu Maria, mama wa Mungu, umbebarikiwa kati ya wanawake, na utuombee sisi wakosefu sasa na saa ya kufa kwetu. Amina." Ati Maria anaomba? Loo, ha, jamani! Unaona, haya oneni basi, "wanawake," raia wa Ibilisi. Kristo, kitu cha kuabudiwa, na yeye peke Yake! Oneni basi, haya oneni.

147 Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye. Adamu hakudanganywa. Na basi ungewezaje kuwa na mchungaji mwanamke, shemasi? Adamu hakudanganywa, lakini mwanamke alidanganywa. Yeye kweli yeye . . . Yeye hakufikiri alikuwa amekosea, lakini alikuwa amekosea. Mwanamke kwa kudanganywa aliingia katika kukosa. Kwa sababu wao ni . . . Kila wakati ambapo ma—mazishi yanapopitia barabarani, mwanamke aliyasababisha. Kila wakati mtoto mchanga anapopiga makelele, mwanamke alikusababisha. Kila wakati mtu fulani alipokufa, mwanamke alisababisha. Kila mvi, mwanamke alisababisha. Kila kitu, na mauti, mwanamke alisababisha. Kila jambo lililo baya, mwanamke alilisababisha. Halafu eti mumfanye kichwa cha kanisa, mchungaji, loo, askofu wakati mwingine. Na aone aibu.

148 Sasa hebu niwaelekeze kwenye kingine, kwa muda kidogo tu, unaona. Sasa hebu na tufungue I Wakorintho 14:32 pale, tuone yale Paulo anayosema hapa, na halafu tunaenda moja kwa moja kwenye mengine katika tu muda mfupi. Na halafu hatutaki kuwaweka kwa muda mrefu sana, mpaka mtakuwa mmechoka sana asubuhi hamwezi kurudi. Vema, ninataka kusoma. Ni wangapi wanaamini ya kwamba Paulo alikuwa mwalimu aliyevuviwa? Sasa, kumbukeni, Paulo aliandikia Timotheo jambo hili pia. Mnaona? Hiyo ni, sasa, I Wakorintho 14:32. Sasa hebu tuanzie moja kwa moja hapa na tuanze kusoma hapa, 14:34, ninaamini.

> *Wanawake* wenu *na wanyamaze katika kanisa,* . . .

149 Je! ulisikia alilosema?

> *Wanawake wenu na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena; bali* wameamrishwa *watii,* . . .

150 Je! una maneno ya pambizoni juu ya hicho? Kama unayo, rejea nyuma uone kama hayakupeleki kwenye Mwanzo 3:16. Wakati Mungu alipomwambia Hawa, kwa sababu alikuwa amemsikiliza yule nyoka badala ya mumewe, ya kwamba mumewe angemtawala siku zote za maisha yake. Mwanamke anawezaje kuja na kumtawala mwanamume, awe mchungaji ama shemasi, wakati Biblia ilisema "na awe mtiifu" kama tu ilivyokuwa hapo mwanzo wakati Mungu . . . Mungu hawezi kubadilika. Huwezi kulifanya Neno liseme jambo moja *hapa* na lingine *hapa*. Halifanyi hivyo. Ni jambo lile lile wakati wote. Kwa hiyo hapo mwanzo, hapo ndipo . . .

151 Kabla jambo hili halijaisha, kama nikipata nafasi, ninataka kunyosha kisa hicho cha hiyo ndoa na talaka kwenu. Sijawahi kufanya jambo hilo katika kanisa hili bado. Lakini angalieni agano hili la maradufu. Mmoja anasema mwanamke anaweza kuolewa, na huyo mwingine alisema mwanamume hawezi kuoa, na huyu anasema *hili, lile*, ama *jingine*. Hebu ngoja tu kidogo

uone jinsi Biblia inavyosema tutakapofikia jambo hilo. Unaona? Vema. Sasa angalia hapa.

> *Wanawake* wenu *na wanyamaze katika makanisa,. . . . hawana ruhusa kunena; bali wameamrishwa kutii, kama vile inenavyo torati nayo, . . .*

152 Basi, katika Agano la Kale wao hawakuruhusiwa kunena, maana Paulo alisema hapa hawakuruhusiwa. Hiyo ni kweli? "Wanawake wenu na wanyamaze, ni kutii." Sasa kama unataka kurejea kwenye maneno yako ya pambizoni hapo, rudi katika Mwanzo 3:16. Unaona? Vema. "Chini ya ninii, kama ilivyo chini ya torati."

> *Nao wakitaka kujifunza neno lo lote, na* ninii wao . . . *wawaulize—wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu* mwanamke *kunena katika kanisa.*
>
> *Au je*? . . .

153 Sasa angalieni alama hiyo ya kuuliza katika kila moja ya Biblia zenu juu ya hilo "Au je?" Ni kitu gani kilichomfanya Paulo kusema jambo hilo na kutenda namna hiyo? Sasa, kama utawahi kupata zile barua ambazo Wakorintho walimwandikia Paulo. Sasa, unaweza kuzipata katika maktaba yo yote nzuri. Unaona, ambazo Wakorintho walimwandikia Paulo, walizomwandikia na kumwambia. Baada ya wanawake hawa walioongoka . . . Walikuwa na—na mungu mke kule aliyeitwa "Diana," naye alikuwa wa Efeso, pia. Nao Wakorintho walimwabudu yuyo huyo, maana ilikuwa ni ibada ya kipagani. Nao walipata jiwe huko nje kondeni siku moja, lilikuwa na umbo kama la mwanamke. Wakasema, "Mungu ni mwanamke, naye alishusha sanamu yake kwetu." Na hekalu lake lilikuwa zuri sana kupita lile la Sulemani, ndivyo walivyosema, wanahistoria. Loo, lote lilikuwa la marmar, iliyotiwa dhahabu kwa njumu; ambapo, hekalu la Sulemani lilijengwa kwa mierezi iliyotiwa njumu. Unaona? Na lilikuwa zuri kwa mbali sana! Na jambo hilo, basi, kama Mungu alikuwa ni mwa—mwanamke, mbona, hakika, angeweza kuwa na makuhani wanawake. Hakika, kama Mungu ni mwanamke, basi mhubiri mwanamke ni sawa. Lakini Mungu ni Mwanamume, Biblia ilisema yeye alikuwa Mwanamume ni. Yeye ni Mwanamume. Unaona? Na kama Mungu alikuwa ni Mwanamume, basi haina budi kuwa ni mwanamume.

Sasa angalia hapa, "Au je?"

154 Sasa, baadhi ya hao makuhani wanawake, walipoongolewa kutoka upagani wakaingia katika Ukristo, walifikiri wangeweza kudumisha vyeo vyao kama mhubiri, waje tu upande huu. Kama walihubiri kule juu ya Diana, walikuja huku na kuhubiri juu ya Kristo.

155 Akasema, "Au je? Neno la Mungu lilitoka . . . " Hebu sikilizeni tu jambo Hili. Ndugu, wahudumu wanawezaje kufanya jambo hilo? Kifungu cha 36.

*Au je! neno la Mungu lilitoka kwenu? au kuwafikia ninyi peke yenu?*

*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni*, (hata haimbidi kuwa nabii; mtu mwenye mawazo ya rohoni tu,) *na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana*. (Unaamini jambo hilo?)

*Lakini kama* yeye . . . kama mtu ye yote *akiwa mjinga,* hebu tu *na awe mjinga*.

156 Sasa, hayo ni hakika tu kama ninavyojua kuyaweka. Unaona? Akasema, "Kama mtu ni mtu wa rohoni, ama nabii, atatambua ya kwamba ninayoandika hapa ni Maagizo ya Bwana." Lakini alisema, "Kama yeye—kama atakuwa mjinga, na awe mjinga tu." Unaona, jambo pekee unaloweza kufanya. Kama wanataka kuendelea na jambo hilo, itakubidi tu kuwaacha waendelee nalo, maana aliona jambo hilo likianza kule.

157 Na mwanamke fulani aliniambia, akasema, "Loo, Paulo alikuwa tu maskini mchukia wanawake."

158 Yeye hakuwa mchukia wanawake. Mnajua, Paulo alikuwa mtume, na kwa kanisa la Mataifa. Angalia hapa. Je! ulijua Paulo . . . Ni wangapi wanaamini ya kwamba hayo ndiyo Paulo aliyohubiri? Hayo ndiyo a—aliyosema hapa? Basi Paulo akasema . . .

159 Unasema, "Vema, ngoja kidogo sasa, Ndugu Branham. Ngoja kidogo! Sasa, askofu wetu anasema ya kwamba hilo ni sawa. Msimamizi mkuu, kusanyiko wanasema ni sawa. Askofu wa umoja anasema ni sawa."

160 Sijali wanayosema, ni uongo! Na niliwaambia tutashindilia hili kwelikweli. Na manabii wa uongo wangesema hivyo. Kwa maana Biblia ilisema, "Kama mtu akijiona kwamba yeye ni wa rohoni, ama ni nabii, na atambue ya kwamba ninayosema ni Maagizo ya Bwana." Na iwapo roho yake haishuhudii pamoja na Neno hilo, yeye ni nabii wa uongo kwanza. Afadhali niwe mchukia wanawake kuliko mpenda wanawake, niingilie upuuzi kama huo, kuvumilia upuuzi kama huo, kanisa la Mungu likipingana na maagizo ya Mungu. Ndipo Paulo akasema, hebu fungueni Wagalatia 1:8, Paulo alisema, "Kama malaika kutoka Mbinguni akiwahubiri ninyi Injili nyingine yo yote isipokuwa ile niliyowahubiri, na alaaniwe." Sasa utafanya nini juu ya jambo Hilo?

161 Sasa unasema, "Vipi mahali ambapo lilisema, 'Wana wenu na binti zenu watatabiri,' katika Yoeli, na—na ambapo Paulo alinukuu katika Siku ya Pentekoste?" Hiyo ni kweli kabisa.

162 Je! ulijua, katika Agano la Kale, ya kwamba njia pekee, na njia pekee sasa, ambapo mtu ye yote anaweza kuingia katika agano kupitia, kwa . . . Ibrahimu ndiye aliyepewa ile ahadi, na—

na ule muhuri wa ahadi ulikuwa ni tohara. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Hiyo ilikuwa ni Mungu akithibitisha.

163 Kama vile ndugu Mbatisti, yeye alisema, "Ndugu Branham, mbona, sisi Wabatisti tumempokea Roho Mtakatifu."

Nikasema, "Mlimpokea lini?"

Kasema, "Saa tuliyoamini."

164 Nikasema, "Paulo alisema, 'Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?'" Mnaona? Nikasema, "Sasa, ninyi Wabatisti njoni mumpate Huyo kidogo, nasi tutazungumza juu ya usalama wa Milele pamoja," nilisema.

"Lakini, sawa, unalipata wapi namna hiyo?" Unaona?

165 Alisema, "Je! mmepokea Roho matakatifu *tangu* mlipoamini?" Wao walikuwa ni waamini, na walikuwa wakipiga makelele na furaha na cho chote kile. Hawakuwa wamempokea Roho Mtakatifu bado, Paulo alisema hawakuwa wamempokea. Unaona? "Mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Wakasema, "Hatujui kama kuna Roho Mtakatifu ye yote."

Kasema, "Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?"

166 Wakasema, "Tumebatizwa." Lakini kwa uongo, unaona, ilibidi tu abatizwe tena. Vema.

167 Sasa angalia jambo hili sasa, ya kwamba wahubiri hawa wa kike, walipoingia, walifikiri wangechukua mamlaka yao. Lakini hairuhusiwi kabisa na Mungu kufanya jambo hilo. Na hebu . . . wakati tu tukiwa papa hapa kwenye somo hili hapa, wanawake hawa, unaona, tukiwa katika hilo. Sasa, Lenyewe lilisema, "Kama kuna mtu ye yote kati yenu, ambaye ni wa rohoni, ama nabii, na atambue ya kwamba yale ninayoandika ni Maagizo ya Bwana. Lakini kama yeye ni mjinga, na awe tu mjinga." Na hiyo ndiyo sababu ninii . . . maskani hii haisimami na kuwaweka wakfu kwa huduma wahubiri wanawake, mashemasi wanawake, ama jambo lo lote la kufanywa na mwanamke kama cheo cha kanisa hili, ni kwa sababu Maandiko haya yanaliweka hapa na ni wazi kabisa.

168 Sasa, Biblia ilisema, "Wana wenu na binti zenu watatabiri." Sasa, neno "kutabiri" lina maana gani? Liangalie. Ni "kusema jambo fulani, chini ya uvuvio," ama "kutabiri jambo fulani," ni neno lenye maana mbili.

169 Kama vile tu kutakasa kunavyomaanisha "kusafishwa, na kuwekwa kando kwa ajili ya kutumika," Unaona? Ama, ni neno lenye maana mbili likimaanisha zaidi ya jambo moja, kama tulivyo na mengi sana katika Kiingereza hapa.

170 Kama vile, tuseme neno "board" (ubao). Vema, *board* lingemaanisha nini? Unasema, "Vema, yeye ana maana kwamba alilipa *board* (malazi) yake." "La, hakumaanisha hivyo, alimaanisha yeye (alichimba) *bored* shimo. "La, hakulichimba,

alimaanisha yeye (alimchosha) *bored*." Ama, unaona, ni neno tu, nawe huna budi kujua unachozungumzia. Unaona?

171 Na hivyo ndivyo lilivyo hili, Neno hili lenye maana mbili, ambapo, "Wana wenu na binti watatabiri." Sasa, njia pekee ambayo Mungu . . .

172 Huyu Mbatisti akasema, "Hakika, tumempokea Roho Mtakatifu." Nikasema . . . "Basi tulipoamini." Nikasema . . . Sasa, unaona, akasema, "Mungu alimpa Ibrahimu ninii . . . " Akasema, "Ibrahimu alimwamini Mungu." Hivyo ndivyo alivyosema. Alisema, "Ibrahimu alimwamini Mungu na akahesabiwa kwamba ana haki." Ni wangapi wanajua hilo ni kweli? Sasa angalia jinsi—jinsi Shetani anavyoweza kupenyeza hilo kwa urahisi kwa ndugu. Unaona, ni rahisi tu. Sasa, hayo ni Maandiko.

173 Ndugu, ninakwambia, katika jambo hili, ndani hapa juu, huna budi kutiwa mafuta kabla hujaiingia hii. Unapaswa kuingia mahali pa siri na kuomba. Watu wanasema, "Mbona usitoke nje uende ukawaone watu?" Ndugu, kama utaenda kuzungumza na watu, ama kuwafundisha, afadhali ukae peke yako na Mungu kwa muda kidogo kabla hujaingia kwenye hiyo mimbara. Kweli kabisa, unaona, maana Shetani ni mwerevu, ni mwerevu sana.

174 Akasema basi, angalia, akasema, "Ibrahimu alimwamini Mungu, na akahesabiwa kwamba ana haki." Hiyo ni kweli. Akasema, "Lakini, Ibrahimu anaweza afanye nini cha zaidi ila kuamini?"

Nikasema, "Hivyo ndivyo tu angaliweza kufanya."

175 Akasema, "Unaweza kufanya nini zaidi ama mtu ye yote mwingine anaweza afanye nini zaidi ila kuamini?"

176 Nikasema, "Hivyo ndivyo tu tunavyoweza kufanya. Lakini angalia, ndugu, ndipo Mungu akapatanisha, ama akatambua imani ya Ibrahimu. Akampa muhuri, ishara ya tohara kama muhuri wa agano. Unaona, Yeye alimpa. Akasema, 'Sasa, Ibrahimu, ninaitambua imani yako, kwa hiyo nitakupa ishara sasa ya kwamba nimekupokea.'"

177 Kwa hiyo akamtahiri Ibrahimu, na huo ndio uliokuwa mhuri wa hilo agano. Na sasa katika siku hii . . . Sasa, mwanamke hangeweza kuwa katika agano hilo; ni mwanamke aliyeolewa tu. Tafuta uone, hungeweza kumtahiri mwanamke; kwa hiyo ilibidi kuingia, kwa hiyo yeye pamoja na mume wake ni mmoja. Si wawili tena; wao ni mmoja. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Maandiko yanasema jambo hilo. Kwa hiyo yeye akiwa ameolewa, basi yeye—yeye wanakuwa mmoja. Basi endelea hapa mbele uangalie hapa katika Timotheo, alisema jambo lile lile, kasema, "Walakini ataokolewa katika kuzaa watoto, kama akidumu katika imani na utakatifu, pamoja na moyo wa kiasi."

178 Sasa, lakini basi, tohara ya Agano la Kale ilikuwa katika mwili, lakini katika Agano hili Jipya, Yoeli alisema, "'Nitamimina Roho Yangu juu ya watu wote wenye mwili, na wana wenu na binti zenu watatabiri.'" Sasa, neno *kutabiri* halimaanishi kufundisha. *Kutabiri* linamaanisha aidha "kusimulia tukio, chini ya upako," ama "kutabiri jambo fulani litakalotukia." Nasi tunajua ya kwamba kulikuwako na manabii wa kike katika Agano la Kale. Hawangezungumza ndani ya jengo kamwe, kuzungumza kanisani, katika kusanyiko, kama mwalimu. Lakini, unaona, Ana na wengi wao huko hekaluni, wao walikuwa manabii wa kike, na Miriamu alikuwa nabii mke ama kitu kama hicho. Yeye alikuwa na Roho juu yake, hiyo ni kweli, lakini mahali pake palikuwa na mpaka. Wanawake wanaweza kuwa manabii leo, kweli kabisa; lakini si waalimu, na kadhalika, nyuma ya mimbara hapa. Ukifanya jambo hilo, unaifanya—unaifanya Biblia ijipinge Yenyewe. Biblia haiwezi kusema jambo moja *hapa*, na jambo jingine *hapa*. Haina budi kusema jambo lile lile wakati wote la sivyo si Neno la Mungu. Unaona? Kwa hiyo, "Wana wenu na binti zenu watatabiri," inamaanisha ya kwamba wao aidha "watabashiri" ama "kushuhudia." Sasa, hebu angalia jambo hilo, halafu uchukue kamusi ya Biblia uone kama jambo hilo si kweli. "Wana wenu na binti zenu watatabiri."

179 Sasa, Biblia pia inanena juu ya mwanamke ambaye alijifanya, ama alidai ya kwamba yeye . . . Hili lingetumika kwa kanisa Katoliki, na lingetumika pia kwa ninii—kwa somo hili dogo tutakalozungumzia sasa. Hebu tufungue kwenye Kitabu cha—cha Ufunuo, na hebu tuchukue m—mlango wa 2 na kifungu cha 20, wakati tu tukangali papa hapa karibu na jambo hilo, ili kwamba mpate kuona hapa na mwone tu jinsi hilo linavyoweza kuwa la kiibilisi, kwa kunena katika siku hizi za mwisho yale yatakayotukia, jinsi ambavyo hizi, jinsi mwanamke huyu angalikuwa. Kumbukeni, kanisa Katoliki ni mwanamke. Tumesoma hilo hivi sasa, sivyo? Sikilizeni hili sasa, jinsi Hiyo inavyosema, Ufunuo 2:20, "Walakini sasa . . . " Yeye analizungumzia kanisa hili la Thiatira, unaona, "walakini sasa," ambalo ni kanisa la wakati wa katikati pale, lililopitia katika Nyakati zile za Giza.

> Walakini sasa *nina mambo machache juu yako, ya kwamba wamridhia yule mwanamke Yezebeli, yeye ajiitaye nabii kuwafundisha na* . . . kuwatiisha *watumishi wangu na* kufanya uzinzi *na kula vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu*. Unaona?

180 Sasa, kama umewahi kuangalia, angalia nyakati hizi za kanisa, kisha tutafunga. Na ndipo asubuhi tutayachukua mambo haya mengine. Angalia. Katika . . . Chini ya vinara vya taa vya dhahabu vya maskani ya Kiyahudi, kule ndani, kwenye ule mkate wa wonyesho na kadhalika, kulikuwako na vinara

vya taa saba vya dhahabu. Ninyi nyote mnajua jambo hilo, mnaona. Na kuna nyakati saba za kanisa. Hizo zinawakilisha nyakati saba za kanisa vivyo hivyo. Sasa kama ukiangalia katika Ufunuo 1, tunamwona Yesu amesimama katika nyakati saba za kanisa, vile vinara vya taa saba vya dhahabu, wakati alipogeuka na kuona Mtu kama Mwana wa Adamu amesimama amevikwa ninii. . .Jinsi ilivyokuwa, ilikuwa ni Bibi-arusi amesimama katika vile vinara vya taa vilivyotokeza.

181 Sasa, katika Agano la Kale, wangechukua hivi ninii, taa hii moja na kuiwasha, na kuchukua taa hiyo nyingine na kuwasha hiyo nayo, wakawasha hiyo nyingine, moja kutoka kwa nyingine namna hiyo, mpaka wakamaliza hivyo vinara vya taa saba vyote.

182 Kama ukiangalia hapo mwanzo, wakati Mungu alipoanza kushughulika na Wayahudi, nao wakapitia katika ule wakati wa ufanisi. Na halafu wakati wa giza sana wa kushughulikiwa kwa Wayahudi, ambao Mungu aliutumia kwa Myahudi, ilikuwa ni katika utawala wa Ahabu. Na kama mtaangalia, tukisoma nyakati hizo za kanisa pale, Yeye anarudi moja kwa moja kwa hizo tena. Alisema, sasa, mambo machache yaliyopita, na kusema. Sasa, moja kwa moja katika Wakati huo wa Giza, miaka elfu moja mia tano kule, ama ule wakati wa Ahabu, kwanza, na wa Wayahudi. Wakati wa giza sana waliopata kuwa nao, wakati Ahabu alipomwoa Yezebeli na kuingiza ibada za sanamu katika Israeli, na kuwafanya watu wote waabudu kwa kumfuata Ahabu, wamwabudu mungu wa Yezebeli. Mnakumbuka, walichukua, wakaweka maashera, na wakavunja madhabahu za Mungu. Naye Elisha akalia, alikuwa ndiye "pekee," na Mungu alikuwa na mia saba ambao walikuwa hata kidogo bado hawajampigia Balaamu goti. Mnakumbuka hilo? Huo ni mfano wa lile Kanisa lililoteuliwa likitoka. Unaona pale, unaona jinsi ilivyo?

183 Sasa, katika kanisa hili, kama utaangalia kanisa la kwanza, kanisa la kwanza, kanisa la Efeso, lilikuwa kanisa kuu. Alisema, "U hai, bado." Na kama ukiangalia kila kanisa, lilianza kufifia, fifia, mpaka likafikia Thiatira. Halafu ile miaka elfu moja mia tano. Ndipo likatokea upande huo mwingine, "Na una nuru kidogo tu. Imarisha kile ulicho nacho, kinara chako cha taa kisije kikaondolewa." Ndipo ikaendelea kuja ikafikia basi kwenye wakati wa kanisa la Filadelfia, na halafu ikaingia katika wakati wa kanisa la Laodikia.

184 Sasa, huu hapa uzuri. Loo, jamani, ninapenda tu jambo hili, Ndugu Smith. Unaona, angalia jambo hili. Sasa, katika wakati huu wa kanisa, kama tulivyopitia. . .Sasa angalia jambo hili. Wakati ule wa kwanza wa kanisa ulikuwa wa Efeso, wakati wa Kanisa la Efeso. Sasa, kila moja ya nyakati hizo za kanisa, mpaka ilipofikia katika miaka hii elfu moja mia tano, kama utaangalia. . . Yasome sasa utakapoenda nyumbani usiku wa leo, kama ukiwa na wakati, ama asubuhi na mapema, kabla hujaja

kanisani, katika mlango wa 1, wa 2, na wa 3 wa Ufunuo. Utaona ya kwamba, kila moja ya nyakati hizo za kanisa, Yeye alisema, "Una nguvu kidogo, wala hujalikana Jina Langu," mpaka alipofikia kwenye miaka hii elfu moja na mia tano ya Thiatira, ule Wakati wa Giza. Ndipo akatokea upande wa pili, na kusema:

. . . una *jina ya kwamba* u hai, lakini *umekufa*.

185 Na hizi, hakuna moja ya nyakati hizi nyingine za kanisa, huo ama wakati wa kanisa wa Filadelfia, hawakuchukua Jina hilo tena. Kamwe hawakupata Jina hilo, maana lilipotea katika wakati huu. Sasa, loo, jinsi tungaliweza kuweka jambo hilo kwenye hayo mafundisho ya uongo sasa, pale pale, niwaonyeshe ya kwamba yeye ni mama, kanisa Katoliki ndilo mama wa kitu hicho chote, jinsi lilivyo "Mama, Babeli wa Siri." Na ndivyo ilivyo, angalia, wakati huu wa kanisa hapa wakati lilipotoka, lilikuwa na nuru kidogo, ndipo likaendelea kufifia, kufifia, halafu likafikia kwenye madhehebu zamani hizi, miaka hii elfu moja na mia tano. Nalo likatoka sasa, si kama kanisa la Bwana Yesu Kristo, lakini kama kanisa Katoliki. Luther alitoka namna gani? Kama kanisa la Kiluteri. Kanisa la Kibatisti lilitoka namna gani? Kama kanisa la Kibatisti. Si Jina Lake, si Jina Lake; jina jingine, "una jina." "Kwa maana hakuna jina jingine chini ya Mbingu ulilopewa likupasalo kuokolewa, ni Jina la Yesu Kristo tu." "Una jina kwamba unaishi, lakini umekufa," hiyo ni kwa madhehebu hayo.

186 "Loo, mimi ni Mpresbiteri," nawe umekufa! "Loo, mimi ni Mbatisti," na umekufa! Wewe ni hai tu jinsi unavyokuwa hai katika Kristo Yesu. Hiyo ni kweli. Na mabatizo yenu ya uongo katika maji, ubatizo wa uongo, kunyunyiza, kumimina, badala ya kuzamisha, ukitumia "Baba, Mwana na Roho Mtakatifu" badala ya Jina la Bwana Yesu Kristo. Mambo hayo yote ya uongo yakija dhahiri, Biblia ikinena, kama yanayomiminwa ndani yake ya chombo kwa bidii sana iwezekanavyo. Na hapa watu tunachukuana na mambo vizuri sana nayo, "Vema, kanisa langu linaamini jambo Hilo namna *hii*." Lakini Biblia inasema *Hivi*. Unaona? Hakuna cha hiyo, hakuna vitu kama hivyo.

187 Wala hakuna mahali katika Biblia ambapo waliwahi kutoa ulimi wao na kula ushirika mtakatifu, naye kasisi anywe divai na kuita ni Roho Mtakatifu. Kamwe katika Biblia hawajawahi kupeana mikono na kupeana mkono wa kuume wa ushirika na kuita ni Roho Mtakatifu. Kamwe mtu ye yote hakuwahi kusimama na kusema, "sasa mimi ni mwamini," na kupokea Roho Mtakatifu. Kama ilikuwa hivyo, hivi ndivyo Matendo 2 ingalisomeka, "Na hapo siku ya Pentekoste ilipotimia, huko barabarani akaja kasisi wa Kiroma, na ukosi wake umepinduliwa. Anakuja, na kasema, 'Ninyi nyote toeni ulimi sasa na mle ushirika mtakatifu, ushirika wa kwanza.'" Je! hiyo si ingekuwa ndiyo njia fulani ya kusoma Matendo 2?

188 Vema, ninyi Waprotestanti ni wabaya vile vile kama wao. Rudini kwenye siku hiyo, “Sasa tunapokuja kwenu ninyi Wamethodisti, mnawaweka kwenye mkono wa kulia, mnawapa mkono wa kuume wa ushirika, na miezi sita ya majaribio.” Unasoma hayo wapi katika Matendo 2? Unaona? Unapata wapi hayo? Unaona?

189 Imesema, “Wakati hao wote walipokuwa katika mahali pamoja na katika moyo mmoja!” Hapakuja askofu ye yote na kufanya *hivi*, wala kamwe hapakuja kuhani ye yote na kufanya *hivi*. “Lakini ulikuja uvumi kutoka Mbinguni kama Upepo wa nguvu ukienda kasi, nao ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.” Hivyo ndivyo walivyompokea, naam, bwana, kama upepo wa nguvu ukienda kasi ukitoka Utukufuni. Si kutokea huko barabarani ama kutoka kwenye madhehebu fulani.

. . . wewe una *jina ya kwamba* unaishi, ila *umekufa*.

190 Unaona, kanuni zenu za imani na madhehebu zimemzuia Mungu kwa namna hiyo, mpaka, “Tunaamini *hivi*, na tunaamini siku za miujiza zimepita.” Anayesema hivyo ni nabii wa uongo. Ni nabii wa uongo yeye anayekwambia “unaweza kupeana mikono na umpokee Roho Mtakatifu.” Anayekwambia “unampokea Roho Mtakatifu unapoamini ni nabii wa wongo.” Anayekwambia “unapaswa kumiminiwa na kunyunyiziwa badala ya kubatizwa,” ni nabii wa uongo. Anayekwambia “ubatizwe katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” wakati hakuna Maandiko kwake katika Biblia, ni nabii wa uongo. Hiyo ni kweli. Hakuna Andiko katika Biblia linalokwambia ubatizwe, ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa, ni kwa Jina la Yesu Kristo tu; ni wanafunzi wa Yohana tu, nao iliwabidi kuja na kubatizwa tena katika Jina la Bwana Yesu Kristo wapate kumpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Sasa, hilo si fundisho la Yesu Pekee; ninajua fundisho la Yesu Pekee, si hilo. Hilo ni Fundisho la Biblia hii. Hiyo ni kweli.

191 Lakini haya basi yaoneni. Utafanya nini na jambo hilo? Huyo hapo mama yenu. Huyo hapo mama wa kanuni hizo za imani.

192 Sasa, kama ukiangalia nyuma papa hapa katika Biblia na uniambie mahali mtu ye yote alipopata kunyunyiziwa. Ewe Mmethodisti, Mpresbiteri, Mkatoliki, niambie ni mahali gani mtu ye yote alipopata kunyunyiziwa, katika Biblia. Niambie mahali ambapo mtu aliwahi kumiminiwa, katika Biblia, kwa ondoleo la dhambi. Patajeni. Je! unaweza kupapata? Kama unaweza kupapata, njoo kwangu, nami nitashuka nitembee kwenye barabara hii nikiwa na kibao mgongoni mwangu, na niseme, “nabii wa uongo, nimekosea.” Ama upate mahali pamoja katika Biblia nzima ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, jinsi asilimia themanini yenu mlivyobatizwa. Nipatieni Andiko

moja ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa namna hiyo, nami nibandike kibao mgongoni mwangu, “nabii wa uongo,” na nishuke nitembee barabarani nikiwa nayo namna *hii.* Na unionyeshe mahali ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa, katika lile kanisa jipya, ambaye haikumbidi kuja na kubatizwa tena katika ninii . . . si katika Jina la Yesu Pekee, lakini katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Angalia uone kama jambo hilo si kweli.

193 Na, hapa, ni kitu gani? Yeye alikuwa ni mama wa makahaba. Ni kitu gani kilichomfanya malaya? Ni kitu gani kilicho mfanya kahaba? Mafundisho yake! Ni kitu gani kilichowafanya makahaba? Fundisho lake!

194 Na hiyo ndiyo sababu hatuyavumilii madhehebu yao na mafundisho yao ya sharti. Tunakaa wasafi kwa Biblia hii. Sijui mnaliishi vizuri jinsi gani, lakini mnaifundishwa Hiyo, hata hivyo. Vema. Hiyo ni juu yenu. Siwezi kuwafanya muiishi. Ninaweza tu kuwaambieni iliyo Kweli. Hiyo ndiyo sababu sisi si madhehebu. Nisingetaka—nisingetaka tujitie unajisi kwa kujiingiza katika upuuzi kama huo, kwamba itubidi tujifunge na namna fulani ya mafundisho ya sharti. Afadhali nishike njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Afadhali nidumu msafi na mtakatifu mbele ya Neno na Mungu, na kusimama pale, na kusema hakuna damu ya mtu ye yote kwenye nguo yangu. Hiyo ndiyo sababu tunakaa kwenye Maskani ya Branham. Hiyo ndiyo sababu sisi si Waasemblies. Hiyo ndiyo sababu sisi si wa Umoja. Hiyo ndiyo sababu sisi si wa Yesu Pekee. Hiyo ndiyo sababu sisi si wa Methodisti. Hiyo ndiyo sababu sisi si Wabatisti. Ni maskani ndo—ndogo tu hapa. Hatuna madhehebu yo yote, hata kidogo. Sisi ni huru, katika Kristo. Hiyo ndiyo sababu tunakaa jinsi tunavyokaa. Na Mungu ametubariki na Mungu anatusaidia.

195 Sasa, tunaweza kuwaambia ni kwa nini tunakula ushirika, tukwambie kwa nini tunaadhimisha kutawadha miguu, kwa nini hatuwaruhusu washiriki wale kama tunajua wao wako katika dhambi. Na hiyo ndiyo sababu majuma haya mawili ama matatu nimekuwa nikienda kutoka kwa mshiriki mmoja hadi kwa mwingine, ambapo mmekuwa na makelele yenu madogo hapa pia. Nikizunguka, mmoja hangezungumza na mwingine, wanapitana barabarani na kugeuza kichwa chao, oneni aibu, ambao mmekunywa kikombe kilichobarikiwa cha Mungu hapa, madhabahuni hapa. Na kuwafanya ninyi ndugu na dada na hao wengine kuchukua simu na kusengenyana ninyi kwa ninyi, hufai kuitwa Mkristo ukiwa namna hiyo. Kweli. Acheni hizo simu, kama huwezi kunena mema juu ya mtu fulani usizungumze kabisa. Kumbuka, Mungu atakuwajibisha. Mradi tu roho wa aina hiyo yumo ndani yako, unajua hauko sawa na Mungu. Na kama hujisikii . . .

196 Kama mtu amekosea, mwendee, mkapatane. Kama huwezi kupatana naye, mchukue mtu mwingine. Si ajabu Mungu

hawezi kuliadibisha kanisa Lake, maana hamfanyi jambo hilo sawa. Badala ya kwenda kwenye simu na kumzungumza *huyu*, *mambo* yaliyotukia, na vikundi vidogo vidogo vya kujitenga na kadhalika, hapa namna hiyo. Badala ya kufanya jambo hilo, kwa nini msifanye yale Biblia isemayo? Kama ndugu fulani ameghalifika katika kosa fulani, mwendee uone kama huwezi kupatana naye. "Vema, sasa alinifanya!" Sijali alifanya nini, mwendee hata hivyo! Haikusema yeye akujie. Wewe mwendee kama amekosea. Unasema, "Vema, yeye alikuwa makosani, alipaswa kunijia." Hivyo sivyo Biblia ilivyosema. Biblia ilisema wewe umwendee. Kama amekosea, mwendee.

197 Halafu basi kama hatakusikiliza, basi chukua mtu mwingine kama shahidi.

198 Halafu kama hataki kumwona huyo shahidi, basi, useme, sasa nitamchukua mchungaji wako. Ndipo umwambie, "useme, nitaliambia kanisa, na katika siku thelathini kutoka sasa, kama ninyi ndugu hamjasuluhisha hilo . . . Huyu ndugu hapa anataka kupatanishwa. Wewe hutaki. Na kama hutasuluhisha jambo hilo katika siku thelathini, basi jambo litakalotukia, wewe si mmoja wetu tena."

199 Biblia ilisema, "Kama hatalisikia kanisa, basi na awe kwenu kama kafiri na mtoza ushuru." Unaona, mradi ndugu yuko chini ya ulinzi huo wa kanisa, Damu ya Kristo inamlinda. Hiyo ndiyo sababu hatulioni kanisa likitembea jinsi linavyopaswa. Sasa, mimi sininii . . . Hili ndilo fundisho la Wabatisti—la kanisa la Kibatisti, ama la Maskani ya Branham hapa, kama mtafanya hivyo. Mnaona, kwa nini . . .

200 Unafika hapa na kusema, kwa mfano, watu wawili, tuseme mimi na Leo. Vema, huna budi kusema . . . nami ninasema, "Vema, yeye—yeye alinikosea." Hilo halileti tofauti yo yote, nami ninapaswa kumwendea. Vema, yeye ni mshiriki wa kanisa hili. Yeye—yeye amekuwa Mkristo. Anakula ushirika hapa ukingoni mwa madhabahu pamoja nami. Nasi tumebatizwa katika Jina la Bwana Yesu. Tukatembea kwa uaminifu kama ndugu mbele ya mwingine, kisha jambo fulani likatukia.

201 Si mtu huyo, asilimia tisini mara nyingi ni Ibilisi aliyeingia katikati ya hao watu. Si hao watu, ni Ibilisi. Na mradi tu unamwacha Ibilisi afanye jambo hilo, unamdhuru ndugu yako. Hiyo ni kweli.

202 Sawa, kuna kasoro kati yangu na Leo, hebu twende tukalisuluhishe. Na kama ukiona kuna jambo fulani, ni juu yako kuja kwetu, na kusema, "Ninyi wavulana wawili njoni hapa mkutane, tutalitatua hili. Sasa, halafu kama ikifikia hapo—hapo, tunakuja kuona kwamba basi, sisi hapa, ninasema vema, jambo la kwanza, kama sisi—hatuwezi kupatana, basi mnakuja kanisani namna hiyo.

203 Halafu basi kama mradi tu hufanyi jambo lo lote juu yake, loo, Damu ya Yesu Kristo inatukinga sisi wawili. Unaona? Lakini basi hiyo—hiyo kansa ya kale itaanzisha kansa nyingine, na kansa hiyo itaanzisha kansa nyingine, na kitu hicho chote kitakuwa kigonjwa juu ya kanisa lote. Ndipo unafikia mahali unakuja kanisani, na ni baridi tu, itawabidi kumwacha bawabu aje kuvunja barafu kabla kusanyiko halijaingia. Sasa, unajua jambo hilo ni kweli. Na ni baridi! Mtu fulani anaketi, unajua, na asiseme kitu. "Tulikuwa wa kiroho sana." Vema, ni nini kilitokea? Ulipiga mbio vizuri, kulikuwa na kitu gani? Unaona, dhambi zenu zinawatenga. Mungu anawawajibisha kwa jambo hilo, ndugu. Sasa nyosheni jambo hilo.

204 Hakuna kitu kibaya kwangu, hakuna kibaya kwa Leo; ni Ibilisi alipenyeza kati yetu. Hiyo ni kweli. Nyosheni jambo hilo. Mwendee. Ndipo kama hatasikiliza, au mimi sitasikiliza, vyo vyote vile, basi liambie kanisa. Kama haji apate kupatanishwa na kanisa hilo katika siku thelathini, ndipo anatolewa chini ya ulinzi wa Yesu. Tunamfungulia. Hiyo ni kweli kabisa. Ndipo angalia jambo litakalotukia. Acheni Mungu amwadibishe basi. Mmeondoa mikono yenu. Mmefanya jitihada zote mlizoweza. Ndipo mwacheni Mungu ashughulike naye kidogo, Yeye atamwachilia kwa Ibilisi. Ndipo atakuja. Kama haji, maisha yake ni mafupi tu.

205 Nanyi mnakumbuka katika Biblia ambapo kulikuwako na ndugu ambaye hangejiweka sawa na Mungu? Ni wangapi wanakumbuka kisa hicho? Yeye aliishi na mama yake wa kambo, nao hawakuweza kumrekebisha. Paulo alisema, "Mtoleeni Ibilisi, ili aadhibiwe. Mnapata kwamba, katika II Wakorintho, yeye alisahihishika.

206 Nina ndugu mmoja, rafiki mzuri, ninapenda kutaja jina lake hapa. Yeye ni ndugu mhubiri, na ndugu huyu mhubiri, jina lake ni Ndugu Rasmussen. Wengi wenu wahudumu mnaoketi hapa usiku wa leo, jina lake limo katika magazeti yenu. Ni lile la madhehebu yote huko Chicago. Basi angalia. Yeye alikuwa na mvulana mmoja, muhudumu, naye akatoka akaenda akamwoa msichana Mkatoliki, akaanza namna hiyo, naye alikuwa anaenda kufanya *hivi*, *vile,* na *vinginevyo*. Na—na baada ya yote, akaingia katika shida fulani. Ndipo babaye akamwendea, akasema, "Sasa angalia, mwanangu, je! utasuluhisha mambo na baba yako?" Yeye aliita kanisa lao kundi la watakatifu wanaojifingirisha, baba yake. Akasema, "Sasa angalia, je! utasuluhisha jambo hilo na kanisa hili?"

207 Yeye akasema, "Sasa, baba, wewe ni baba yangu, nami sitaki kugombana nawe."

208 Vema, akaenda akamleta shemasi mmoja kisha wakaenda nyumbani kwake. Kasema—kasema, "Wesley, ninataka kuzungumza nawe." Kasema, "Je! utanyosha jambo hili na

kanisa?" Naye akampa jibu fupi la maneno mawili namna hiyo. Kasema, "Kumbuka, Wesley, mimi ndiye mchungaji wa lile kanisa. Mimi ni baba yako, lakini nitafanya yale Mungu anayosema tufanye. Ninakupa siku thelathini kujiweka sawa na kanisa lile, la sivyo tutakutupa nje kutoka kwenye Uwepo wa Mungu. Wewe ni mwanangu hasa; Huyo ni Mwokozi wangu." Kasema, "Ninakupenda. Nawe unajua ninakupenda, Wesley, ningekufa sasa hivi kwa ajili yako, lakini huna budi kujiweka sawa na Neno la Mungu, unaona." Kasema, "Mimi ni mchungaji, mimi ni mchungaji wa lile kundi, na ikiwa wewe ni mtoto wangu ama ye yote yule uwaye, huna budi kujiweka sawa na Neno la Mungu. Usipofanya hivyo, basi mimi sistahili kuwa mchungaji Wake."

209 Jamani, huyo ni mchunguaji kwelikweli. Huyo ndiye mtu. Hauoni hivyo? Huyo ndiye mtu. Alimwambia mvulana wake hivyo, na kumuudhi, alisema. Lakini alisema nini? "Utamuudhi nani, mtu huyo ama Mwokozi wako?" Hivyo ndivyo alivyosema, "Basi tukaendelea."

210 Basi akasema, "Hangefanya jambo hilo. Nasi . . . Nililiambia kanisa, na nikasema, 'Mwanangu mwenyewe, Wesley, anakataa kunisikia mimi katika jambo hili. Anakataa kumsikia shemasi. Wewe ni shahidi wa jambo hili, Ndugu *Fulani*? 'Ndiyo, mimi ni shahidi.' 'Vema, saa mbili Jumapili ijayo, majuma manne tangu sasa, kama hajasahihisha jambo hilo pamoja na kanisa hili, tutamtolea Mwanangu Wesley Ibilisi, mwili wake upate kuharibiwa, damu hii, Damu ya—ya Yesu Kristo na kanisa hili havimkingi tena.'"

211 Na usiku huo ukafika, akasimama mimbarani, kasema, "Yeye ana dakika mbili zaidi." Wakati ukawadia, akasema, "Sasa, kama mwanangu, Wesley Rasmussen, ndipo akasema kwa kusanyiko hili na kwako Wewe, Mwenyezi Mungu, tumefanya yote tuwezayo kufanya, kulingana na Maneno Yako na maagizo Yako ya Mwa—ya Mwanao, Mwokozi wetu, aliyotuachia, sasa sisi . . . ninamtoa kijana wangu, na kanisa hili pamoja nami, kwa—kwa Ibilisi, mwili wake uharibiwe, kusudi nafsi yake iokolewe." Hayo tu ndiyo yaliyosemwa. Hakuna kilichotukia kwa juma moja ama mawili, labda mwezi mmoja ama miwili.

212 Usiku mmoja maskini Wesley akaugua. Na alipougua, akazidi kuugua. Akamwita daktari. Daktari akaja akampima. Alikuwa na homa ya kipimo cha mia moja na tano, hakujua sababu yake. Aliendelea tu kuwa mgonjwa zaidi. Daktari akasema, "Kijana, sijui ni jambo gani lililokupata." Hakujua la kufanya. Kasema, "Tutamwita daktari bingwa." Wakamwita daktari bingwa na huyo daktari bingwa akaja hapo. Wakampeleka hospitali, wakampima, kila kitu, akasema, "Siwezi tu kukwambia, mvulana huyu ni ninii—anaonekana tu ni mgonjwa sana." Mkewe akisimama pale, akilia na kila kitu namna hiyo. Na watoto wamesimama wamekizunguka

kitanda, na kila mtu namna hiyo. Akasema, "Yeye anakufa, ni hilo tu." Kasema, "Mapigo yake ya moyo na kupumua kunazidi kushuka."

213 Akasema, "Niitieni baba." Loo, ndiyo, hivyo ndivyo inavyopaswa kufanywa. Jambo ndilo hilo. "Niitieni baba." Ndipo baba yake akakimbia kwenda kule hospitalini upesi sana kumwona. Akasema, "Baba, siwezi sasa, lakini Mungu anayasikia maneno yangu, nitatengeneza mambo yote. Nitayatengeneza. Ndiyo, nitayatengeneza." Naam, bwana, ndugu, papo hapo kupumua kwake kukaanza kurudia kawaida.

214 Ndipo Jumapili iliyofuata, akasimama mbele ya kanisa, akasema, "Nimefanya dhambi mbele za Mungu mbele ya kanisa hili. Nilikataa kuyasikia maneno ya mchungaji. Ni—nilikataa kumsikiliza shemasi hapa." Kisha akasema, "Ninaomba kanisa hili linisamehe kwa ajili ya uovu nilioutenda namna hiyo." Kasema, "Mungu ameyaokoa maisha yangu." Ninawaambia, yeye alijiweka sawa. Ndiyo. Hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa, unaona. Unaona? Ninyi, kama tu mngalitenda hilo kwa njia ya Mungu! Mnaona?

215 Sasa, unaona, jinsi tunavyofanya jambo hilo, tuna mkutano wa halmashauri, nasi tunasema, "Vema, sasa, tunapaswa kumweka . . . " Sisemi Maskanini, lakini ninasema sisi Waprotestanti, tuna mkutano wa halmashauri, "Je! mnafikirije juu ya Jones? Mnafikiri tunapaswa kumfanyia nini? Nafikiri angekuwa mfuasi mzuri zaidi wa Kimethodisti kuliko angalikuwa kwetu." Haya basi. Hilo, hilo ni kosa. Hiyo ndiyo sababu si lazima tufuate mapokeo yao na askofu fulani tunayepaswa kumwita, ama nanii fulani, vyo vyote unavyowaita, mkuu wa wilaya katika Kanisa hili la Kipentekoste, Mzee wa kanisa wa Wilaya, mnamwitaje aje aone mwenendo wa mtu huyu.

216 Biblia inatwambia la kufanya. Hiyo ndiyo sababu sisi hatujipumbazi na madhehebu yao. Hatuhusiki na kitu hicho. Amina. Hamnikasirikii sana, sivyo? Msifanye hivyo. Labda nitapata maswali mazuri sana kesho usiku, lakini tutaninii . . . Hiyo ni kweli, unaona.

217 Kumbukeni, hapana, ninasema jambo hili sasa. Ninyi watu mlio hapa kutoka katika madhehebu mbalimbali ya makanisa, madhehebu yenu . . . Ndugu, sisemi ya kwamba ninyi si Wakristo. Sisemi ya kwamba madhehebu yenu hayana maelfu ya Wakristo wazuri sana kule. Ninajaribu kusema ni kwa sababu gani sisi si madhehebu. Maana mimi singestahimili jambo hilo. La, bwana, hakika nisingestahimili, wala kujaribu kuwaambia la kufanya. Kama Mungu aliniita kuhubiri Injili, basi nitaihubiri jinsi Mungu anavyoniambia niihubiri. Hivyo ndivyo tu vile—vile ilivyoandikwa hapa katika Biblia. Kama haliambatani na Hii, basi ni kwamba . . . Mungu atanihukumu kwa hilo. Lakini

kama ni—kama ni—kama nikiona mbwa mwitu anakuja, ama adui akija, nami ninashidwa kuwaonya, basi Mungu atayataka kwangu. Lakini kama nikiwaonya, basi ni juu yenu basi. Unaona?

218 Kumbukeni, hapo katika siku za mwisho, ya kwamba zitakuja nyakati za hatari, watu watakuwa wenye kujipenda, wenye kujigamba, wenye kujivuna, wenye kukufuru. Unaona, wenye kukufuru, "Loo, wao ni kundi la majuha. Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho." Yeye ni maskini nabii wa uongo wa miaka na miaka. "Sasa, tunajua ya kwamba wanawake wetu wana akili nyingi tu kama wanaume wetu." Sipingi jambo hilo hata kidogo, lakini Biblia ya Mungu ilisema mwondoe mimbarani. Hilo—hilo ni zuri vya kutosha kwangu, unaona, hiyo ni kweli. Vema. Unaona? Na mseme, "Vema, sasa, madhehebu yetu, tuna watu wengi tu wazuri kama mlio nao kule Maskanini." Sisemi jambo hilo hata kidogo, lakini Biblia inahukumu madhehebu. Hiyo ni kweli. Na kwa hiyo, sasa, sisemi ya kwamba hamna wafuasi wazuri kanisani mwenu. Hilo ni jambo zuri sana. Wao ni watu wazuri. Baadhi ya watu walio wazuri sana, ninakutana nao katika hayo yote, Wakatoliki na wengine wote. Yote hayo, mimi ninakutana na wafuasi wazuri.

219 Sasa, jinsi tutakavyolileta jambo hili sasa, rafiki, Bwana akipenda, katika masomo haya mengine kadha yafuatayo, labda nitawajulisha kesho asubuhi kama itatubidi kuendelea kesho alasiri ama hatutaendelea, unaona, kuyatoa. Sababu ya sisi kujaribu kufanya jambo hili, ninataka kulileta kulifikisha mahali fulani sasa. Sasa, kama ukitaka kuja na mtu fulani, unakaribishwa vizuri sana kufanya jambo hilo. Lakini kumbuka sasa, usi—usiondoke tu ukijaribu kupata makosa, ama kuja hapa. Ninazungumza tu na kusanyiko la—langu, unaona. Mimi sifundishi jambo hili nje ya kusanyiko langu hapa, maana hiyo ni kazi ya huyo mtu mwingine, kwamba yeye ndiye mchungaji wa kundi hilo. Na mimi ni ninii tu. . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]

220 Moja kwa moja akirudi Mwanzo, yeye atalipata moja kwa moja na kuona lilipo. Sasa tutarudi hadi Mwanzo tuone ni kwa nini mtoto haramu hangeingia katika kusanyiko la Bwana kwa vizazi kumi na vinne. Jinsi inavyoenda. . .Hiyo ingekuwa ni miaka mia nne kwa dhambi hiyo kwisha. Jinsi tutakavyoenda kuona jinsi vile ma—maovu ya wazazi yanapatilizwa watoto na watoto, jinsi jambo hilo lilivyoanza katika Mwanzo, na kadhalika.

221 Ndipo utaona jinsi ambavyo, ukirudi kule nyuma kabisa, ambako Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kabla atomi moja haijavunjika bado kule nyuma kabla hakujatokea nuru ya kimondo, Mungu alijua kila kiumbe na kila kitu ambacho kingekuweko duniani. Kuna mtu ye yote hapa, usingeweza kueleza neno hilo, na kulivunja-vunja, na kusema

maana ya neno “bila mwisho”? Ni kama tu kuelekeza kamera yako huko—huko kusiko mwisho, ninii tu—ni kutoka tu hapo na kuendelea. Hivyo tu, unaona, pasipo mwisho. Nasi hatuwezi, katika akili zetu zenye kikomo, hatungefahamu yale akili isiyo na kikomo ingeweza kuwazia. Unaona, hatuwezi kufanya jambo hilo. Wewe, huwezi kufanya jambo hilo. Unaona? Lakini kama utaangalia tu, ushikilie katika Roho, unaweza kuisikia huko mbali sana, na—na urudi hapa kwenye Maandiko na utaona sasa, unaona, huko mbali kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

222 Sasa, Biblia ilisema ya kwamba Yesu Kristo alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu. Sasa sikilizeni kwa makini sana, ili kwamba kama baadhi yenu hamtakuwako kesho kusikia mwisho wake. Biblia ilisema ya kwamba Yesu Kristo alikuwa Mwana-Kondoo wa Mungu aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo ni kweli? Yeye alichinjwa lini? Tangu kuwekwa misingi. Huo ni ulimwengu, kama umeumbwa kwa kundi la atomi zilizovunjwa-vunjwa, zilizotolewa kwenye jua huko ng’ambo, kabla halijakuwa hivyo. Halafu kabla hapajakuwapo na atomi hata moja iliyovunjika kutoka kwenye jua, kama hiki kilikuwa ni kimondo kutoka kwenye jua, ambacho kingekuwa bilioni mia moja trilioni trilioni trilioni za miaka huko nyuma kabla hapajakuwepo na hata kimondo kimoja cha nuru, Kristo alikuwa amechinjwa. Wakati akili kuu ya Mungu inapotulia juu ya jambo moja, huwa ni jambo lililokamilika. Hapo Mungu aliposema, “Na iwe,” imetimia tayari. Kama ilichukua miaka bilioni mia moja kutimia, tayari imetimia mara Yeye aliposema jambo hilo. Na hapo Mwana-Kondoo alipochinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Biblia ile ile, Roho yule yule aliiandika na kusema, “majina yetu yaliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.”

223 Kwa hiyo yule mtu aliyeandika ule wimbo, “*Kuna Jina Jipya Limeandikwa Utukufuni,*” alikuwa anawazia mema, lakini alikuwa si wa kimaandiko. Unaona? Hilo jina liliandikwa Utukufuni wakati ulimwengu. . .wakati kabla ulimwengu haujaanza bado. Wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa, majina yetu yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

224 Hebu—hebu niwape Andiko moja dogo. Mtangoja kwa dakika moja? Hili linakuja mwanzoni mwangu sasa. Nafikiri ninaweza kulifungua moja kwa moja. Sina hakika. Na sasa ninasikitika kuwaweka kwa muda mrefu namna hii, lakini niliwaambia itakuwa usiku wa manane, haujatimia bado. Lakini ni—ninapenda tu ku—kupata jambo hili, Andiko moja tu kwake. Fungueni pamoja na mimi sasa katika Kitabu cha Warumi, nami ninataka mu—msome jambo hili pamoja nami sasa. Sasa, hebu tuone, Warumi, kama ninaweza kulipata, karibu tu papa hapa. Sasa, hebu tufungue Warumi 8, na—na tuanzie kifungu

cha 28 cha mlango wa 8 wa Warumi, nami ninataka muisome tu kwa maombi pamoja nami sasa. Sikilizeni hapa yale aliyosema Mungu sasa.

> *Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi Lake.*
>
> *Maana wale aliowajua . . .*

225 Hiyo inakupa . . . mnaweza kusoma na mimi? "Maana yeye . . ."

> *Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili* vema, *wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.*
>
> *Na wale aliowachagua tangu asili, hao akawaita; na wale aliowaita, hao akawahesabia haki; na wale aliowahesabia haki, hao akawatukuza.*

226 Tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Mungu alipoangalia chini. Sasa, Mungu haendeshi ofisi Yake, aseme, "Vema, sasa, nitaninii . . . Loo, tutafanya nini sasa?" Unaona? Hakuna kitu . . .

227 Kumbukeni, uovu, dhambi ni haki iliyopotoshwa. Ibilisi hawezi kuumba. Je! kila—kila mtu anaelewa hilo? Hilo ndilo fundisho la kanisa hili. Ibilisi hawezi kuumba. Anaweza kupotosha kile Mungu alichoumba. Sasa, upotovu ni nini? Hapa, nyote mnaonekana kama watu wazima, karibu nyote. Sikilizeni jambo hili. Sisi ni watu waliofunga ndoa. Na wewe mwanamume uliyeoa na ninyi wanawake mlioolewa mnaweza kuishi pamoja kama mume na mke, na hao wanawake ni kama tu kwamba hawajawahi . . . wao ni bikira mradi tu ulidumu na mume wako. Hiyo ni kweli. Sasa, hilo ni halali na ni jambo la haki, na ni sawa kabisa, iliamriwa na Mungu kufanya jambo hilo. Mwanamke mwingine anaweza kufanya tendo lile lile la mkeo. Mmoja wa hao, wewe ni mwenye haki mbele za Mungu; na tendo lile lile kwa mwanamke mwingine, umehukumiwa mbele za Mungu, mauti. Ni kitu gani? Haki iliyopotoshwa, unaona, haki iliyopotoshwa. Sasa, Ibilisi hawezi kuumba, lakini anaweza hupotosha yale ambayo Mungu ameumba tayari.

228 Uongo ni kitu gani? Ni ukweli uliopotoshwa. Mtu fulani alisema, loo, "Ilikuwa Jumamosi usiku, saa tatu, naam, Bill Branham alikuwa Jeffersonville." Ni kweli. "Kule chini kwenye klabu cha Anthoni, amelewa." Uongo. Ilikuwa ni kitu gani? Nilikuwa Jeffersonville, hiyo ni kweli. Ilikuwa kweli iliyopotoshwa ikawa uongo. Unaona ninalomaanisha? Unaona, uongo hupotosha ukweli. Ni kitu fulani kilichosema mahali nilipokuwa. Sasa, kama ingesema, "Huko kanisani, akihubiri." Ni kweli. Hiyo ni haki, yeye alisema kweli. "Kwenye baa,

akinywa pombe." Ni uongo. Imepotoshwa, unaona, ukweli uliopotoshwa. Unaona ninalomaanisha? Siyo haki yote ni haki iliyopotoshwa.

229 Mauti, ni kitu gani? Uzima uliopotoshwa. Ugonjwa? Afya iliyopotoshwa. Unapaswa kuwa mtu mzuri mwenye nguvu. Vema, kama wewe una afya mbaya, ni kitu gani? Afya yako imepotoshwa. Unaona, ni hayo tu. Ni kitu gani? Mlikuwa ni vijana wanawake wenye sura nzuri, na mwanamume mwenye nguvu na sura nzuri, sasa una makunyanzi na unazeeka, ni kitu gani? Uzima uliopotoshwa, unaona, unarudi moja kwa moja tena. Unaona? Na hauna budi kurudi tena, Jina la Bwana libarikiwe, Mungu ameahidi kuurudisha tena. Na hakika tu kama . . . kama uko, tunajua uko hapa; kwa hiyo hakika tu kama ilivyo, Mungu ataurudisha tena. Aliahidi jambo hilo na kuapa ya kwamba atalitimiza. Hilo ndilo linalotupa ninii . . .

230 Sasa, tunapaswa kuwa watu wa namna gani? Sasa angalieni jinsi mambo haya yanavyotukia. Sasa, wale aliowajua tangu zamani, hao aliwaita; wale aliowaita, hao aliwahesabia haki. Lini? Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kabla ulimwengu haujaanza bado. Sasa, kama tungaliweza kuchukua Andiko hili na kweli tulihakikishe, tungechukua masaa mengi juu yake, lakini ha—hatutaki kufanya jambo hilo. Lakini maovu yote haya hapa, ni haki iliyopotoshwa ikawa maovu. Hivyo ndivyo Ibilisi anavyofanya. Sasa, wakati unapofikia umri wa kujua mema na mabaya, nawe unajua yasiyo mema na yaliyo kweli, unapaswa kuacha mabaya yako. Kwa sababu, wewe ulizaliwa katika dhambi, ukaumbika katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo. Ndipo una ninii—kwa kweli unazaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili, ndipo huna budi kuzaliwa mara ya pili ili upate kupokea uzao upya, upate kuingia Mbinguni. Kwa sababu uzao wa namna hii ulio nao hapa . . .

231 Unaona ambapo Shahidi wa Yehova angekuwa amekosea sana hapo kwa mbali mno, kuwazia ya kwamba kuzaliwa upya ni ule ufufuo wa mwili, unaona. Haiwezekani. Unaona? Haina budi kuwa ni jambo fulani . . .

232 Wewe, uko katika uwanda wa wakati, na jambo pekee lililo la Milele ni kitu ambacho hakina mwanzo wala mwisho. Cho chote kilicho cha Milele hakijawahi kuwa na mwanzo, wala hakitakuwa na mwisho. Unaona? Kwa hiyo kama wewe ni sehemu ya Mungu, Roho aliye ndani yako hakuwa na mwanzo kamwe wala hatakuwa na mwisho, nawe ni wa Milele pamoja na Roho aliye ndani yako. Unaona? kama vile u—u—upendo wa agape, kisha unashuka unakuwa upendo wa fileo, kisha unakuwa upendo wa tamaa mbaya, unaendelea tu kushuka na kushuka, ukiendelea kupotoshwa mpaka unakuwa tu lundo la machafuko kabisa. Mbona, njia pekee, Yesu alishukia kwenye ngazi hiyo hiyo akaja chini hapa kuchukua na kurudisha

tena kwenye kiwango cha juu kuliko vyote; kutoka hali ya chini kabisa, kutoka mautini kuingia Uzimani, kutoka maradhi kuingia kwenye afya njema, kutoka kwenye maovu kuingia kwenye haki. Mnaona? Yeye alitoka kutoka aliye wa juu sana akawa aliye wa chini sana, apate kumwinua aliye chini sana awe wa juu sana. Yeye alifanyika mimi ili kwamba kwa neema Yake nipate kufanyika Yeye, mrithi wa Kiti cha Enzi Utukufuni. Mnaona ninalomaanisha, mambo hayo? Sasa angalia, huko nyuma kabisa kabla ulimwengu huu haujaanza kwenye hizo atomi kule nyuma, wakati Mungu alipoona jambo lililokuwa linaenda kutukia, pale pale Yeye alikuona, Yeye aliniona mimi, aliona kila kiroboto, kila inzi, kila chura, kila mbu, kila kitu kitakachowahi kuwa duniani, Yeye alikiona wakati uo huo. Hakika, alikiona.

233 Sasa, Yeye kamwe hakusema, "Nitamtuma Mwanangu kule chini na nimwache afe, na labda mtu fulani atamwonea huruma. Na litakuwa ni jambo la kuhuzunisha sana, wao . . . labda huenda ikawa mtu fulani ataokolewa."

234 Yeye alitangulia kujua yule atakayeokolewa! Ndiyo, bwana. Alisema, "Esau namchukia, na Yakobo nampenda," kabla mmoja wao hajapata nafasi ya wao kuthibitisha kile walichokuwa, kwa sababu Yeye alijua hao walikuwa ni nani. Alijua. Anajua kila kitu. Alijua wewe ungefanya nini, kabla hujazaliwa, na wakati ulimwengu ulipoanza.

235 Sasa angalia, kama mjuavyo, Mimi—mimi—mimi ni shabiki wa bunduki. Ni—ninapenda bunduki. Na mwanamke mmoja huko Texas, ninaamini ni Texas, alininunulia moja ya Swift, muundo wa Swift .220. Daima nilitamani kuwa na moja, nilitaka kuichuguza. Ni bunduki ndogo yenye nguvu sana ya kuwindia. Ni ya risasi ishirini na mbili, risasi ya kipimo cha arobaini na nane, nawe unaweza kuitumia hiyo . . . Sasa, kiwanda kinasema, "Usifanye hivyo, ni hatari sana." Lakini unaweza kuifanya risasi hiyo iwe ya futi elfu tano kwa sekunde, na hata hivyo uishikilie imara. Futi elfu tano kwa sekunde, hiyo ni maili moja kwa sekunde. Kwa maneno mengine, koho anayeketi umbali wa yadi mia mbili, unaweza kumwua huyo koho na kuona manyoya yake yakiruka kabla bunduki hiyo haijakutikisa. Unaona? Hiyo, lakini chukua upande huo mpanapana wa kijiti cha kuchokoa meno na ukiingize kwenye baruti yako, na uongeze kiasi kama *hicho* mle ndani, ya kutosha tu ambayo ungeweza kuichota kwa kijiti cha kuchokoa meno; nawe unaweza kumpiga risasi nguruwe anayeketi kwenye mwisho wa jengo hili hapa, naye aketi tu akikwangalia. Ni kitu gani? Ile risasi inavunjika—vunjika, inaenda kasi sana. Nawe unaweza kuweka shiti kati ya hapa na pale, wala kamwe hutaona hata baki moja dogo likianguka kwenye shiti. Inageuka tu hali ya awali. Si ikawa—ikawa majivu, majivu ya volkeno; lakini inaenda mbali na hapo. Inarudi kwenye asidi asilia zinazofanyiza shaba na bildi iliyo

mle ndani. Inarudi ikawa kama ilivyokuwa miaka billioni mia moja iliyopita. Sasa, hii hapa risasi ndogo, risasi ya kipimo cha arobaini na nane, ninaishika mkononi mwangu, na katika sekunde moja ijayo inarudi jinsi ilivyokuwa miaka milioni mia moja iliyopita. Na kama ulimwengu ungesimama miaka mingine elfu mia moja, ingerudi kuwa risasi tena, ingerudishwa moja kwa moja, sababu imefanyika shaba tena.

236 Sasa angalieni yale Mungu aliyofanya, na ndipo mtampenda, kisha mtaenda nyumbani, na asubuhi yake mlale zaidi kidogo na—nanyi—nanyi mtampenda Yeye kuliko mlivyowahi. Sasa, Mungu ni Kondrakta. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Yeye ni Mjenzi. Sawa, sikilizeni kwa makini sana. Sasa, Mungu kule nyuma, wao wanasema . . . Sasa tutachukua wazo la wataalamu wa utaratibu wa miaka. Mungu, miaka bilioni mia moja iliyopita, alipokuwa anataka kuumba ulimwengu, vema, Yeye alianza tu. Sasa Yeye alikuwa . . . Yeye alipata wazo fulani niani mwake.

237 Sasa mtasema, "Kama Yeye ni mkuu hivyo, Ndugu Branham, yeye alimruhusu Ibilisi namna gani kutenda dhambi?" Vema, Yeye alijua kabla Ibilisi hajaumbwa ya kwamba Yeye angekuwa Ibilisi. Utukufu! Sasa ninajisikia ni wa rohoni. Loo, jamani! Alijua kabla Ibilisi hajaumbwa ya kwamba angekuwa Ibilisi. Sasa utauliza, "Na jambo hilo je?" Unasema, "Kwa nini akamwacha awe Ibilisi?" Kusudi aweze kuthibitishwa kuwa Mungu. Hiyo ndiyo sababu alifanya jambo hilo. Kwa nini kulipata kuwa na uovu?

238 Kwa nini, ni nani aliyetangulia, Mwokozi ama mwenye dhambi? Ni nani aliyetangulia? Mwokozi. Ni nani aliyetangulia, Mponyaji ama mgonjwa? Kwa nini mwenye dhambi akaruhusiwa kuwapo? Kwa sababu sifa Zake ni Mwokozi. Kama hakungekuwako na mwenye dhambi, Yeye hangaliweza kujulikana kuwa Mwokozi. Haleluya! Yeye anaweza kufanya mambo yote yaishie kwenye utukufu Wake. "Je! mfinyanzi anaweza kukiambia . . ." Ama, "Je! chungu kinaweza kumwambia mfinyanzi, 'Ulinifanya hivi'?" Ni nani aliye kwenye gurudumu? Ni nani aliye na udongo? Uko kwenye mikono ya nani? Paulo alisema, "Ewe mtu usiye na akili, Yeye hakusema alimwinua Farao kwa kusudi lili hili?" Bila shaka, Yeye alijua jambo hilo kabla hapajakuwepo na ulimwengu, Yeye alijua ni nani atakayekuwa nini. Naye akaruhusu dhambi itokee kusudi Yeye apate kuwa Mwokozi. Aliruhusu magonjwa yawepo kusudi apate kuwa Mponyaji. Aliruhusu kuwe na chuki kusudi Yeye apate kuwa upendo. Hakika, aliruhusu. Yeye ni Mungu, na hizo ndizo sifa Zake, naye hana budi kuwa na kitu fulani cha kuonyesha sifa Zake.

239 Ungewezaje kamwe kujua ya kwamba kulikuweko na usiku, ungewezaje kujua ya kwamba ulikuweko wo wote; kama yote ilikuwa ni mchana, ungewezaje kujua kulikuwako na usiku.

Usiku upo kusudi uthibitishe mchana. Hakika, upo. Amina. Unaona jambo alilofanya?

240 Lakini Yeye alipokuwa huko nyuma kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kabla Yeye hajalichukua jua hili la kale na kulisogeza karibu na nyota hii ya kale tunamoishi sasa, dunia hii, na kuifinyanga hapa kwa jua na kuiweka karibu na jua. Tuseme, hili *hapa* jua. Yeye alilifinyanga upande *huu* na kuliacha lining'inie pale kwa miaka bilioni mia moja. Alikuwa akitengeneza nini? Gesi. Akasogea upande *huu*, akaumba kitu kingine. Alikuwa akiumba nini pale? Magadi. Akasogea huku *hivi*, na alikuwa akifanya nini hapa? Akitengeneza kasiamu. Alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiniumba mimi na wewe. Alikuwa akifanya nini? Kama vile kondrakta akiweka mbili-kwa-nne zake zote na mbili-kwa-nane zake, shiti zake, mbao zake, yeye alijua tu ni nyumba ngapi atakazojenga. Nasi tumeumbwa kwa elementi kumi na sita za dunia, Naye alikuwa akituumba sisi sote, na kutuweka nje kule kabla ulimwengu haujaku-. . . Na huenda ulikuwa mraba mrefu upande mmoja wakati huo, sijui ulikuwa nini. Kwa nini alikuwa akiumba dhahabu, na shaba nyekundu, na shaba nyeupe, na maji, na vitu hivyo vyote? Yeye ni Kondrakta. Yeye ni ninii . . . Mjenzi, alikuwa akiweka kila kitu kule nje, alikuwa tayari amekata kila kitu na kukiunda. Wakati alipomaliza vyote, vilikuwa tu ni bubujiko kubwa sana la volkeno. Yeye aliachilia hizo volkeno za kale ziatamie kule juu kwa miaka milioni mia moja, apate kufanyiza kasiamu. Ni kitu gani? Ni sehemu yako.

241 Na halafu kabla hapajakuwapo na chembe moja ya uhai katika dunia hii, miili yetu ilikuwa imekaa hapa. Haleluya. Kabla tone moja la unyevu halijaja duniani, tulikuwa tumekaa hapa. Wakati Adamu alipoenda huku na huko katika Bustani ya Edeni, nilikuwa hapa. Amina. Naam, bwana. Loo, utukufu! Wakati Makerubi, nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu wakapiga makele kwa furaha, nilikuwa nimekaa hapa nikingojea tu ile pumzi ya uhai ije. Nilikuwa hapa. Yeye aliniumba hapa, na mwili wangu ulikuwa umelala hapa. Ndiyo, bwana. Haikuwa ulikotoka wewe. Jamani, ulifikaje hapa? Mungu aliuweka hapa. Mungu aliuumba. Tumeumbwa kwa elementi kumi na sita, petroli, shura na mialimwengu, na kadhalika. Unaona, tulikuwa tumelala hapa.

242 Ndipo nini kilitukia? Basi Mungu akamwambia Roho Mtakatifu, tutalichukua tu katika mfano, "Sasa Wewe ondoka uende, na uende ukafanye mapenzi na dunia ile, kwa kuwa Mimi ni Upendo nawe umetokana Nami, kwa hiyo sasa ondoka uende ukafanye mapenzi na dunia ile." Ndipo Roho Mtakatifu mkuu, tunafikiri, akatoka akaja kule, kwa mfano tu wa picha sasa. Haikuwa namna hiyo. Hasa, Roho Mtakatifu na Mungu ni yeye yule, kusudi lile lile, kusudi moja, Mtu mmoja. Samahani. Na tuseme tu Yeye alitupa mbawa Zake kuifunika dunia,

akaanza kuatamia. Alikuwa akiatamia nini? Kama vile kuku kwa vifaranga wake, akinong'oneza, akifanya mapenzi, "ku-ku, ku-ku, ku-ku." Loo.

243 "Ee uhai, njoo!" Akalia kwa sauti kuu. Akaangalia kila upande. "Ninataka uzuri juu ya dunia hii. Njoo, ewe nuru!" Roho Mtakatifu akitenda kazi. Na alipofanya hivyo, ninaona ikija, kule ikitelemka kwa kishindo kule kilimani, ile kule kalisiamu ikitiririka, na inachanganyikana na shura. Inafanyiza kitu gani? "Uhai, njoo!" Ua dogo la Pasaka linatokeza kichwa chake chini ya mwamba. "Njoo hapa, Baba, angalia hilo."

244 "Hilo linaonekana zuri, endelea tu kuatamia." Akayaatamia maua, akaleta mimea yote, akaleta wanyama, na ndege wakaruka kutoka mavumbini. Baada ya kitambo kidogo, akatokea mwanamume na mwanamke; akatokea mwanamume, naye mwanamume huyo alikuwa mwanamume na mwanamke. Si mwenye sehemu za kiume na za kike sasa; ni katika—katika yeye tu.

245 Kulikuweko na roho ya kike. Unapomchukua mwanamume ambaye ni dondoadume sana, huenda akawa sawa, kimaumbile yuko sawa, lakini ana kasoro. Na unapomchukua mwanamke, anayetaka kukata nywele zake na kuvaa ovaroli, na kutoka huko nje, "Na Mungu na abarikiwe, nakwambia," kuna kasoro. Mwanamke ana roho ya kike, na mwanamume ana ya kiume. Tunajua jambo hilo, nanyi mnajua jambo hilo. Je! mwanamke anaonekana sawa anayejaribu kuwa ninii, kutenda kama mwanamume?

246 Mbona, niliketi wakati mmoja, nilikuwa mlinzi wa wanyama pori hapa, nami niliketi kwenye basi na nikaenda kule nami nilikuwa nikimpigapiga huyo mwanamke kwenye mguu, kwa mkono wangu, nikizungumza naye, nami sikujua alikuwa ni mwanamke. Alikuwa na moja ya kofia hizi za hawa wachomelea chuma na miwani mikubwa ya jua namna *hiyo*, nami nilikuwa nimeketi kule nyuma kabisa, naye alikuwa akielezea jambo fulani hivi kuhusu jambo fulani alilofanya. Akasema, "Unajua," na akasema, "jana usiku," anaonekana jeuri tu awezavyo kuwa, akivuta sigara. Akasema, "Jana usiku, nakwambia, yule jamaa aliteleza juu ya kitu hicho," na akasema, "jamani, alikuja anaporomoka chini kupitia pale." Kasema, "sijapata kucheka namna hiyo maishani mwangu."

247 Nami nilikuwa ninacheka, unajua, namna hiyo. [Ndugu Branham anafanya kelele za kupiga makofi—Mh.] Nikasema, "Wacha wee, hilo linachekesha sana, sivyo?" Ameketi pale akizungumza namna hiyo. Na kama hangalitoa kitu hicho na kutikisa kichwa chake, naye alikuwa na nywele nene kule kwamba alikuwa ni mwanamke. Sijajisikia duni hivyo maishani mwangu. Ni—nikasema, "Je! wewe ni mwanamke?"

Akasema, "Ala, bila shaka!"

248 Nikasema, "Samahani." Sijaona kitu cha namna hiyo. Sasa, hiyo ilikuwa ni kweli.

249 Niliona ishara hivi majuzi ambayo ilitaka kunifurahisha sana. Ilikuwa na ilani kubwa pale juu, ikasema, "Akina mama wako tayari kuvaa nguo." Nikawazia, "Mungu asifiwe kwa jambo hilo." Unaona? Lakini, nikaja kuona kwamba, zilikuwa ni namna fulani tu ya nguo walizokuwa wameshona tayari, unajua. Ni—nilidhani kweli watavaa nguo."Kweli nilidhania hivyo. Ilisema, "Akina mama wako tayari kuvaa nguo." Nikasema, "Bwana asifiwe kwa ajili yao. Hilo ni jambo zuri. Hiyo ni kweli, hakika ninamshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo." Lakini, unaona, ilikuwa tu ni namna fulani ya nguo walizokuwa wameshona tayari, kitu fulani. Hilo lingekuwa ni jambo la kuchekesha, sivyo, katika nchi hii? Vema.

250 Ndipo wakati Adamu alipotokea. Halafu basi Adamu akaonekana mpweke, kwa hiyo Yeye akatoa ubavu kutoka ubavuni mwake na kumfanya Hawa, kama zaotuka wake. Kisha akafanya, akatoa roho ya kike kutoka kwa Adamu na akaiweka kwa mwanamke, roho ya upendo, ya kike, pole, nyenyekevu. Na akaacha roho ya kiume kwa Adamu. Sasa, kama kuna jambo lo lote tofauti, kuna upotovu mahali fulani. Sasa, ndipo hao wawili walikuwa mmoja.

251 Na kwa hiyo hebu tuchukue tu mchezo wa kuigiza basi kabla hatujafunga. Huyu hapa anakuja, huyu hapa Adamu anamshika Hawa mkono nao wanatoka. Ninapenda tu hadithi hii. Nao wanatoka, mwajua, naye Hawa akasema, "Loo, mpenzi, unataka kusema umeshafanya hivyo?"

"Ndiyo, nilimpa huyo jina."

Vema, unamwitaje *yule*?"

"Huyo anaitwa farasi."

"A-ha. Na yule ni *nani?*"

"Huyo ni ng'ombe."

"Ulimpa huyo jina?"

"Naam, A-ha."

252 "Unamwitaje *yule, yule,* wale wawili waliokaa pale wameweka vichwa vyao pamoja?"

"Hao wanaitwa ndege-vipenzi."

253 "Loo, sawa. Sawa." Nao wanaendelea namna hiyo pamoja. "Na huyu *hapa* ni nani?"

"Ninamwita huyo *vile*, na *huyu* hapa."

254 Na, "Loo, sawa. A-ha, hilo ni zuri." Ndipo simba ananguruma.

"Unamwitaje *huyo*?"

"Huyo ni simba."

"Huyu ni *nani*?"

"Simba marara."

255 Na wote namna hiyo . . . "Loo, sawa." Ni kama tu watoto wa paka, wajua, na wanalialia.

256 Kwa hiyo baada ya muda mfupi akaangalia kule, akasema, "Mpenzi, angalia kule, jua linashuka, wakati umefika wa kwenda kanisani." Unajua, kuna jambo fulani kuhusu wakati jua linapotua, unataka kuabudu. Kama huendi kanisani usiku huo, unataka kuingia chumbani kusoma Biblia. Ni wangapi wanaotaka kufanya hivyo? unakaa peke yako? Unaona? Mwanadamu anapenda sana kufanya hivyo. Unapaswa kufanya hivyo. "Wakati wa kwenda kanisani umewadia."

257 Sasa, hawakusema kamwe, "Sasa, ngoja kidogo, sasa, sasa Jones ni wa Assemblies, nasi ni wa ninii.." La, haikuwa hivyo wakati huo, kwa hiyo wakapanda tu wakaenda. Hawakuwa na kanisa, kiti kizuri cha kukalia namna hiyo. Walipanda tu wakaenda chini ya kanisa kuu la msitu, na kupiga magoti.

258 Na ile Duara ya Mwanga ilikuwa ikining'inia huko vichakani, unaona. Naweza kusikia Sauti ikizungumza kule na kusema, "Je, watoto wangu wamejifurahisha juu ya nchi, siku ambayo Bwana Mungu wenu amewapa?"

259 "Naam, Bwana, tumejifurahisha leo." "Sivyo, mpenzi?"

260 "Ndiyo, ndiyo, mpendwa, tumejifurahisha." "Bwana, hakika tunakupenda Wewe. Sasa nataka kulala." Unaona? Naye analaza mkono wake mkubwa chini, na Hawa analala chini kwenye mkono wa Adamu, na Adamu anamlaza simba marara chini na simba chini, na kila kitu kinalala, kwa amani.

261 Kwa hiyo Mungu anashuka na kuwashusha, loo, kundi la Malaika, Gabrieli, viumbe Vyake vya Mbinguni. Kwa hiyo wanashuka na kunyemelea pole pole sana katika chumba cha kulala, unaona, wanaangalia huku na huko. Gabrieli akasema, "Njoo hapa, Baba. Njoo hapa, angalia hapa. Huyu hapa. Hapa, hawa hapa watoto Wako wamelala hapa."

262 Ni wangapi hapa waliowahi kwenda kitandani, baadhi yenu akina mama, wewe pamoja na baba, na kumwangalia mvulana huyo mdogo na msichana huyo mdogo, na mnakumbushana tu, "Yeye si—si anafanana na wewe, hivi na vile?" Mlipata kufanya hivyo? Mbona, mara nyingi mimi ninaenda na kumwambia Meda, kusema kuhusu Joseph. Yeye angesema, "Bill, yeye ana paji la uso lililotokeza kama lako."

263 "Ndiyo. Lakini, Meda, ana macho makubwa kama yako." Kwa nini? Yeye ni sehemu ya zao letu, yeye ni zao la—la muungano wetu.

264 Sasa, naye Baba akasema, naweza kusema hivi juu ya jambo hili, kasema, "Unajua . . ." Na Gabrieli akasema, "Unajua, yeye anafanana na Wewe kabisa." Hiyo ndiyo sura ya Mungu,

jiangalie. Hiyo ndiyo sura ya Mungu, anafanana na wewe. Wewe ni uzao Wake. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Unaona?

265 Sasa angalia. Kiumbe cha chini kabisa tulicho nacho ni kipi? Ni chura. Kiumbe cha hali ya juu sana ni kipi? Binadamu. Bila shaka. Na cha hali ya juu sana ni kipi? Viliendelea tu kuja kutoka kwa walio wa chini sana na kwenda juu, kutoka chura kufikia kwa *huyu* na kwa *yule*, hadi kwa ndege, na kwa . . . loo, kadhalika, hali za juu tu za viumbe, mpaka inafikia tu kilicho juu sana kingaliweza kufikia, ndipo kikafanywa kwa mfano wa Mungu. Haya basi. Naye mwanamke hakufanywa katika mfano wa Mungu, lakini katika mfano wa mwanamume. Unaona? Sasa, sasa, haya basi. Naye Mungu anamwangalia, kasema, "Naam, wao wanaonekana—wanapendeza sana."

266 Hiyo ilikuwa nini, ndugu? Haikuwa kamwe wafe. Hiyo ilikuwa konzi tu moja ya kasiamu, shura ya kwanza, na kila kitu kilianzia namna hiyo. Hilo si ni zuri sana? Lakini dhambi ilikuja ikaharibu hiyo picha. Sasa, ni Mungu . . . Mungu aliiruhusu kufanya nini? Kwa nini akairuhusu kuwa kama tulivyokuwa tukinena habari zake muda kidogo uliopita? Yeye aliiruhusu kusudi aweze kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa Mwokozi. Alifanya hivyo. Aliruhusu magonjwa yaje kusudi apate kuthibitisha ya kwamba alikuwa Mponyaji. Aliruhusu mauti ije apate kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa uhai. Mnaona? Aliruhusu mambo hayo yote mabaya yatendeke apate kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa mwema, jinsi alivyokuwa. Tutaninii . . .

267 Nena kuhusu kuimba hadithi ya ukombozi! Mbona, ndugu, Yesu atakapokuja, hili—kanisa hili litasimama huko ng'ambo kwenye kingo za dunia hii na kuimba hadithi za ukombozi, wakati Malaika watakapoinamisha kichwa chao, bila kujua yale tunayozungumzia. Vema, wao hawajawahi kupotea kamwe. Hawajui yale tuliyopitia. Tunajua maana ya kupotea na kupatikana. Loo, je! hatuwezi kupiga kelele kwa sauti za sifa Zake? Yeye si Mwokozi kwao. Wao hawakuhitaji wokovu wo wote. Hakuwa Mponyaji kwao. La. Utukufu! Yeye si—Yeye si Uzima kwao, la bila shaka, wao hawakufa kamwe katika dhambi na makosa. Sisi tulikuwa tumekufa, bali tumefanywa hai. Tuko hapo. Tutasema nini tukiwa tumevua taji zetu, "Wewe ni Kasisi *Fulani*"? Loo, la, la, la, la. Utukufu wote Kwake! Naam. Haya basi. Ndipo tutasimulia hadithi ya jinsi tulivyoshinda, tutafahamu jambo hilo vizuri zaidi baadaye.

268 Halafu, humo katika jambo hilo basi, basi ni jambo gani lililotukia? Je! Mungu alisema tu basi, "Vema, afadhali tu hata niangamize shura yangu yote pamoja na kasiamu, yote imeharibiwa"? La, la, Yeye alijua ya kwamba itakuja kuwa namna hiyo. Ikiwa, basi, kama Roho Mtakatifu alinifanya jinsi nilivyo, nami ninakula chakula na kukirudisha katika mwili wangu na kujengeka kufikia nilivyo sasa, sasa, hata hivyo,

nilifanywa katika mfano. Kila picha ambayo Mungu aliona, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, inakomaa, inatokea. Unaona? Ilitokana na mwanamke, kama Yeye alivyosema ingekuwa. Wakati huo mwingine ilitoka kwa Mungu. Wakati huo ilitokana na mwanamke; inakuja wakati huu kwa njia ya Mwanamume. Unaona? Wakati huo ilikuja kwa tamaa ya kujuana kimwili; inakuja wakati huu kwa Neno lililonenwa la Mungu? Unaona?

269 Na hapo, sasa, hakuna jambo lo lote linaweza kunidhuru. La, bwana. Hakuna kitu cho chote kinachoweza kutudhuru. Kama Paulo alivyosema, “Wala hakuna vitu vilivyoko, vitu vijavyo, maradhi, mauti, hakuna kitu kinachoweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo.” Hakuna jambo lo lote linaloweza kututenganisha.

270 Kama vile nilivyosimulia hadithi moja ndogo. Nimebakiza tu nywele tano niwe upara, kabisa. Nami nilikuwa nikichana hizo chache hapa hivi majuzi, mke wangu akasema, “Billy, wewe karibu umekuwa upara.”

Nikasema, “Lakini sijapoteza hata unywele mmoja.”

Akasema, “Ziko wapi?”

271 Nikasema, “Zilikuwa wapi kabla sijazipata? Unaona, po pote pale zilipokuwa kabla sijazipata.” Sasa, kulikuwako na wakati mmoja, miaka mia moja iliyopita, nywele hizi hazikuweko hapa hata kidogo, lakini zilikuwa hapa nje katika mavumbi. Hiyo ni kweli? Ndipo yapata miaka hamsini iliyopita, zilianza kuja kwenye kichwa changu. Zilitoka wapi? Kutoka mavumbini. Na sasa zinarudi zilikokuwa. Hiyo ni kweli? Hazikuwako, kisha zikawa, na sasa haziko. Ni kitu gani? Ni kitu gani kilizifanya namna zilivyo? Mungu! Huyo hapo. Yeye alichora picha fulani, na hivyo ndivyo ninavyomtaka.

272 “Ee Mauti, uchungu wako uko wapi? Kaburi, u wapi ushindi wako?” Unaweza kunizika moja ya siku hizi kutoka hapa, sijui. Lakini, ndugu, sitakuwa maiti. Ninakwambia jambo hilo. La, bwana. Loo, tutafufuka, haleluya, tutafufuka! Kwenye asubuhi hiyo ya ufufuo wakati vizuizi vya vifo vitakapofunguliwa, tutafufuka, haleluya, tufafufuka. Hakuna kitu kinachoweza kunifanya nisifufuke. Hakuna pepo wa kutosha katika kuzimu yote wanaoweza kunifanya nisifufuke. Hakuna cho chote cha kutosha mahali po pote cha kunifanya nisifufuke. Nina ahadi ya Mungu, nina Roho Mtakatifu. Nina Zoe, Uzima wa Milele wa Mungu, unaokaa hapa. Mzoga huu wa kale ulitoka kule, ndipo Mungu akaniatamia nikatoka ardhini.

273 Na kama Yeye Ambaye ameniatamia kutoka ardhini, nitakapokuwa mtu mzima sasa, kila ninaposikia kengele ya kanisa, kitu fulani kingenena nami, Sauti ndogo sana. Malaika alizungumza kutoka kwenye kijiti, akasema, “Kamwe usinywe pombe wala kuvuta sigara, nina kazi utakayofanya. Usiuchafue

mwili wako ama kuzurura na wanawake na kadhalika, wewe, nina kazi utakayofanya utakapokuwa mtu mzima."

"Wewe ni Nani? Wewe ni Nani?"

274 "Utajua mengi zaidi kuhusu jambo hilo baadaye." Baada ya kitambo kidogo, Huyu hapa akaja, Yeye ananing'inia pale kwenye ule ubatizo. Anajidhihirisha mwenyewe. Anajitangaza. Anajibu. Ninamwona akisimama kule kila mahali, katika kila upande.

275 Utafanyaje, kama Yeye angalinifanya kile nilicho bila kuwa na hiari yo yote? Sikurudi kule na kusema, "Sasa, Charlie Branham, mwoe Ella Harvey, na unizae duniani." La, bwana. Sikuwa na chaguo lo lote juu ya jambo hilo. Mungu alifanya jambo hilo. Na kama Yeye alinifanya nilivyo mimi, bila uchaguzi, ni zaidi sana vipi wakati huyo Roho Mtakatifu anapoanza kuniatamia na mimi niseme, "Naam, Bwana, Wewe ni Muumba wangu, nami nakupenda na nakukubali kama Mwokozi wangu."

276 Utanishikiliaje mavumbini? Huwezi tu kufanya jambo hilo, ndugu, huwezi tu kulifanya. Mungu kamwe hakuumba kipande kimoja cha kalisiamu hii wala shura, ama cho chote kile, ambacho kingeweza kutu—kutupwa. "Wote alionipa Baba Yangu, kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, watakuja Kwangu." Whiu! Ninajisikia kama kupiga makelele sasa hivi. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu, wala hakuna hata mmoja wao atakayepotea, lakini nitamfufua tena katika ule ufufuo. Nilimsikia Yeye akiita, nami nikamjia. Wao wanawezaje kunishikilia katika mavumbi ya nchi? Hakuna wazishi wa kutosha duniani kunishindilia usoni na sepetu, watawahi kunishikilia kwenye mavumbi ya nchi. Nitafufuka siku moja na kusimama katika mfano Wake, nimeoshwa na Damu Yake, nimezaliwa kwa Roho Wake! Haleluya! Mwe na madhehebu yenu yote mtakayo; nitamchukua Yesu. Amina!

277 Mtu mmoja wa bima alikuja kwangu, Wilbur Snyder, rafiki msiri wangu. Akasema, "Billy, ninataka kukuuzia bima."

278 Nikasema, "Ninayo tayari." (Mke wangu akageuka na kuniangalia kama anayetaka kusema, "Mbona unadanganya, kijana?")

Kasema, "Ati una bima?"

Nikasema, "Ndiyo, bwana."

Kasema, "Ni ya kampuni gani? Ni ya nini?"

279 Nikasema, "Dhamana iliyobarikiwa, Yesu ni wangu, loo, ni malimbuko matamu namna gani ya utukufu wa Mungu! Mrithi wa wokovu wangu, nimenunuliwa na Mungu, nimezawa kwa Roho Wake, nimesafishwa katika Damu Yake."

280 Akasema, "Hiyo ni zuri, Billy, lakini haitakuzika makaburini."

281 Lakini nikasema, “Itanitoa.” Haleluya! Mimi sijali juu ya kuingia mle; ni kule kutoka.

282 Kwa hiyo, nina bima inayoniambia, “Ninaleta wote alionipa Baba Yangu, ni Wangu.” Sijali baba yangu amefanya nini, mama yangu amefanya nini, cho chote kile kilichokuwa. “Wote anaonipa Baba Yangu watakuja Kwangu, wala hakuna mtu awezaye kuja asipovutwa na Baba Yangu.” Haleluya! Kwa nini Yeye akawajua? “Nilitangulia kuwajua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Nilimpomchinja Mwana-Kondoo, nilimchinja pamoja Naye.” Amina. “Nililichagua Kanisa tangu zamani.” Ni kitu gani kilichaguliwa tangu zamani? Kanisa. Unaingiaje katika Kanisa? “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja.” Yeye alijua kabla ya kuwekwa misingi ya dunia kwamba tungekuwako. Na hao ambao alitangulia kuwajua, aliwaita. Hao aliowaita, amewahesabia haki. Wale aliowahesabia haki, tayari amewatukuza.

283 Katika Vitabu vya Mungu Yeye tayari amesema atakutana nami papo hapo. Hakuna pepo wote kutoka kuzimu wanaoweza kumweka mahali pengine po pote ila kumzuia kuja moja kwa moja pale, maana Mungu tayari amesema jambo hilo, na hilo linatosha. Kama miaka bilioni mia moja kabla ulimwengu haujaumbwa, nyota za asubuhi ziliimba pamoja, na wana wa Mungu walipiga mekelele kwa furaha, kabla ya kuwepo misingi ya dunia, unaona, kabla ya kuwepo na misingi ya dunia. Na hao Malaika na kila kitu kilifurahi, kikipiga makelele juu ya jambo hilo, kabla hapajakuwako na misingi ya ulimwengu, ibilisi ataniwekaje katika mavumbi ya nchi? Hawezi tu kufanya hivyo kamwe. Umesema kweli.

284 Hebu tuone, sasa, huu ni wakati wa demokrasia nilio nao hapa. Hii ni saa tano kasoro dakika ishirini, hiyo ni dakika ishirini tu kufikia saa nne kamili. Hiyo ni kweli, Ndugu Wood? Hiyo ni kweli, saa nne kasoro dakika ishirini. Kila mtu anafurahi?

> Loo, ninajisikia kama kuendelea na safari,
> Ninajisikia kama kuendelea na safari;
> Makao yangu ya mbinguni ni maangavu na ni
> mazuri,
> Nami najisikia kama kuendelea na safari.
>
> Loo, ninajisikia kama kuendelea na safari,
> Ninajisikia kama kuendelea na safari,
> Makao yangu ya mbinguni ni maangavu na ni
> mazuri,
> Nami najisikia kama kuendelea.

285 Mnazipenda hizo nyimbo za kale namna hiyo? Kulikuwa na mmoja wa kale tuliokuwa tunaimba juu ya, jambo fulani, kuhusu “*Neema na rehema zilinipata, hapo ile Nyota ya Asubuhi ilipoangaza*. Ni kitu gani hicho, Dada Gertie? Hebu

tuone. Vipi, ni nini, Ndugu Neville? Unaona, jambo fulani, "Neema na rehema zilinipata, hapo ile Nyota ya Asubuhi yenye Kung'aa iliponionyesha makao Yake karibu nami." A-ha, naam. *Msalabani*. Tupe sauti ya huo, dada. Hiyo ni *Karibu na Msalaba*. Njoo hapa. Loo, ninapenda hizi. Ni wangapi wanaopenda hizo nyimbo za kale zilizovuviwa? Unaweza kuwa na bugi zako za kuruka-ruka unazozitaka. Nipe hizi, hapa ndipo neema na rehema ziliponipata. Naam. Vema, uimbeni sasa.

Yesu unihifadhi,
Hapa msalabani,
Wajiao Kalvari,
Waponywe damuni.

Msalaba, msalaba,
Humu nina sifa;
Hata nitapumzika
Mahali pa Raha.

286 [Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Karibu Na Msalaba*—Mh.] Loo, jinsi unavyopendeza! Wazia jambo hilo! Vipi kama hapangekuwapo na Mwokozi? Vipi kama hatungekuwa na Neno hili? Vipi kama Yeye hakuwa amekuita? Vipi kama hangekujua tangu zamani, nawe ungalikuwa huku nje pamoja na walimwengu wengine usiku wa leo? Je! unampenda? Loo, jamani! Msisahau ibada asubuhi, sasa, saa tatu na nusu.

Msalaba, msalaba
Humu nina sifa;
Hata nitapumzika
Mahali pa raha.

287 Sasa tupe sauti ya *Nafasi Kwenye Chemchemi*. Wimbo huu mzuri wa kale, *Kuna Nafasi Kwenye Chemchemi*. Ni wangapi wanaoujua? "Nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi, nafasi kwenye Chemchemi." Na wakati unapofanya jambo hilo sasa, kwa utulivu sana, nyosha tu mkono wako karibu nawe, peana mkono na huyo ndugu. Unajua, kuna nafasi sasa kwa Wamethodisti wote, kuna nafasi kwa Wabatisti, kuna nafasi kwa Mpentekoste. Kuna nafasi kwa ajili ya sisi sote sasa, kwenye Chemchemi. Ni wangapi wanaoujua huo wimbo wa kale? Loo, hakika, mnaujua. Baadhi yenu ninyi watu wa zamani sasa, huu ni wimbo mzuri wa zamani wa Kentucky sasa.

Nafasi, nafasi, (hebu tupeane mikono), naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako;
Nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako.

Loo, nafasi, nafasi, kuna nafasi kubwa,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako;
Loo, nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako.

288 Sasa, nina kitu kidogo cha kuwashangaza. Mahubiri yote pamoja na vitabu vyote vya hivi karibuni sana na kila kitu vitakuwa vinauzwa upande ule mwingine wa kanisa, juma lijalo, kwenye mikutano. Kanda na kila kitu, na vyote katika vitabu vya hali nzuri. Kutakuwako na meza kule nyuma katika chumba kimojawapo, na vitabu, mahubiri ya karibuni sana, na baadhi ya maandishi mazuri yaliyotolewa hapo awali katika vitabu vipya, nakala mpya, vyote vitapangwa kwenye upande—upande wa nyuma wa jengo hili Jumatano hii ijayo usiku. Nasi tunatarajia wa—wakati mzuri katika Bwana. Njoni mkiomba, sasa. Sasa, waite wagonjwa wako na wanaoteseka, waandikie barua na uwalete hapa, nasi tutaninii tu. . . Mungu atatenda kazi tu kwa nguvu. Sisi tuko hapa na tunajua ya kwamba Yeye atafanya jambo hilo sasa.

289 Na sasa nimeenda kwa kila mtu niliyemjua, aliye na kitu kidogo. Kama kuna jambo lo lote lilisilo sawa sasa, ninyi kumbukeni, niliwaambia muda mrefu uliopita, tutalinyosha jambo hilo. Nami ninajua ya kwamba mnajua ya kwamba kuna roho tofauti hapa mbali na ile iliyokuwako. Mnaona? Mnaona? Mnaona? Hiyo ni kweli. Sasa, msiache iondoke tena. Ninawaagiza mbele za Yesu Kristo, msiiache iondoke. Dumuni papa hapa nayo, mnaona, nyosheni tu kila kitu na msonge mbele. Ninyi ni ndugu. Si ndugu yako ama dada yako anayetenda jambo lo lote baya, ni huyo roho wa Ibilisi anayeingia mle. Unaona, anaenda kila mahali. Nawe msikitikie tu huyo ndugu ama huyo dada, na ujue ni Shetani anayeingilia kati. Na kama unaudhika na jambo hilo, liondoe ndani yako mara moja, unaona, maana litakutafuna. Ndiyo, litakutafuna, kwa hiyo usilikaribie. Kumbuka tu.

Kuna nafasi, nafasi, nafasi kubwa sana,
Kuna nafasi kwa ajili Wamethodisti, nafasi kwa ajili ya Wabatisti,
nafasi kwa ajili ya Wapresbiteri, kuna nafasi kwa kila mtu;
Nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako.

290 Ni wangapi wanaukumbuka wimbo wetu wa kufumukana, ule, "Peleka Jina la Yesu, liwe silaha yako; litafurahisha moyo, peleka uendako"? Laiti ungaliweza kukaa pamoja nasi, Ndugu Jeffreys, wewe na Dada Jeffreys, na hawa vijana pale, na hao wote. Na—na halafu, "Watamvika taji Mbinguni kama Mfalme

wa wafalme, hapo safari yetu itakapomalizika." Loo, jamani! "Ndiye Mfalme wa wafalme, hakika ya maisha. Peleka Jina la Yesu, lipeleke kama Ngao leo. Loo, utakapojaribiwa, lilia Jina hilo Takatifu." Loo, ninalipenda hilo, hilo Jina la ajabu la Yesu. Sasa, hebu tusimame sasa hivi, tunapouimba sasa. Vema.

Peleka Jina la Yesu,
Ko kote uendako;
Litafurahisha moyo,
Peleka uendako.

Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, (Loo thamani) na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.

291 Kuna tofauti kidogo sasa. Hebu na tuinamishe tu vichwa vyetu sasa, na kwa utulivu sana tuinue mkono mmoja, tuseme:

Kwa Jina la Bwana Yesu,
Nimejiinamisha,
Ndiye Mfalme wa Wafalme,
Halika ya maisha.

Thamani (thamani), na tamu! (na tamu!)
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani (naam, thamani) na tamu! (na tamu)
Ni Jina Lake Yesu.

292 Huku vichwa vyetu vikiendelea kuinamishwa, tunasema, [Ndugu Branham anavumisha, *Peleka jina la Yesu*—Mh.]

*Kwa Nini Sisi Si Madhehebu?* SWA58-0927
(Why Are We Not A Denomination?)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 27 Septemba, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Hii tafsiri ya Kiswahili ilichapishwa mwaka wa 1999 na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1999 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org